ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaibah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
19.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
47.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe.

48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.

68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Pili – Tarehe 25 Machi, 2010

Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani ya hotuba ya Mswada wa Marekebisho ya Sheria Nam. 3 ya mwaka 1994, Sheria ya Kufuta Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe na kuanzisha Sheria Mpya ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe na kuanzisha Sheria mpya ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Hamad Masoud Hamad (Waziri Kivuli wa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe wa Zanzibar Nam. 3 ya Mwaka 1994 na kuanzisha Sheria mpya ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe na mambo mengine yanayohusiana nayo. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 76

Jengo la Baraza la Wawakilshi Pemba

Mhe. Ashura Abeid Faraji – Aliuliza:-

Serikali ina mpango gani kwa Jengo la Afisi ya Baraza la Wawakilishi Pemba, baada ya kujengwa kwa Jengo Jipya la Baraza Unguja?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora (Kny. Mhe. Waziri Kiongozi) – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri Kiongozi naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 76 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi tangu lianzishwe limekuwa likitumia jengo hili ambalo hapo kabla lilikuwa ni Klabu ya Wananchi (*Peoples Club*). Baada ya kupita miaka takriban 25 tangu Baraza lianzishwe, serikali ilifikia uamuzi wa kujenga jengo jipya ambalo ujenzi wake unaendelea huko Mbweni. Uamuzi huo umetokana na haja ya kuwa na jengo lenye nafasi nzuri ya kufanyia kazi, jengo linalolingana na haiba ya Baraza la sasa na jengo lenye utulivu na mazingira bora ya kufanyia kazi.

Mhe. Spika, baada ya jengo hilo kukamilika litahamiwa na kutumika kwa shughuli za Baraza kama linavyotumika jengo hili la hapa Kikwajuni.

Baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, jengo la Pemba litaendelea kutumika sehemu muhimu ya shughuli za Baraza Pemba, litaendelea kuwa ni Afisi ya Baraza Pemba kwa ajili ya kuratibu shughuli zote za Baraza zitakazofanyika Pemba; kutoa huduma kwa wajumbe wanaotoka Pemba na Wajumbe wanaokwenda Pemba kutoka Unguja kwa ajili ya kazi za Baraza.

Mhe. Spika, bila shaka shughuli hizo zitafanyika vyema na kwa ufanisi iwapo jengo la Baraza Pemba litakuwa katika hali nzuri. Hivyo, serikali itaendelea kulienzi jengo hilo kwa kulifanyia matengenezo yatakayohitajika kama inavyofanika sasa ambapo jengo hilo kwenye eneo la ofisi limefanyiwa matengenezo makubwa ya kuwekewa dari ya zege, kuongezwa nafasi ya ofisi sehemu ya juu na kuezekwa. Baada ya matengenezo hayo sasa tutajipanga kukabiliana na maeneo mengine yanayohitaji matengenezo ili kuliweka jengo hilo katika hali nzuri.

Nam. 66

Wafanyakazi Vibarua

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

Inasemekana kuwa kuna wafanyakazi kwenye Taasisi mbali mbali za Serikali ambao wamefanya kazi kwa zaidi ya miaka 10 bila ya kupatiwa uajiri wa

kudumu, hali ambayo inasababisha kukosa haki za waajiriwa wa kudumu kama vile malipo ya kustaafu.

(a) Je, Mhe. Waziri kwa kuwa suala hilo unalifahamu, wizara yako inachukua hatua gani kuondoa tatizo hilo?

(b) Iwapo wafanyakazi kama hao watapatiwa ajira za kudumu. Je, muda waliotumia katika ajira ya muda utafidiwa ili wafaidike zaidi na malipo ya kustaafu?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.66 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi kifungu Nam.5, Watumishi wa Serikali wanapaswa kuajiriwa katika makundi manne (4) yafuatayo:-

(i) Wafanyakazi wa Kudumu
(ii) Wafanyakazi wa Mkataba Maalum
(iii) Wafanyakazi wa Muda
(iv) Wafanyakazi wa Kutwa.

Haki na fursa zinazotawala wafanyakazi wa makundi hayo zimeelezwa katika Kanuni za Utumishi kwenye vifungu mbali mbali.

Hata hivyo, Mhe. Spika, sera ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kupunguza kwa kiasi kikubwa ama kusitisha ajira ya wafanyakazi wa kundi la tatu na kundi la nne kadiri inavyoyumkinika.

(a) Naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba nafahamu kuwepo kwa suala hili na hatua mbali mbali zinachukuliwa na serikali kuondosha tatizo hili ikiwa ni pamoja na kuwabadilisha watumishi waliomo kwenye uajiri huo na kuingizwa kwenye uajiri wa mashari ya kudumu.

Kwa mfano, hivi karibuni serikali imeshachukua hatua za kuwabadilisha wafanyakazi wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira waliokuwa katika masharti ya uajiri huo.

(b) Kwa mujibu wa utaratibu wa watumishi waliokuwa katika ajira hiyo kabla ya kupatiwa ajira ya kudumu, serikali

inachukua muda walioutumia katika masharti wanayotoka pamoja na muda wakuutumia kwenye masharti ya uajiri wa kudumu na kuzingatiwa haki zao wakati wa kustaafu.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza. Katika jibu mama amekiri kwamba bado wapo wafanyakazi wa muda na wa kutwa hawajaajiriwa kuwa wa kudumu. Je, zoezi hili litachukua muda gani ili tuondoshe tatizo hili?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, labda nieleze tu kwamba kuna baadhi ya wizara kwa hali ya kazi zao lazima wanakuwa nao hawa vibarua, yaani mkataba wao ni wa muda tu. Lakini kosa tulikuwa tunalifanya huko siku za nyuma kwamba tunawaachia wanakuwa kama wa kudumu sasa, wale wanatakiwa kila baada ya miezi mitatu wanaachishwa huo ndio utaratibu wake. Sasa kwa *nature* ya kazi nyengine kama za kilimo kwa kweli lile huwa haliondoki moja kwa moja, lakini lazima zile taratibu zifuatwe.

Sasa wale niliosema wengine ambao ni wa muda tunajitahidi kwa mikataba maalum, wale inakuwa ni kwa mikataba maalum wanaajiriwa basi ikisha mikataba yao wanaambiwa ahsante na chake anapewa.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Waziri naomba ruhusa anisaidie kujibu swali moja la nyongeza. hawa wafanyakazi wa kudumu, wa mikataba lakini pia kuna watu huwa wameshastaafu wakawa wanaajiriwa kwa mikataba. Sasa Mhe. Waziri hivi kwa nini sasa hivi tuendelee na kuwachukua watu kwa mikataba wakati vijana, wasomi, tunao wengi hawana ajira na tunaajiri hawa ambao wameshastaafu na kuwanyiima nafasi wale vijana wetu wapya.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, nafikiri Mhe. Haji Mkema nilisema kwenye jawabu langu mama, kwamba lengo la serikali ni kupunguza kwa kiasi kikubwa au ikiyumkinika ni kusitisha kabisa ajira za wafanyakazi wa muda na wafanyakazi wa kutwa. Lakini lazima tukumbuke na ndio hali halisi, inabidi kwa kweli hawa wafanyakazi wa mkataba hatuwezi kuwaacha moja kwa moja, kuna taaluma nyengine kama madaktari, wauguzi, hata walimu wazoefu na wataalamu wengine.

Kumsomesha daktari tu miaka mitano ende *internship* na uzoefu na bado tunahisi anaweza kufanya kazi, basi kwa mapendekezo ya wizara ndio tunawachukua, na wako wengine tunawaifa ma-*specialist*, lakini ndio

wameshafikia umri wa kustaafu. Sasa bado tunatoa fursa kubwa kwa vijana wapya. Lakini hata hivyo, kutokana na uzoefu na matakwa ya ajira tuliyonayo serikalini inabidi kama nilivyosema twende nao hawa wengine.

Nam. 64

Viashiria vya Utawala Bora

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

Inasemekana wizara yako ipo katika harakati za kuanzisha viashiria vya Utawala Bora Zanzibar kwa lengo la kuweza kupima utekelezaji wa malengo yanayohusiana na Utawala Bora.

(a) Je, Mhe. Waziri suala hili ni kweli?

(b) Kama ni kweli kazi hiyo itafanywa kwa utaratibu gain?

(c) Je, Mhe. Waziri zoezi hilo litachukua muda gani kukamilika?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 64 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kutoa majibu kwanza naomba kuanza kwa maelezo mafupi kama ifuatavyo:

Miongoni mwa malengo ya msingi ya wizara yangu ni pamoja na kuimarisha Utawala Bora hapa Zanzibar. Wizara yangu imebaini kwamba kwa kipindi kirefu haikuwa na viashiria/vigezo ambavyo vingeweze kutumika katika kujitathmini kwa kiasi gani imefanikiwa katika kuimarisha misingi ya Utawala Bora. Katika lugha ya kawaida viashiria ni alama/vigezo ambavyo vinaweza kutumika katika kujitathmini kwa kiasi gani wizara imefanikiwa katika kuimarisha misingi ya Utawala Bora hapa Zanzibar. Vigezo ambavyo vitaweza kutoa ishara juu ya utekelezaji kuona kama hapa nchini utawala wa sheria unatumika, matumizi ya serikali yanafuata kanuni, ushirikishwaji wa wananchi katika uendeshaji wa nchi na kadhalika.

Baada ya maelezo haya sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba Wizara imo katika harakati za kuanzisha

viashiria vya Utawala Bora Zanzibar kwa lengo la kuweza kupima utekelezaji wa malengo yanayohusiana na Utawala Bora.

(b) Kazi hii inafanyika kwa kuajiri wataalamu wa ndani kwa kuandaa viashiria hivyo na kisha itawasilishwa kwa wadau mbali mbali wa Utawala Bora kwa lengo la kuvipatia na kupata maoni yao kwa kuiboresha zaidi kazi hiyo.

Hatua itayofuata baada ya hapo ni kuichapisha na kuvisambaza kwa wadau mbali mbali kwa ajili ya kutumika.

(c) Kazi ya utayarishaji wa viashiria vya Utawala Bora imeshaanza na inatarajiwa kukamilika si zaidi ya miezi mitatu (3).

Mhe. Haji Faki Shaali: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipatia fursa hii. Kwanza namshukuru Mhe. Waziri kwa kueleza dhamira nzuri ya kuweka hivi viashiria vya utawala bora hapa Zanzibar. Lakini mimi swali langu ni kwamba, kwa kuwa tayari vipo viashiria vya *APRM* ambapo Tanzania ni mwanachama na wanafanya tathmini ya utawala bora. Matokeo ya miaka miwili ya nyuma inaonekana Zanzibar au Tanzania hatuko katika *position* nzuri. Sasa ikiwa tunashindwa kutekeleza hivi vigezo vya *APRM* kujisawazisha kwa yale makosa tunayoyaona. Hivyo kutakuwa na umuhimu gani kuanzisha vigezo vyetu.

Lakini la pili hivyo vigezo vyetu tutakavyoviweka kweli vitakuwa katika *standard* ya vigevyo vya kimataifa. Kwa sababu kuna vigezo vinavyotumiwa na *World Bank, World Wide Global Indicator*, kuna hivi vya *APRM*. Sasa mimi nina wasiwasi na Mhe. Waziri labda anitoe wasi wasi, hivi vigezo local tatakavyojiwekea sisi wenyewe havitakuwa vigezo vya kienyeji tunavyojipendelea na kuleta tathmini ambayo si ya ukweli.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, nakubaliana na yeye kwamba kweli vipo viashiria vinavyotumika na *APRM*. Viashiria vya *APRM* vinakwenda katika eneo pana kabisa la Afrika nzima na nchi kwa kawaida zinakuwa zinatofautiana katika hali yake na uelewa wake. Napenda kumtanabahisha tu kwamba ripoti ya kwanza ambayo imeshatoka katika *APRM* na imeshasambazwa tumeshaona pale kiasi gani na sisi Zanzibar tunatakiwa kutekeleza ili kwenda katika hali hiyo ya kwamba tunatekeleza huo utawala bora. Kwa hivyo, hilo nakubaliana naye.

Lakini vigezo ambavyo tunataka kuvitumia hapa ndani yeye anasema kwamba vitakuwa katika *standard* au vitakuwa vya kuripua ripua! Napenda kumwambia kwamba vitakuwa vigezo vinavyofanana na vile ambavyo vinatekelezeka. Kwa

sababu jambo la kwanza lazima wananchi wajue hivyo vigezo vyenyewe na lazima tuwaelimishe wavielewe hivyo vigezo vyenyewe. Kwa sababu utekelezaji wa utawala bora haufanywi na wizara moja ni *cross cutting* vyombo vingi na idara nyingi zinahusika katika utekelezaji wa masuala hayo.

Nam. 26

Huduma za Minara ya Simu

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Zanzibar imebahatika kuwa na kampuni kadhaa zinazotoa huduma za simu.

(a) Ni kwango gani cha fedha huchangiwa na makampuni hayo kwa mwaka na kuingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali?

(b) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) inasaidia vipi Zanzibar kuboresha huduma za mawasiliano na kuongeza mapato?

(c) Lipo tatizo la baadhi ya minara ya baadhi ya Kampuni za Simu kuwa na huduma mbovu za mawasiliano (*Network Coverage*) mfano mnara wa *Tigo* uliopo Mtambile unapatikana zaidi maeneo ya Nungwi na haupatikani kabisa maeneo ya Mtambile, Kengeja, Mwambe, Kangani na kadhalika. Tatizo kama hilo linasababishwa na nini? Je ni kwa nini hali hiyo isirerekebishwe?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuhudhuria Kikao cha Baraza ili kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 26 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kiwango cha mchango wa Kampuni ya Simu katika Mfuko Mkuu wa Serikali unashughulikiwa na Hazina kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi ambayo ndiyo yenye Mamlaka ya kukusanya mapato ya nchi toka vyanzo mbali mbali vikiwemo viwango vya kodi na visivyo vya kodi.

(b) Mamlaka ya Mawasiliano imeisaidia Zanzibar kuboresha huduma za mawasiliano na kuongeza mapato kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Ufunguzi wa Afisi ya Zanzibar ili kusimamia masuala yote ya mawasiliano yakiwemo ubora, utatuzi wa matatizo, uchambuzi wa hali ya hewa na maombi ya leseni, kuchangia huduma za kijamii pamoja na kutoa ajira.

(ii) Utoaji wa leseni kwa Makampuni mbali mbali ya Zanzibar, kuyawezesha kutoa huduma Tanzania Bara na Visiwani ili kuongeza ushindani ambao unawezesha kutoa huduma bora kwa gharama nafuu.

(iii) Pia utoaji wa leseni hizo umewezesha makampuni kadhaa kuchangia gharama mbali mbali za serikali kwa mujibu wa sheria, utoaji wa ajira na kurahisisha mawasiliano kwa kusaidia wananchi wa Zanzibar uchambuzi wa kutoa huduma bora kati ya watoa huduma walioko sokoni.

(c) Matatizo ya mawasiliano yanayosababishwa na minara yanashughulikiwa mara tu baada ya kupata taarifa ya tatizo husika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

(a) Kwa kuwa amekiri kwamba *TCRA* ni chombo cha Muungano na kimefungua afisi yake hapa Zanzibar, ningetaka nijue katika afisi ya Zanzibar ni Wazanzibari wangapi wameajiriwa hadi hivi sasa.

(b) Kwa kuwa amekiri kuwa matatizo ya minara hufumbuliwa baada ya kupatikana tatizo hilo, tangu mnara wa Mtambile ujengwe ni takriban miaka mitano. Kwa nini hadi sasa hayajatatuliwa matatizo yale.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba *TCRA* ni taasisi ya Muungano ambayo pia ina afisi zake Zanzibar. Kwa Zanzibar wafanyakazi karibu wote wanatoka Zanzibar.

Kuhusu mambo mengine ambayo aliuliza Mheshimiwa katika swali lake la msingi ni kwamba *TCRA* kila mwaka wanatoa michango kwa jamii hapa Zanzibar, ambayo kila mwaka inakuwa inakaribia shilingi milioni 15 na zaidi. Kwa mfano, mwaka jana walichangia hospitali ya Cheju shilingi milioni 11 na walitoa shilingi milioni 5 kwa Skuli ya Kiembesamaki na waliwachangia watoto 2 walioingia Chuo Kikuu Tunguu U$ dola 1,600.

Kwa mwaka huu mamlaka hiyo imetoa msaada wa shilingi milioni 7.5 kwa Skuli ya Chwaka, shilingi milioni 6 kwa Skuli ya Kidoti na shilingi milioni 2

kwa Kituo cha Afya cha Mtambwe na shilingi milioni 1.5 kwa *saccos* ya Sharifumsa.

Kuhusu mnara huo ambao umejengwa kwa muda mrefu, lazima tukiri kwamba miaka ya nyuma kabla ya mwaka jana kampuni za simu zilikuwa zikijenga minara kiholela, lakini baada ya kubaini tatizo hilo Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi imeunda kamati ambayo inawashirikisha wataalamu kutoka Wizara ya Ardhi, Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ, hiyo Mamlaka yenyewe ya *TCRA* na afisi yetu ili kudhibiti uanzishwaji wa minara kiholela lakini pia kupokea malalamiko kama ya Mhe. Hija Hassan ambayo tutayafanyia kazi ili kuondoa tatizo hilo.

Lakini pia tukumbuke kwamba, wenye kujenga minara hawa ni kampuni binafsi, kampuni nyengine zilitaka kuanza lakini kama zimesua sua na kufilisika. Kwa hivyo, mamlaka haiwezi kwenda kujenga mnara isipokuwa kuwataka wamiliki wa minara wairekebishe. Sasa kampuni kama imeshindwa itakuwa hakuna la kufanya.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa sasa *ZANTEL* inaonekana kwamba mawasiliano yake hayatoki vizuri, lakini yote inasemekana kwamba inatokea migongano baina ya mnara huo na minara mingine. Hata yale maeneo ambayo yana minara mingi kama ukanda wa Matemwe – Kiwengwa, basi pia panakuwa na matatizo ya mawasiliano kwa *ZANTEL*.

Mhe. Spika, naomba niulize swali (a) na (b).

(a) Nini tatizo linalopelekea kwamba kupelekea mgongano baina ya minara na minara na wateja kukosa mawasiliano?

(c) Nini faida ya wanavijiji wale ambao wana minara mingi wakati inapowekezwa hakuwekwi mikataba baina ya kijiji na mwekezaji bali inawekeana mikataba baina ya serikali na mwekezaji? Je, lini hawa wananchi watapata faida moja kwa moja tukiacha wale watu ambao wamemiliki ile sehemu lakini kama jimbo au wadi wanafaidika vipi?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kwanza haijathibitika hasa kwamba wingi wa minara ndio unaosababisha mgongano wa mawasiliano. Lakini kama ni *ZANTEL* kuna tatizo la mawasiliano nafikiri kuna kipindi wao wenyewe walikiri na wamesema timu yao ya wataalamu inalifanyia kazi suala hili ili kulimaliza. Unajua kila wakipata wateja wengi wanakuwa na matatizo kidogo ya mawasiliano pengine kutokana na uwezo wao

wa wateja, lakini wamejitahidi sana sasa hivi kidogo kurekebisha matatizo yao.

Kuhusu vijiji ambavyo vina minara mingi na hawanufaiki. Kwanza serikali haiingii mkataba na mwekezaji kuhusu ujengaji wa minara, kazi hii kwanza inaanzia kwa mwenye eneo, ndiye ambaye anazungumza na mwekezaji, wanalipana huko baadae nafikiri wanalipa na Halmashauri ya Mji au Manispaa kwa kuruhusiwa kuweka hicho kitu. Kuna kipindi sisi wenyewe tulikuwa tukiwakatalia watu kwa sababu nakumbuka kuna sehemu za Kwamtipura mtu ndani ya nyumba yake alitaka kuweka mnara na akakubaliana kuwa uwekwe mnara na kwa sababu ni nyumba yake na yeye mwenyewe atakuwa mlinzi wa mnara.

Kwa hivyo, alikuwa anataka kupata faida mara mbili, kwamba yeye eneo lake lakini na mlinzi atakuwa yeye kwa sababu ni ndani ya nyumba yake. Sisi huwa tunapinga suala hili kuwa sio zuri, kwa sababu mtaani kati kati ya mtaa, ingawa mpaka sasa hawajathibitisha madhara ya mnara lakini tulipinga kwa sababu kelele za jenereta na mambo mengine kati kati ya mtaa.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. *TCRA* kwa sababu ni chombo cha Muungano na *TCRA* ndicho chombo kinachosimamia ugawaji wa mawimbi aidha redio au televisheni. Je, kwa Zanzibar tuna magari mangapi ya kusimamia matatizo hayo? Kama hatuna kwa sababu wana magari zaidi ya matatu na chombo hiki ni cha Muungano, lini watatupatia angalau gari moja ili kusimamia masuala hayo ya mawimbi?

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kwa upande wa Zanzibar *TCRA* hawagawi hayo mambo ya redio na televisheni, hapa nafikiri kuna Mamlaka ya Utangazaji ambayo iko chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ndio ambao wanafanya kazi hiyo.

Nam. 52

Matokeo ya Mtihani wa Darasa la Saba na la Kumi

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

(a) Je, ni skuli ipi Unguja na Pemba iliyochukua ushindi wa jumla kwa mtihani wa *Form II* na darasa la saba?

(b) Je, ni skuli ipi ya mwisho kwa matokeo Unguja na Pemba?

(c) Ipo taarifa kwamba baadhi ya skuli wamefutiwa matokeo, ni skuli zipi

na ni kwa sababu zipi?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali nambari 52 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, skuli bora katika mtihani wa Kidato cha Pili kwa mwaka 2009 ni Skuli ya Ukongoroni, Wilaya ya Kusini Unguja na skuli bora katika mtihani wa darasa la saba ni Skuli ya Wazazi Amani, Wilaya ya Mjini, Unguja. Skuli zilizofuatia katika mtihani wa Kidato cha Pili ni Skuli ya Uwandani Wilaya ya Chake Chake, Pemba. Mshindi wa pili ni Skuli ya Kajengwa, Wilaya ya Kusini, Unguja. Kwa upande wa Mtihani wa Darasa la Saba, mshindi wa pili ni Skuli ya Mitiulaya, Wilaya ya Wete, Pemba na Skuli ya Kisiwandui, Wilaya ya Mjini Unguja.

(b) Skuli iliyofanya vibaya sana katika mtihani wa Kidato cha Pili ni Skuli ya Matemwe, Wilaya ya Kaskazini "A" Unguja ikifuatiwa na Skuli ya Langoni Wilaya ya Magharibi, Unguja na skuli ya tatu kwa matokeo mabaya ya mtihani wa Kidato cha Pili ni Skuli ya Kombeni Wilaya ya Magharibi, Unguja.

Kwa upande wa mtihani wa Darasa la Saba, skuli iliyokuwa ya mwisho ni Skuli ya Kibuteni, Wilaya ya Kusini, Unguja ikifuatiwa na Skuli ya Gana Wilaya ya Kati, Unguja na Skuli ya Kandwi na Kinyasini Mkoa Kaskazini Unguja.

(c) Mhe. Spika, jibu © nimelijibu katika swali Nam. 51 nililojibu jana na jibu lake ni kama nilivyojibu jana.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza nakiri kwamba katika skuli ambayo imefanya vibaya kwa mara ya pili ni Skuli ya Matemwe. Kosa hili limetokezea mara hii ya pili lakini tulijaribu kuielekeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuwa iwapeleke wakaguzi mara kwa mara ili kuona tatizo ni nini? Lakini ukiielekeza wizara ipeleke wakaguzi inakwambia Mwalim Mkuu anafaa kuwa mkaguzi.

(a) Je, hivyo wizara bado inaridhika kwamba Mwalim Mkuu peke yake ndie mkaguzi? Kama hairidhiki itapeleka wakaguzi lini?

(b) Kuna tatizo la ajira. Wananchi wengi wa Matemwe waliomba kwamba waajiriwe wale vijana ambao wamezaliwa kule kwa

sababu hawa wanaotoka mjini na Makunduchi wanafika kwa wakati sio, wanafika skuli saa nne wanarudi saa sita. Je, Mhe. Waziri wanafunzi hawa watafanikiwa kama mwenendo wa walimu ndio huo?

(c) Skuli ya Kandwi kwa muda mrefu imejenga nyumba ya walimu ili kupunguza tatizo na ilifika sehemu ambayo ilibakia kwamba wizara ikamilishe. Hivyo, nyumba ile ya walimu Kandwi wizara itakamilisha lini? Na kama haikamilishi kwa muda huu bado eneo la Kandwi matokeo itakuwa ndio hayo hayo ambayo hayapendezi kutangazwa katika Baraza.

Mhe. Spika: Naona Mhe. Ame Mati Wadi amejipapatua vya kutosha.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, wizara ina utaratibu wa kupeleka wakaguzi kila baada ya muda katika maskuli yetu. Mimi mwenyewe binafsi nimeshuhudia matatizo ya skuli hizo alizozizungumzia ikiwemo Skuli ya Matemwe.

Mhe. Spika, kwa kawaida wakaguzi huwa wana utaratibu maalum wa kukagua na katika baadhi ya skuli ambazo amezitaka Mhe. Mwakilishi wakaguzi tayari wameshapita na tunaendelea kupeleka wakaguzi na kuona matatizo ambayo yamo katika skuli hizo.

Jibu (b) Mhe. Spika, kuhusu ajira. Mhe. Spika, kama utakumbuka hivi sasa tuna mchakato wa kuajiri walimu katika Wilaya ya Kaskazini ‘A’ Unguja, Wilaya ya Kaskazini ‘B’ na Wilaya za Pemba ikiwemo Micheweni na Mkoani. Mhe. Spika, mchakato huo tayari umeshakamilika na walimu ambao walitarajiwa kuajiriwa ni wale ambao wanaishi katika maeneo yenye matatizo. Hayo ndio tuliyoyazingatia kwa mwaka huu na wao wenyewe walikuwa ni washiriki wa kuchagua vijana ambao walitakiwa waajiriwe katika maeneo hayo. Kama kuna makosa yamefanyika basi tushirikiane tuone kwamba makosa hayo tunayarekebisha.

Mhe. Spika, kuhusu nyumba ya mwalimu Kandwi. Napenda nimhakikishie tu Mhe. Mwakilishi kwamba wizara inalielewa tatizo hilo na inafanya jitihada ya kuweza kuikamilisha nyumba hiyo.

Mhe. Mohamed Ali Salim: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa baada ya mitihani hupaswa kufanywa uchunguzi kuonekana ni kitu gani kilichosababisha skuli ama ifanye vizuri au ifanye vibaya.

(a) Je, wizara imeshalifanya hilo?

(b) Kama imelifanya hilo imegundua ni mambo gani yaliyosababisha skuli nyengine zifanye vizuri na skuli nyengine zifanye vibaya?

(c) Ili kuzifanya na skuli zilizofanya sio vizuri zifanye vizuri, haionekani kama kuna haja ya hizi skuli zilizofanya vizuri kupewa tunza. Kama wizara inatoa tunza, ni tunza gani inazozitoa?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, suala la skuli kufanya vizuri au kufanya vibaya inategemea mambo mbali mbali ambayo yanaizingira skuli ile yakiwemo kama haya ambayo nitakayoyataja.

La kwanza ni matatizo ya walimu, la pili ni jitihada ya wanafunzi na la tatu wazee kwa kiasi fulani nao wanachangia ama kufanya vizuri au kufanya vibaya. Jengine ni suala la vifaa ambalo pia linaweza likachangia kufanya vizuri au kufanya vibaya.

Lakini kwa ufupi ni kwamba sisi tumefanya uchunguzi na jitihada za kurekebisha mambo hayo tayari tumeshazichukua ikiwemo hili la walimu ambao hivi karibuni tumeanza kuwaajiri katika maeneo ambayo yanaonekana yana upungufu mkubwa ikiwemo Skuli ya Matemwe na skuli nyengine ambazo pia zinaonekana zimefanya vibaya.

Mhe. Spika, jambo jengine kuhusu mambo hayo sikulipata vizuri swali lake la pili lakini nadhani alizungumzia kwamba kuna mambo gani ambayo yanasababisha skuli nyengine zifanye vizuri na skuli nyengine zifanye vibaya. Nadhani ndio kama hili ambalo nimejibu kwamba ni walimu, wanafunzi, vifaa pamoja na wazazi nao wanaweza wakachangia kufanya vizuri au kufanya vibaya.

Kuhusu tunza Mhe. Spika, kila mwaka nadhani tunakuwa na Siku ya Elimu ambapo pale nadhani skuli bora huwa zinazawadiwa zawadi mbali mbali zikiwemo za fedha.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, katika utaratibu wetu hapa chombo hiki tunatakiwa kuzungumza maneno yaliyo sahihi. Kwa hivyo, naomba ruhusa katika kauli ya Mhe. Naibu Waziri kufanywe masahihisho. Ukongoroni kataja iko Wilaya ya Kusini, kiutawala ni Wilaya ya Kati. Naomba kuwasilisha taarifa hii.

Mhe. Spika: Tunamnyang'anya ile sifa nzuri kuipeleka Wilaya ya Kusini kumbe iko Wilaya ya Kati ambayo yeye anakaribiana nayo. Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja nafikiri ndio yenyewe.

Mhe. Ali Denge Makame: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri anafahamu kwamba baadhi ya wanafunzi wengi katika kipaji chao cha kufanya mitihani vizuri ni kupata walimu wa sayansi. Hapa petu Zanzibar kuna baadhi ya skuli nyingi hazina walimu wa sayansi ambapo wanafunzi wa sayansi wapo.

(a) Je, huoni hili linachangia wanafunzi kutokufanya vizuri mitihani yao katika maskuli?

(b) Kwa kuwa anafahamu walimu wa sayansi kuna upungufu. Je, ana mpango gani wa kuongeza walimu wa sayansi katika maskuli yetu hasa Skuli ya Kwamtipura?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nafahamu vizuri umuhimu wa walimu wa sayansi katika skuli zetu. Pia nafahamu kwamba bado tuna tatizo la walimu wa sayansi hapa Zanzibar. Mhe. Spika, pia napenda ieleweke kwamba tatizo la walimu wa sayansi si Zanzibar peke yake lakini liko katika dunia nzima.

Mhe. Spika, wizara yangu inajitahidi kuona kwamba tatizo hili linaondoka kwa kutoa fursa mbali mbali ya vijana wetu ambao wenye sifa ya kujifunza katika vyuo vyetu mafunzo ya ualimu kikiwemo Chuo Kikuu cha Taifa.

Lakini pia hivi karibuni tumekuwa na madarasa maalum ambayo tumeyaandaa pale Chuo cha Kiislam kwa ajili ya wanafunzi wa sayansi ili kuweza kuondoa tatizo hili.

Mhe. Spika, tatizo kubwa tulilonalo hivi sasa ni wanafunzi wenyewe wa sayansi kupendelea kusoma mafunzo haya ya ualimu ni tatizo kwa Zanzibar. Hatuna wanafunzi wa kutosha ambao wanapenda kusoma masomo haya ya sayansi hivi sasa na ndio maana kwamba tunakabiliana na tatizo hili.

Nam. 40

Timu ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes)

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Hivi karibuni Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Zanzibar (Zanzibar Heroes) ilishika nafasi ya tatu katika Mashindano ya Afrika Mashariki na Kati ya Wachezaji Wakubwa (Senior Challenge Cup) yaliyofanyika nchini Kenya.

(a) Mhe. Waziri, Zanzibar Heroes mbali na zawadi walizopewa kwa ushindi huo kwa utaratibu wa *CECAFA*, kwa upande wake serikali imewapa zawadi gani wachezaji hao ili kuwatia moyo wafanye vizuri zaidi mashindano yajayo?

(c) Kwa kuwa kocha aliyeifikisha hapo timu yetu ni mzalendo, utakubaliana nami kuwa Zanzibar haina haja ya kuchukua kocha wa nje ya nchi bali ni kuwaendeleza makocha wetu wakuze taaluma zao wafanye vizuri zaidi siku zijazo?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 40 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kuwa Timu yetu ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes) ilishika nafasi ya tatu katika mashindano ya Afrika ya Mashariki na Kati ambayo maarufu yanaitwa Senior Challenge Cup na kuwabwaga vigogo wengine wengi kwa mashindano hayo.

(a) Mhe. Spika, mbali na sifa walizozipokea kutoka sehemu mbali mbali ikiwemo Afisi ya Ubalozi wetu nchini Kenya kutokana na ushindi na kiwango kikubwa cha uchezaji, wachezaji hao pia waliweza:

(i) Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iliizawadia timu ya Zanzibar Heroes Dola za Kimarekani 13,700 kama motisha ili wafanye vizuri zaidi, kabla hawajafikia hata hiyo nusu fainali.Fedha hizo zilitoka moja kwa moja kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

(ii) Uongozi wa Wizara uliandaa mapokezi ya aina yake kwa timu yetu iliporejea hapa nchini ambapo wananchi na viongozi wa Serikali na Vyama mbali mbali walishiriki katika mapokezi hayo wakiongozwa na Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Mhe. Ali Juma Shamuhuna.

(iii) Mhe. Rais wa Zanzibar aliwapa heshima maalum wachezaji wa timu hiyo kwa kuwakaribisha Ikulu na kula nao Chakula cha Mchana pamoja na kuwapa motisha zaidi ya kufanya vizuri katika michezo ijayo.

(b) Mhe. Spika, Timu yetu ya Zanzibar Heroes ni matunda ya jitihada za Serikali kuandaa timu za vijana. Wengi kati ya wachezaji walioshiriki

mashindano hayo ya Challenge ya mwaka 2009 ni wale vijana waliokuwa wakifundishwa na Kocha kutoka Misri Ndugu Badr el Din ambaye aliiwezesha timu yetu kupata nafasi ya maandalizi nchini Misri kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo. Kocha huyo alimaliza muda wa mkataba wake kabla ya Kombe la Challenge na nafasi hiyo kuchukuliwa na Kocha mwenzake kutoka huko huko Misri Ndugu Abdilfatah

Mhe. Spika, ni kweli mashindano ya Challenge ya mwaka 2009 yalikuwa na walimu wazalendo wawili pamoja na mwalim mmoja kutoka Misri. Mwalim wa Misri alikuwa Ndugu Abdilfatah ambaye alishirikiana na Kocha mzalendo Ndugu Morocco.

Mhe. Spika, ili tuweze kupiga hatua zaidi za kimaendeleo katika mchezo wa mpira bado tunahitaji utaalamu mkubwa kutoka nje sambamba na kuwaendeleza kitaaluma makocha wetu ili wapate ujuzi zaidi wakufundisha vijana wetu hapa nchini Zanzibar, kutokana na taaluma na uzoefu wa wakufunzi na walimu kutoka nchi za nje na hususan nchi zilizoendelea kisoka kama vile Misri (Egypt) ambao hivi sasa ni mabingwa wa Bara hili.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuthamini michezo Zanzibar. Baada ya pongezi hizo naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa timu yetu imeonesha kiwango kikubwa cha mchezo. Je, wizara itachukua juhudi gani kumshawishi Kocha Maximo ili Wazanzibari waingie kwenye Timu ya Taifa ya Tanzania?

Swali (b) juhudi gani itafanywa kwa Kocha Morocco ili sasa apatiwe uwezo maalum wa kwenda kujifunza nje ili hatimaye michezo tuweze kushika hapa Zanzibar?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwanza kabisa tunapokea pongezi za moja kwa moja kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambazo naamini zitafikishwa na Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kwake yeye Mhe. Rais akiwa pia ni Naibu Waziri Kiongozi.

Mhe. Spika, jibu (a) Zanzibar mara nyingi huwa haisemi maneno yake kwa maneno huwa inasema kwa vitendo. Kocha Maximo baada ya yote ambayo amezungumza kule juu ya Timu ya Zanzibar katika hiyo *Challenge* basi

vitendo vimethibitisha nafasi ya Zanzibar ambayo imepata kupitia hawa hawa makocha wetu.

Kwa kuwa tunajibu kwa vitendo hatujibu kwa maneno, juzi wakati tunakwenda Pemba ziara pamoja na Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Mama Shadya Karume wakati tunafungua viwanja vyengine vya michezo kwenye mchezo wa *basketball* tukamkuta Maximo kisiwani Pemba na nadhani taarifa zake zilitoka kwenye gazeti la Zanzibar Leo. Tukauliza anafanya nini Pemba? Tukaambiwa amekuja kusaka vipaji baada ya kupata vipigo huko vya Timu ya Taifa ya Zanzibar.

Kwa hiyo, amepata mafunzo ya kivitendo zaidi ya kuona kile kipaji kilichoko hapa Zanzibar na hivi sasa wao wenyewe katika program zao TFF wameshaona kwamba hawawezi kukosa wachezaji kutoka huku. Kwa hiyo, wanajipanga na kuja kimya kimya kutafuta vipaji huku tofauti na vile walivyokuwa wakifanya awali kupitia Yanga na Simba ambapo wachezaji wa Zanzibar walikuwa wanapata nafasi kupitia timu hizo mbili, lakini sasa wanakuja moja kwa moja.

Kwa hiyo, kila tukiendelea kufanya vizuri zaidi basi wachezaji wetu watalazimika wenzetu kutoka Tanzania Bara kuwachukua katika Timu ya Taifa ya Tanzania na huenda tukaishia siku moja kama ilivyokuwa mwaka 1968/69 Timu ya Taifa ya Tanzania nzima ilikuwa na wachezaji wote kutoka hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, jibu (b) kwa makocha hawa ambao wanatusaidia wazalendo tunaendelea na jitihada za kuwatafutia nafasi mbali mbali za kwenda kupata masomo nje ya nchi na jitihada hizo bado zinaendelea kufanywa na wizara, mara tu zitakapopatikana nafasi hizo tutahakikisha wale makocha wazalendo ambao wamesaidia kufikisha timu katika *standard* iliyokuwepo sasa hivi kama vile Morocco na wao wanapatiwa nafasi hizo.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza mimi nawapongeza walimu wa timu ambazo zimetuletea sifa na kuwa historia kubwa katika nchi yetu. Mmoja wapo katika mwaka 1995 ndugu yetu Kocha Hafidh Badru ambaye kwa ujasiri wake na uzalendo na wachezaji wetu ambao walikuwa mahiri walituletea Klabu Bingwa ya Afrika Mashariki na Kati hapa Zanzibar. Kwa hivyo, nampongeza na kielelezo tosha wenzetu hawa walipokelewa kwa shangwe na kupata zawadi ambazo hawatozisahau maisha yao, kila mchezaji alipata vespa.

Mhe. Spika, la pili nimpongeze sana Kocha Hemed Morocco pamoja na wasaidizi wake na wachezaji wetu kwa kutuletea sifa ya kuwa timu bora ya tatu

katika mashindano haya yaliyopita ya Afrika Mashariki na Kati, hasa tukizingatia kwamba Hemed Morocco ni kocha mzalendo, kijana wetu kasoma hapa hapa hakwenda nje. Kamshinda kocha mwenye sifa na taaluma za kila aina ndugu yetu Maximo, Kocha wa Timu ya Taifa ya Tanzania.

Mhe. Spika, kwa mfano kama timu ya Simba imepata ubingwa hivi sasa lakini ubingwa ule hautonoga mpaka nimfunge mtani wangu Yanga. Kama atanifunga Yanga nitakuwa sina sherehe ya ubingwa. Kwa hivyo, sisi ilikuwa huu ushindi wa tatu kumshinda Tanzania Bara ilikuwa inatosha kama tumeshinda katika mashinda ya Afrika Mashariki na Kati.

Je, Mhe. Waziri pamoja na ubora wote huo, pamoja na uzalendo wote ambao wenzetu hawa wametuonesha ili kuendeleza vipaji vya wachezaji na makocha wetu. Hivyo, serikali pamoja na kuzingatia kwamba tunapendekeza zaidi makocha kutoka nje kwa taaluma zaidi. Hatuoni ni fahari kwenda kuwasomesha wazalendo wetu ili wapate taaluma na wakatuletea sifa kama hizi.

Swali (b) tutazame Misri katika mashindano yote yanayoendelea kocha wao huyo anaitwa Al-Shihata, Shihata huyo huyo anaileta sifa timu hiyo mpaka hii leo anawashinda hao wenye *madigrii* na *madiploma* kutoka nchi mbali mbali. Mhe. Spika, hatuoni fahari hiyo tukaitumia kuwasomesha vipaji walimu wetu ili tukapata sifa kama hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nikubaliane nae na melezo yote aliyotoa, pongezi kwa Kocha Hafidh Badru pamoja na mambo mengine yote ambayo yamefanyika hapo awali, yote ni katika jumla ya kudumisha michezo.

Kweli Mhe. Spika, hivi sasa Simba inaongoza Ligi Kuu ya Tanzania. Pia ni kweli tunaweza kusema ameshashinda tayari kama bingwa. Lakini ubingwa huo utaingia uchungu Mwenyezi Mungu akitujaalia Jumamosi wakati ile mechi waliyotarajia ya kushinda basi wakija kufungwa, nadhani ubingwa huo utakuwa mchungu lakini watakuja kusherehekea kwa ubingwa.

Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi pia amechukulia mfano wa huyu kocha wa Misri. Mhe. Spika, hivi karibuni nilikuwa napitia ile rekodi yake wanasema ni kocha ambaye amevunja rekodi karibu ya dunia nzima kwa sababu ameshiriki mfululizo katika Kombe la Dunia mara tatu na katika Afrika amechukua ushindi mara tatu. Kwa hiyo, amevunja rekodi ya Bara la Afrika na pia amevunja rekodi ya dunia kwa sababu timu yake ikiwa kama ni kocha wa Timu ya Taifa mara tatu mfululizo. Hiyo ni jumla ya miaka 15 ya *professional carrier* yake kocha huyu Al-Shihata.

Mhe. Spika, la pili mara nyingi tunapopeleka makocha kwa ajili ya mafunzo huwa tunalinganisha bajeti wizarani. Bajeti ya kumpeleka kocha mmoja kwa ajili ya kwenda kupata mafunzo nje na kumleta kocha mmoja au mkufunzi mtaalam kutoka nje ili wafaidike makocha wengi basi huwa tunaona kwamba ni vizuri kumleta kocha mmoja ambaye ataweza kufundisha makocha wengi zaidi hapa kwetu Zanzibar.

Kwa hiyo, mara nyingi huwa tunapendelea kuwaleta wale wakufunzi kuja kuwafundisha makocha wetu kuliko kuwapeleka nje. Kwa sababu bajeti ya kumleta mmoja wanafaidika wengi zaidi kuliko kumpeleka mmoja.

Lakini bado nasema tena kwamba ikipatikana nafasi kuna haja ya makocha wetu kwenda kuona *standard* ya nje, kuna *standard* za viwanja na kuona ule muono wa hali ya nje ilivyo ili waweze kuongeza taaluma yao.

Nam. 59

Fidia ya Mwani – Chwaka

Mhe. Ali Abdalla Ali – Aliuliza:-

Mwekezaji wa Hoteli ya *Chwaka Bay* aliwahi kuwa na mzozo na wakulima wa mwani wa kijiji cha Chwaka kuhusu mwani ambao umepandwa kwenye eneo la pwani la Hoteli hiyo. Mzozo huo uliosababisha eneo la kupanda mwani kuhamishiwa sehemu nyingine lakini wananchi hao bado hawajalipwa fidia ya TZS 160 milioni kwa kukubali kuhamisha eneo hilo.

(a) Je, Mhe. Waziri, ni nini kimekwamisha malipo ya fidia hiyo?

(b) Kwa kuwa matatizo kama haya bado yametanda katika maeneo mengine. Je, Wizara ina mikakati gani ya kuyaondoa?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 59 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatayo:-

(a) Mhe. Spika, kwa kawaida wizara inapopata taarifa ya migogoro hiyo hushirikiana na taasisi husika katika kuleta suluhu ya majambo hayo na kufanya pande zote zifanye kazi zao kwa mwenendo mzuri.

Mhe. Spika, kwa suala hili wizara yangu bado haina taarifa yoyote na imeshindwa kupata taarifa rasmi juu ya suala hilo. Hata hivyo,

Wizara yangu kupitia Kamisheni ya Utalii imewasiliana na taasisi husika ikiwemo Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini ambayo ndio yenye kushughulikia masuala ya ukulima wa mwani pamoja na hoteli yenyewe ya Chwaka Bay ili kufuatilia kadhia hiyo, ambao nao walishindwa kutoa taarifa za kuwepo kwa mgogoro huo.

Kwa ujumla Mhe. Spika, Wizara yangu haina ithibati ya kuwepo kwa mzozo huo. Hata hivyo, tunaendelea kufuatilia kadhia hiyo.

(c) Kama ilivyo utaratibu na kawaida ya Wizara yangu matatizo na mizozo kama hiyo ni mambo ya kawaida kutokea hasa katika maeneo ya uwekezaji na Utalii hali ambayo imeipa uzoefu Wizara yangu kutatua migogoro hiyo na kufikia usuluhisho ulio mzuri.
Mkakati unaotumika Mhe. Spika, ni ushirikishwaji wa wadau husika katika kubuni mbinu na kuendeleza mazungumzo ya pande zote zinazohusika. Hivyo, Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji itashirikiana na taasisi zinazohusika na migogoro kuweka mikakati madhubuti itakayosaidia kuondosha matatizo hayo na kuleta manufaa kwa pande zote. Ahsante.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza kwa Mhe. Waziri kama ifuatavyo. Mhe. Spika, nataka nimuulize Mhe. Waziri kwamba kwa mujibu wa majibu ambayo alikuwa anatoa hapo, suala la mizozo baina ya wanavijiji na wawekezaji ni jambo la kawaida kiasi kwamba wizara yake sasa imekuwa na uzoefu wa kutatua kama alivyoeleza.

Je, nilikuwa napenda kujua wakati wa mikataba baina yao na hawa wawekezaji wananchi wanashirikishwa kwa kiasi gani ili kupunguza hii mizozo, au wanaona basi twende hivyo hivyo mpaka tusubiri mizozo na kutatua?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, mikataba ya serikali na wawekezaji huwekwa baina ya mwekezaji na ZIPA pamoja na wizara inayoshughulikia mambo ya ardhi. Hata hivyo kabla ya kusainiwa kwa mikataba hiyo kamati ya utaalamu ya ZIPA ambayo inashirikisha wizara nyingi au zote takriban huwa inashughulika mpaka katika ngazi za chini kwenye eneo ambalo mwekezaji anataka kuekeza.

Kwa hivyo, kabla ya kuingia mikataba huwa wanafanya kazi na wananchi wa eneo lile kabla ya kusainiwa kwa mikataba hiyo. Hii imesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza mizozo sasa hivi ya wanavijiji na wawekezaji.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b). Mhe. Spika, mizozo kati ya wawekezaji wa mahoteli na wanakijiji bado ipo. Nakubaliana na Mhe. Waziri kuwa bado mizozo hiyo inaendelea na hasa wakulima wa mwani, suluhu baadae inakwisha. Serikali huwashawishi wananchi wakubali kulipwa fidia. Mhe. Spika, swali langu liko hapa, Baada ya wananchi kulipwa fidia hiyo, je, Mhe. Waziri haoni wananchi hawa tunawauwa kimapato, hawatokuwa na kazi ya kudumu ya kuendesha maisha yao maana wanachopewa kile kile akishapewa anakitumia haraka?

Pili, mwani ni sehemu ya mazao yetu ya biashara, ikiwa mwani hautolimwa kwa sababu ya hoteli, je haoni sasa hivi nchi yetu itapungukiwa na biashara ya zao la mwani na itapunguza mapato ya nchi?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, ni kweli kwamba inapotokea mizozo sisi serikali huwaomba wawekezaji kuwalipa fidia wananchi wanaolima eneo lile mbele ya hoteli au karibu na ufukwe wa hoteli.

(a) Baada ya kulipwa fidia wananchi wale husogea mbele zaidi, sio kwamba mwekezaji anakataza bahari yote isilimwe mwani hapana, huwa wanasogea mbele zaidi. Mifano hii imetokea maeneo mengi tu. Kwa mfano Kiwengwa, Chwaka na kwengineko. Kwa hivyo, bado wananchi wanaendelea na upandaji wa mwani.

(b) Kwa sababu wananchi wanaendelea na upandaji wa mwani, kwa hivyo suala la kupungua kwa uzalishaji wa mwani hautasababishwa na kuwepo kwa mizozo au kuondoka katika maeneo ya hoteli na kulima sehemu nyengine.

Mhe. Spika, taarifa iliyojitokeza hivi karibuni ni kwamba mwani ni sehemu ya kivutio cha utalii, kwa hivyo watalii wanapokuwa ufukweni huwa wanapenda sana kuona wananchi wanavyolima mwani, na wengine wanakwenda kujaribu kupanda mwani. Kwa hivyo, sio kwamba wanakatazwa kabisa kulima mwani, lakini wanasogea mbele, wanaondoshwa pale eneo ambalo wageni wanaogelea lakini huwa wanasogea mbele na kuendelea na kilimo hiki.

Nam. 16

Ujenzi wa Nyumba za Madaktari Zanzibar

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibiwa swali langu naomba nifanye marekebisho

kidogo. Kwa kuwa katika mkutano uliopita, swali la kifungu (a) na (b) Mhe. Naibu Waziri alinijibu na nikafurahi. Kwa hivyo, naomba nijibiwe swali hili la 16 kifungu (c) na (d).

Serikali nyumba za madaktari katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba ili kupunguza tatizo la ukosefu wa madaktari hasa vijijini.

(a) Mhe. Waziri, Kampuni ngapi ziliingia katika mchakato wa maombi ya ujenzi wa nyumba hizo?

(b) Ni Kampuni ipi imechaguliwa kujenga nyumba hizo na ni kwa gharama kiasi gain?

(c) Katika baadhi ya maeneo hasa ya kwenye visiwa vidogo vidogo kikiwemo kisiwa cha Shamiani – Mwambe, hapana vijana wazalendo wenye ujuzi na taaluma ya afya. Je, Serikali itachukua juhudi gani kuwapata vijana hao?

(d) Majengo yanayojengwa ni ya kisasa na katika baadhi ya maeneo ya kilimo hakuna huduma za umeme. Ni kwa muda gani serikali itachukua juhudi za maksudi ili majengo hayo yapate huduma hiyo muhimu ijapokuwa kwa nishati ya jua (solar energy)?

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, tunaomba ujibu kifungu cha (c) na (d), sijui kama mtiririko wa majibu yako utakwenda vizuri.

Mhe. Naibu WAziri wa Afya na Ustawi wa Jamii – Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake 16 kifungu cha (c) na (d) kama alivyoeleza mwenyewe kuwa kifungu (a) na (b) amekitoa.

(c) Mhe. Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inatoa kipaumbele maeneo kama Shamiani Mwambe, lakini tunahitaji kupata vijana wenye sifa ambao watakaojiunga na Chuo cha Afya Bweni. Kwa mfano maeneo ya Kijini, Tumbatu na kadhalika, tunao wanafunzi hawa katika Chuo cha Afya Bweni.

(d) Mhe. Spika, sehemu ambazo zimekosa umeme kutoka Kidatu, wizara yangu kupitia Mradi wa Kusaidia Kupunguza Vifo vitokanavyo na uzazi na ADB utazipatia nyumba zote umeme mbadala utokanao na jua, yaani *Solar Power*. Hatua za utekelezaji wa mpango huo zimeanza kuchukuliwa na zinaendelea vizuri kuelekea kwenye mafanikio.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa amekiri kwamba wanatoa vipaumbele kwenye visiwa kama Shamiani na Kijini. Ningependa kujua ni vijana wangapi anaohitaji kwa mwaka huu kwa visiwa vya Shamiani Mwambe na Makoongo ili tumpatie haraka wakajifunze?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kwa mwaka huu suala la kuingiza vijana katika kuchukua fani mbali mbali katika Chuo chetu cha Afya Mbweni utaratibu umeshamalizika. Lakini naomba tuwasiliane baadae naamini tutafanya tena *interview* mwaka huu na mwakani tutachukua tena vijana. Kwa hivyo, tuwasiliane na tuweze kupanga hao vijana atatuletea lini ili tutakapoanza awamu nyengine waweze kuingia.

Mhe. Asha Moh'd Hilal: Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kupata nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

(a) Kwa kawaida wanafunzi wakimaliza huwa wanapangiwa popote pale, sijui kama ni kwa mkataba au vipi kwa muda wa miaka miwili. Namuomba Mhe. Naibu Waziri kwa muda huu hatowatumia hao vijana kwa hivi vijiji vilivyokuwa havina hawa wahudumu?

(b) Wengine wanakuwa hawaendi. Je, ni hatua gani za makusudi atakazochukua kwa hao watakaokuwa wakorofi hawatohudhuria huko kwenye sehemu zao za kazi? Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli baadhi ya vijana hasa kati ya kwenda Pemba na Unguja huwa wanapewa miaka miwili miwili, wanakwenda miaka miwili halafu wanarudi wanakwenda wengine. Kwa hivyo, utaratibu upo.

(b) Mhe. Spika, hatua ziko nyingi tu ambazo zinaweza zikachukuliwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa sababu kama atakataa kabisa mtu kupelekwa sehemu anayokwenda, basi anaweza kunyang'anywa hata leseni yake ya uuguzi.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, matatizo ya wafanyakazi au madaktari katika vijiji kama Mwambe na Shamiani yako mengi sana, nashukuru serikali hasa kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii huchukua juhudi za kuwasomesha vijana kutoka sehemu hizo.

Lakini tatizo liliopo hasa kwa wafanyakazi wa kike baada ya muda tu wafanyakazi hao huwa wanaolewa na wanaondoka.

Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri mbali ya juhudi ambazo amemuahidi Mhe. Hija Hassan je, tatizo kama hili atalidhibiti vipi ili kuhakikisha wafanyakazi wale ambao wanateuliwa maalum kwa vijiji fulani basi wanaweza kubakia na kutoa huduma kwa lengo ambalo limekusudi?

Mhe. Spika: Pengine pamoja na kudhibiti kutoolewa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, hili suala si la Mwambe na Shamiani tu, yako maeneo mengi na hili tumeliona kwa sote. Lakini mwanzo wa tatizo hili ilikuwa inaonekana watu hasa wale wahusika au walengwa hawatoki katika maeneo yaliyolengwa kwenda kutoa huduma, walikuwa wakichukuliwa kijumla jamala wanakuja kuchukua mafunzo katika Chuo cha Afya Mbweni katika hali ya ujumla, lakini baadae ndio anapangiwa kule. Hilo lilikuwa likitokea.

Lakini Mhe. Spika, kwa sasa hivi tunaamini kuwa Waheshimiwa Wawakilishi pamoja na wananchi kwa jumla, watatutolea vijana ambao watakuwa waaminifu ili waje wapate mafunzo na halafu warudi kwenye vituo vyao. Naamini watahakikisha basi hata hizo ndoa ziweze kutokea katika maeneo yao hayo hayo, ili wasiweze kuhama katika vituo watakavyopangiwa. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 10

Tume ya Pamoja ya Fedha Tanzania

Mhe. Ali Abdalla Ali – Aliuliza:-

Tume ya Pamoja ya Fedha Tanzania imeanzishwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 134(1). Majukumu yake ni pamoja na kuchambua mapato na matumizi yanayohusu utekelezaji wa mambo ya Muungano na kutoa mapendekezo yake kwa serikali zote mbili na kuchunguza kwa wakati wote mfumo wa shughuli za fedha za Jamhuri ya Muungano na kutekeleza majukumu mengine ambayo Rais ataipatia Tume hiyo.

(a) Je, Mhe. Waziri Tume hii ina wajumbe wangapi na kwa uwiano gani kwa pande zote mbili?
(b) Mhe. Waziri unaweza kutueleza tangu Tume hii ianzishwe hadi leo imepata mafanikio gain?
(c) Muhula mmoja wa wajumbe wa Tume huchukua muda gain?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, anayeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 10 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, kwa mujibu wa ibara ya 134(1) inatamka kwamba "Kutakuwa na tume ya pamoja ya fedha yenye wajumbe wasiozidi 7, ambao watateuliwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kujibu ya ibara hii na masharti ya sheria". Kwa mujibu wa ibara hiyo, tume ina wajumbe 7 kwa sasa kati ya hao wajumbe 4 wanatoka Tanzania Bara na wajumbe 3 wanatoka Zanzibar.

(b) Mhe. Spika, tume ya pamoja ya fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yaani (JFC), iliyoanzishwa kwa mujibu wa ibara ya 134 ya katiba ya Jamhuri ya Tanzania mwaka 1977, hivi sasa imetimiza miaka 6 tangu kuanzishwa kwake.

Mhe. Spika, katika kutekeleza majukumu yake ya msingi, tume imefanya kazi kubwa ya mapitio au *study* na kutoa ushauri katika nyanja mbali mbali za uhusiano wa kifedha baina ya pande mbili za Jamhuri ya Muungano kama ifuatavyo.

Study zilizokamilika;

1. Kuchambua vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za mambo ya Muungano na kutoa ushauri wa fomula inayostahiki kutumika.
2. Kuchambua na kubainisha wizara na asasi za Muungano na gharama za kuendesha mambo ya Muungano katika kipindi cha mwaka 1993/94 hadi kipindi cha mwaka 2003/2004. Ripoti ya kazi hiyo imewasilishwa.
3. Kuchambua madeni na misaada kati ya SMT na SMZ katika kipindi cha mwaka 1993/94 hadi 2003/2004.
4. Kuchambua masuala ya kifedha yanayohusu mambo ya Muungano kwa kipindi cha mwaka 1993/94 hadi mwaka 2005/2006.
5. Kuandaa mpango mkakati wa tume kwa kipindi cha miaka 5 kuanzia mwaka 2008/2009 hadi 2012/2013.
6. Utafiti wa vianzo vya mapato vya Muungano kwa kipindi cha mwaka 2001/2002 hadi mwaka 2005/2006.
7. Kuandaa mfumo wa taarifa ya tume yaani Joint Finance Commission Information System. Mfumo huu una lengo la

kuwezesha tume kuwa na taarifa kamili.

8. Kuchambua uhusiano wa kifedha baina ya SMT na SMZ kwenye sera za bajeti na fedha.
9. Kuandaa tovuti ya tume.
10. Kuandaa sera na muongozo kuhusu uendeshaji wa akaunti ya fedha ya pamoja.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2003 hadi 2009 tume ilitoa ushauri katika maeneo yafuatayo:

i) Mapendekezo ya vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano ambayo yaliwasilishwa katika serikali zote mbili tarehe 29/8/2006.
ii) Mapendekezo ya utaratibu wa kushughulikia ushauri unaotolewa na tume kwa serikali mbili.
iii) Kuendeleza marekebisho ya sheria ya tume ya pamoja ya fedha sura ya 140.
iv) Kupendekeza marekebisho ya sheria ya ushuru wa bidhaa ili iweze kutumika Zanzibar.
v) Kushiriki katika kamati ya marekebisho ya kodi yaani *task force on task reform*.

(c) Mhe. Spika, kwa mujibu wa sheria ya tume ya pamoja ya fedha ya mwaka 1996, ibara ya 6(1) inatamka kwamba; naomba kunukuu kwa Kingereza.

> "*A member of the Commission shall hold office for a term of five years, and shall be eligible for re appointment*".

Kwa hivyo, muhula mmoja wa wajumbe wa tume kutumikia tume ya pamoja ya fedha ni miaka mitano na anaweza kuteuliwa tena.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nimuulize kama ifuatavyo. Mhe. Spika, Mhe. Waziri amekiri kwamba wajumbe wa tume hii ni 7, watumbe 3 wanatoka Zanzibar na wajumbe 4 wanatoka Bara. Lakini katika wajumbe hao 4 kutoka Bara wote ni wabunge.

(a) Je, kwa nini huku Zanzibar hakuna mjumbe hata mmoja wa Baraza au hatuna sifa za kuingia kwenye Tume hiyo?

(b) Pia katika taratibu za tume hii ni kufunguliwa akaunti ya pamoja, lakini hadi leo akaunti hiyo haijafunguliwa. Je, kuna sababu gani za msingi za kukwamisha suala hilo?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi:

(a) Mhe. Spika, kama nilivyosema uteuzi huu ni wa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa haidhuru mapendekezo yanafanywa, lakini uteuzi ni wa Rais. Kwa hivyo, mimi siwezi kumuhoji Rais kwa nini usiteuwe mwakilishi.

Lakini ushauri wake bila shaka tumesikia na tutawasilisha mapendekezo kwake.

(b) Kwa nini akaunti ya pamoja haijafunguliwa. Mhe. Spika, ni lazima niseme kwamba bado mchakato mzima wa hayo mahesabu hayajakamilika. Kwa hivyo, nakiri kwamba sababu moja wapo kwamba haijafunguliwa ni huo mchakato mzima wa hayo mapesa yenyewe hayajakamilika. Nafikiri ndio sababu kubwa. Inshaallah nalo haliko mbali litashughulikiwa ipasavyo.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais anayeshughulikia Fedha na Uchumi, naomba kuuliza swali moja la nyongeza dogo tu. Kwa kuwa mwaka juzi Mhe. Spika, nilikuwa mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, tulitembelea afisi ya tume na tukawauliza kwa nini hamjafanya shughuli zenu. Wao walichojibu ni kwamba wamepeleka mapendekezo yao serikalini, ili namna gani tume ifanye kazi. Lakini mpaka wakati ule serikali zote mbili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Zanzibar, hazijapelekea mapendekezo yake ili namna gani tume iwe.

Lakini leo cha kufurahisha Mhe. Waziri anajibu kwamba tayari serikali zote mbili zimepeleka ripoti tume na tayari zinafanyiwa kazi. Lakini Baraza la Wawakilishi ni chombo ambacho kinawapa fursa wananchi waseme mambo yao. Kuna kifungu kimoja cha katiba kinasema, kuna haki ya mwananchi kupata taarifa kupitia njia yoyote. Hivi kuwanyima taarifa hii Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa maelezo aliyoeleza mheshimiwa ya uchambuzi, huoni kwamba ni batili kwa sababu bado Kamati ya Fedha na Uchumi haina ripoti hiyo? Kwamba tayari zimepelekwa ripoti huko tume na sasa hivi inafanyiwa kazi. Kama inajua hivyo, je itarekebisha vipi ili na Kamati ya Fedha na Uchumi iwe na taarifa rasmi kama ulivyotoa wewe Mhe. Waziri?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, Mhe. Ame Mati Tume ndio iliyoleta ripoti katika serikali zetu mbili, sio kwamba serikali tumeshawajibu, bado. Sasa sisi katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

tumeipokea ile ripoti tumeshaifanyia kazi na tunaendelea kuifanyia kazi. Katika kuifanyia kazi, nakumbuka tulifanya semina na umesema ulikuwa mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi katika kipindi kilichopita, nakumbuka tulijikita *Fisherman Resorts* kule, tukajibanza kule kuchambua baadhi ya mapendekezo ili tupate maoni yenu.

Kwa hivyo, inaonesha wazi Mhe. Spika, kwamba sio kama Baraza tumeliwacha, hapana, sote ni wawakilishi wa wananchi, kwa hivyo tumewashirikisha kupata maoni. Kwa hivyo, bado ule mchakato mzima wa kuichambua serikalini kwetu haujakamilika. Hili sio suala jepesi Mhe. Spika, linataka mazingatio makubwa. Bora kidogo kidogo tuchelewe lakini tufike mahala tupate maamuzi ya mwisho.

Mhe. Spika, kama nilivyosema hili suala limetajwa kwenye katiba. Kwa hivyo, pengine tutakuja na ushauri wa kulibadilisha tusemeje. Kwa hivyo, mimi ningeshauri sana Mhe. Ame Mati kwamba bado tuipe fursa serikali yetu iweze kuishughulikia ipasavyo kwa manufaa ya nchi yetu.

Nam. 45

Kilimo cha Mpunga wa Kumwagilia Maji

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

(a) Je, Mhe. Waziri, tangu kuanza kufufua kilimo cha mpunga wa kumwagilia maji hapa Zanzibar mafanikio gani yamepatikana?

(b) Je, wananchi wanapewa taaluma gani juu ya kilimo hicho ili kiwasaidie kuleta tija na faida kubwa zaidi?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 45 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, mafanikio yaliyopatikana ni kama yafuatayo:-

- Eneo linalolimwa Mpunga wa Umwagiliaji Maji hivi sasa ni hekta 700 sawa na ekari 1750 zinazolimwa. Kabla ya kazi ya kufufua ni hekta 50 tu ndizo zilikuwa zikilimwa kilimo hicho (sawa na ekari 150).

- Kabla ya kufufua wakulima 500 tu ndio waliokuwa wakilima kwa umwagiliaji maji, ambapo sasa wakulima wapatao 17,000 wanajishughulisha na kilimo hichi Unguja na Pemba.

- Hivi sasa wakulima wanalima mara mbili zaidi na mavuno yanafikia tani tano kwa hekta moja kutoka nusu tani kwa hekta moja.

- Mbinu mpya za Umwagiliaji Maji zimeanza kutumika na kuwapatia wakulima tija zaidi.

(b) Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira inao mpango unaendelea kila mwaka kuelimisha wakulima wa mabonde yetu kwa mpango maalum ndani na nje ya nchi yetu. Pia chuo chetu cha Kizimbani kuanzia 2011 kitakuwa na kituo maalum cha mafunzo ya wakulima kwa nia ya kuwawezesha wakulima kupata tija katika kilimo chao na kupata faida kubwa.

Mhe. Spika, kila mwaka wakulima wasiopungua elfu tatu (3000), hupata mafunzo hayo ya kilimo bora cha Umwagiliaji Maji kupitia muongozo maalum uliotayarishwa kwa wakulima wa mpunga, mboga mboga na matunda.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira, naomba nimuulize kama ifuatavyo. Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba hivi sasa wako wananchi wengi wanafunzwa kilimo hiki cha kileo cha umwagiliaji maji ili wapate tija zaidi.

Je, baada ya mabonde ya serikali Mtwango na sehemu nyengine, wananchi hawa wanalima sehemu gani kilimo cha kumwagilia maji?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, tuna mabonde mengi sasa hivi ya kumwagilia, lakini moja katika lengo kubwa la serikali ni kuhakikisha kwamba hekta zote 8,721 zilizokuwepo Zanzibar lengo letu ni kuhakikisha kuwa tunalima kilimo cha kumwagilia.

Lakini kwa sababu kilimo cha kumwagilia kina gharama kubwa na tuna tegemea sana wafadhili wetu kutoka Korea na Japan kwa ajili ya kazi hiyo. Kwa hivyo, kwa sasa hivi tumeongeza, na katika maeneo ambayo tumeongeza kwa hapa Unguja ni maeneo hayo mawili ambayo umeyataja na kwa upande wa Pemba kuna Saninga na kuna kituo chengine ambacho ni Makombeni, kwa sababu sasa hivi tumo kwenye matayarisho ya kuhakikisha kwamba tuna lima katika kilimo hicho cha kumwagilia maji. Pia tunacho kituo chengine cha Kinowe ambacho pia kimo katika matayarisho kwa ajili ya kazi hiyo ya kilimo cha kumwagilia maji.

Vile vile tuna eneo kubwa ambalo sasa hivi limeleta tija kubwa zaidi, eneo la Cheju, pia nalo ni miongoni mwa maeneo ya hapa Unguja ambayo yamo katika kilimo cha kumwagilia maji. Kwa faida ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wao mwaka jana waliweka rikodi ya juu zaidi katika kilimo hicho. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, dunia hivi sasa hasa katika ukanda wetu wa Afrika ya Mashariki na Kati unakabiliwa sana na ukame. Lakini kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu atuepushie, baadhi ya maeneo yana mafuriko makubwa, ndio harakati za hali ya hewa duniani.

Mhe. Spika, pamoja na hayo niseme tu kwamba wenzetu Tanzania Bara wana mkakati wa kilimo kwanza. Kilimo kwanza hiki kinaeleweka kuwa ni mfumo maalum wa kuhakikisha kwamba kilimo kinaongezeka ili wananchi wapate tija ya mazao kwa wingi na kuondokana na hali mbaya ya ukosefu wa chakula.

Je, kwa kuwa mfumo huu ni mzuri na yale mabonde ambayo yalikuwa hayaingiliki katika umwagiliaji maji kwa wenzetu hivi sasa wameyafanya yamwagiliwe maji. Mimi nakubaliana na jibu ambalo amelijibu Mhe. Naibu Waziri kwamba tuna wafadhili wetu wahisani kama Wakorea na Wajapan kuwa wako tayari kutusaidia pindi tukiwahitaji. Je, tuna mpango gani hivi sasa wa makusudi, kwa kuwa kilimo kwanza ni mkombozi kwa yale mabonde makubwa. Kwa mfano Nguli, Kilombero na Cheju yanaendelea na kwengineko ambako yako mabonde makubwa kuliko haya yanayomwagiliwa sasa hivi. Serikali ina mtazamo gani wa kuyatizama mabonde yale ili kuhakikisha umwagiliaji unapatikana ili mazao yaongezeke.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kujibu swali la nyongeza la Mhe. Ali Suleiman Ali, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kutoa majibu ya ziada.

Mhe. Spika, kwa kweli kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba lengo la serikali pamoja na wizara yangu ni kushirikiana na serikali kuu kwa ajili ya kuomba misaada kwa wafadhili mbali mbali, ili hatimaye tuweze Zanzibar nzima, yaani Unguja na Pemba mabonde yetu yote yawe ya umwagiliaji.

Kwa sababu tumeona hiyo ndio njia moja pekee kuwa sana ya kuimarisha kilimo. Kwa hivyo, hatua hizo zimo kuchukuliwa na kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri sehemu mbali mbali hivi sasa zinaendelea na mpango huo wa umwagiliaji.

Kuhusu suala la kwamba wenzetu Tanzania Bara wameanzisha kwa lengo lile la kuimarisha kilimo wao wameanzisha Kilimo Kwanza. Kwa upande wetu hapa serikali imeunda kamati maalum, ambayo moja katika majukumu yake ni kuishauri serikali juu ya namna gani kuendeleza kilimo kiwe bora zaidi katika uzalishaji pamoja na ukulima bora.

Kwa hivyo, sera yetu ni Maendeleo ya Kilimo na kamati ipo ambayo inashughulikia masuala haya. Kwa kweli mpaka hivi sasa kilimo kwa ujumla kimeongezeka sana kama vile kilimo cha mpunga, miti ya matunda pamoja na mboga mboga.

Mhe. Spika, ahsante sana.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe 2010

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi.: Mhe. Spika, kwanza naomba uniruhusu nimshukuru Mwenyezi Mungu muumba kwa kutujaalia sote kufika hapa tukiwa wazima wa afya na siha.

Pili kwa idhini yako naomba uniruhusu kuwasilisha mbele ya Baraza hili tukufu Hotuba ya Marekebisho ya Sheria Namba 3 ya 1994 ya kuanzishwa Mamlaka ya Mji Mkongwe na Mengine Yanayohusiana Hayo, ili upitiwe na Baraza hili kwa ajili ya kuwa na sheria mbadala itayokidhi zaidi haja ya kuuenzi na kuutunza Mji Mkongwe kama Urithi wa Taifa wa Ulimwengu. Vile vile kama eneo la makaazi liliobeba ndani yake Makao Makuu ya Serikali, kitovu cha biashara, utamaduni na elimu kwa nchi yetu.

Mhe. Spika, tangu Sheria ya kuanzishwa Mamlaka ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe ilipopitishwa mwaka 1994, kumetokea mabadiliko mengi muhimu na makubwa katika mustakbali wake na wa taifa letu. Mji wenyewe umepata heshima ya kuwa ni Urithi wa Kimataifa, ukaendelea kukua kwa kasi kuwa Kituo Kikuu cha Utamaduni kwa ukanda huu wa Afrika.

Tamasha la Kimataifa la Filamu, Tamasha la Utamaduni wa Mzanzibari, Chuo cha Muziki kwa Nchi za Utamaduni wa Jahazi na Tamasha la Sauti za Busara ni miongoni mwa viashirio muhimu vya nafasi inayokuwa ya mji wetu kama kituo cha Utamaduni *(Makofi)*.

Mwaka jana tulishuhudia sherehe kubwa za ufunguzi wa Bustani yetu ya Forodhani. Bustani hio mbali ya kuwa rasilmali ya kiuchumi na kiutamaduni kwa kuwa kivutio kikubwa kwa watalii, lakini imetujengea heshima kubwa mbele ya jamii ya kimataifa. Leo wananchi wengi hukimbilia sehemu hiyo, kwa kujipumzikia na kupata huduma muafaka mbali na ajira inayozalishwa kwa kupatikana kwa huduma hizo.

Kwa ufupi, umaarufu wa Zanzibar unazidi kukuzwa na hadhi hii ya Urithi wa Kimataifa na kuongezwa thamani kwa miundo mbinu iliyomo ndani ya mji huu, mambo ambayo ni ufunguo muhimu katika milango ya ustawi wa kiuchumi na kijamii nchini. Ni wazi kuwa ili sifa ipate kuendelea, iko haja ya kuyafanya maendeleo haya kuwa endelevu kwa kuyakimu mahitaji ambayo yatatumika katika kuiweka hali hiyo, kuwa katika taswira iliyo au kuimarisha zaidi.

Mhe. Spika, mbali ya mafanikio hayo, bado kuna changamoto kadhaa zinazoukabili Mji Mkongwe. Bado yako majengo na maeneo kadhaa ambayo yako katika hali mbaya. Kuna mwingiliano mkubwa wa kitaasisi unaochagiza uwajibikaji katika uendelezaji na uhifadhi wa Mji Mkongwe.

Shindikizo la uendelezaji ndani ya Mji Mkongwe ni kubwa kuliko uwezo wa Mji wenyewe, hali ambayo italiweka kila jengo na kila eneo katika hatari ya kuendelezwa kinyume na matakwa ya uhifadhi. Haya ni mazingira ambayo yatakwenda kinyume na ile dhana ya uendelevu ambayo tuliiweka, ili kulinda heshima ya mafanikio yaliopatikana na tunayoyafikiria katika mipango yetu ya baadaye.

Mhe. Spika, ni uzoefu wa kimataifa kwa sasa kuwa maendeleo kama haya ya miji ya aina hii, huletwa kwa mashirikiano ya pamoja baina ya Sekta ya Umma (*Public Sector*) na ile ya Binafsi (*Private Sector*). Kwa bahati mbaya, kwa hali tunayokwenda nayo, mchango wa sekta binafsi katika uhifadhi na uimarishaji wa Mji Mkongwe wenyewe bado ni mdogo ukilinganishwa na uwezo wa sekta yenyewe (*Public Sector*).

Mhe. Spika, mapendekezo ya mabadiliko ya sheria yanayowasilishwa mbele ya Baraza hili tukufu, yana nia ya kukabiliana na changamoto hizi na nyinginezo, sambamba na kukabiliana na mambo mengine yaliyojitokeza baada ya kutungwa sheria inayokusudiwa kubadilishwa. Mojawapo ni kuingizwa Mji Mkongwe kwenye Urithi wa Kimataifa, kwa maana ile orodha, ambapo usimamizi wake utalazimika kuendana na matakwa ya Jumuia ya Kimataifa kwa Mujibu wa Mkataba wa Urithi wa Dunia (*World Heritage Convention*) ambao Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeuridhia.

Jengine ni mabadiliko ya majukumu ya serikali kufuatana na mageuzi yanayoendelea ulimwenguni ambapo kwa sasa serikali inapaswa kuwa mhamasishaji (*facilitator*) zaidi kuliko mpaji (*provider*). Ndani ya Mji Mkongwe hili linamaanisha mabadiliko yatayolazimu katika utunzaji wa milki za serikali ama kuendeshwa kibiashara zaidi au kuhamia katika miliki binafsi. Suala la ushirikiano wa Sekta Binafsi na ya Umma (*Public Private Partnership*) nalo lina mchango wake katika marekebisho yanayowasilishwa.

Mhe. Spika, Muundo wa Sheria inayowasilishwa mbele ya Baraza tukufu la Wananchi wa Zanzibar.

Muundo wa Sheria hii unajumuisha jumla ya sehemu saba kama zifuatazo:-

Sehemu ya Kwanza:

Sehemu hii inazungumzia mambo ya utangulizi, ambayo ni jina fupi la sheria na tarehe ya kuanza kutumika pamoja na ufafanuzi wa baadhi ya maneno muhimu yaliyotumika ya mswada huu katika kifungu cha 1 hadi cha 2.

Sehemu ya Pili:

Sehemu hii inazungumzia kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mji Mkongwe, kazi zake pamoja na hadhi yake kisheria, ambapo imeelezea uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu, majukumu yake, uwezo, muundo wa mamlaka pamoja na kuzungumzia uteuzi wa Wakurugenzi, Washauri Waelekezi na wafanyakazi wa mamlaka katika kifungu cha 3 hadi cha 10.

Sehemu ya Tatu:

Sehemu hii inazungumzia kuanzishwa kwa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Mji Mkongwe pamoja na mambo ya jumla ya kazi na uwezo wa Bodi ya Wakurugenzi katika kifungu cha 11 hadi cha 24.

Sehemu ya Nne:

Sehemu hii inazungumzia uwezo wa jumla ikiwemo uwezo wa Mamlaka kuingia katika majengo na kutoa taarifa rasmi, au uwezo wa kufanya mapitio ya ada,uwezo wa kupata taarifa, uwezo wa kufanya uchunguzi pamoja na uwezo wa kushauriana na washirika pamoja na serikali katika kifungu cha 25 hadi 31.

Sehemu ya Tano:

Sehemu hii inazungumzia uwezo wa utekelezaji amri ambazo zitakuwa zinatolewa na mamlaka, adhabu, kufutwa kwa mkataba na madhara yake pamoja na uwezo wa waziri kutunga kanuni na uwezo wa kulitangaza jengo lolote au eneo la serikali katika Mji Mkongwe kutumika kwa matumizi mahsusi kwa maslahi ya umma katika kifungu cha 32 mpaka 40.

Sehemu ya Sita:

Sehemu hii inazungumzia masharti ya jumla ya Fedha za Mamlaka pamoja na mambo yanayohusiana nayo katika kifungu cha 41 hadi 45.

Sehemu ya Saba:

Sehemu hii inazungumzia masharti ya jumla ikiwemo kubakiza (*saving*) na kufuta (*repealing*) pamoja na masharti ya kurukia (*overriding*) katika kifungu 46 hadi 47.

Asili ya Sheria Iliopo:

Mhe. Spika, sheria iliopo ya kuanzishwa Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe, imefuatia mapendekezo ya Shirika la Makaazi la Umoja wa Mataifa (*UN-Habitat*), ambalo mwaka 1982 liliombwa kutafiti hali iliyokuwa imekithiri ya kuporomoka kwa majengo ndani ya Mji Mkongwe kulikosababisha upotevu mkubwa wa maisha na mali.

Kupitia Ripoti yake iitwayo "*The Stone Town Strategy For Integrated Development* ya mwaka 1992", *Habitat* ilionya kwamba muundo wa kitaasisi uliokuwapo wakati ule haungeweza kuwa na suluhisho endelevu la tatizo hilo. *Habitat* ikashauri kuundwa kwa taasisi maalum itayojihusisha na Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe peke yake. Uhifadhi kama ni njia ya kutatua uporomokaji wenyewe, na uendelezaji kuwa ndio mkakati endelevu wa kupambana na uharibifu wa majengo.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikakubali kimsingi mapendekezo hayo, kwa kuanzia ikabadilisha kitengo chake cha Nyumba Kongwe ndani ya Idara ya Ujenzi kuwa ni Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe, mwaka 1985. Hata bila ya kuwa na sheria, mamlaka ikatekeleza majukumu yaliyopaswa kutekelezwa na taasisi iliyoundwa kisheria, ikiwamo uuzaji wa Nyumba za Serikali, matengenezo ya majengo ya umma yaliyokuwa na hali mbaya kwa kushirikiana wa Sekta Binafsi na Mashirika ya Kimataifa pamoja na kudhibiti ujenzi ndani ya eneo la Mji Mkongwe.

Kwa hivyo Sheria ya Mji Mkongwe ndio ya mwisho kutungwa katika mfululizo wa sheria zinazohusu maswala ya udhibiti ujenzi, zinazohusu utawala wa ardhi, zinazohusu eneo la Manispaa na zinazohusu uhifadhi wa majengo ya kale. Isingeweza kuwapo bila ya kutwaa baadhi ya kazi na majukumu ya taasisi zilizoitangulia katika utekelezaji wa maswala hayo.

Kwa hivyo, kwa mnasaba wa mapendekezo ya *UN-Habitat* yaliyoridhiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, utwaaji huu wa majukumu ya taasisi nyingine haukuwa wa bahati mbaya, kwa kiasi fulani ndio madhumuni mamojawapo ya sheria yenyewe na kuanzishwa kwa Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe.

Mhe. Spika, hali hii ya miji ya kihistoria kuwa chini ya usimamizi wa sheria na taasisi tofauti na mabaraza ya miji husika ni swala linalopatikana kwingi ndani ya nchi zinazoendelea. *UN-Habitat* haikuibua mfano huu, bali iliuchota kutoka kwengineko kwa kuangalia mifano ya miji yenye mazingira kama ya Mji Mkongwe wa Zanzibar.

Hadi miaka michache iliopita, Mji wa Kihistoria wa Havana ulikuwa unasimamiwa na jopo la taasisi mbali mbali chini ya Uratibu wa Chuo Kikuu cha Havana. Mji wa Kihistoria wa Tunis (Medina of Tunis) unasimamiwa na taasisi isiyo ya Kiserikali, "*Society for the Safeguarding of the Medina of Tunis*".

Baada ya Mji Mkongwe wa Zanzibar kuingizwa kwenye Orodha Urithi wa Kimataifa, Mji wa Kihistoria wa Lamu ukafanikiwa pia kwa mfumo kama huo wa kuwa chini ya Idara ya Makumbusho ya Kenya. Kisiwa cha Msumbiji ambacho kilitangulia kuingizwa kwenye Orodha kuliko Mji Mkongwe, nacho kimebadilisha mfumo wa utawala wake, ili kukabiliana na matatizo ya uharibifu wa majengo. Sasa nao uko chini ya "*Cabinet for the Conservation of the Mozambique Island*".

Hali hii haipatikani kwenye miji ya kihistoria ya nchi zilizoendelea kwa sababu kumekuwa na usimamizi endelevu wa miji hiyo kupitia mabaraza ya miji yao, jambo ambalo halikupelekea kuharibika kwa miji yao asilia kiasi cha kulazimika kuanza kuifufua. Kwa upande mwingine, miji mingi ya kihistoria au sehemu za kihistoria zinazosimamiwa na Mabaraza au Halmashauri za miji pekee kwenye nchi zinazoendelea imetoweka kutokana na Mabaraza ya Miji kushindwa kusimamia uhifadhi wake. Kwa mfano, Bagamoyo, Mombasa, Pangani na sehemu za Dar-es-salaam.

Mhe. Spika, kulipita miaka tisa baina ya kuanzishwa Mamlaka ya Mji Mkongwe na kutungiwa sheria. Ndani ya kipindi hicho, uhifadhi wa Mji

Mkongwe uliendelea vizuri bila ya dhana ya kuwapo kwa mgongano wa kitaasisi.

Ingawa haikukusudiwa, miaka tisa hiyo ya utekelezaji bila ya kuwa na sheria, iliyotokana na hofu za baadhi ya washirika dhidi ya mgongano wa kitaasisi na kimaslahi, ilisaidia sana kupima uhalisia wa hofu hiyo. Kilichosaidia wakati ule ni uwezo wa Mamlaka kifedha kutekeleza majukumu yake kulikotokana na kusimamia mauzo ya fedha za uuzaji Nyumba za Serikali, na ushirikiano baina ya taasisi.

Marakebisho ya sheria yanayowasilishwa yanalengwa kurejesha hali hiyo kwa kuwa na Bodi ya Wakurugenzi shirikishi, kuwa na Kikao cha washirika wote wa Mji Mkongwe angalau mara moja kwa mwaka, na kuwa na vyanzo endelevu vya mapato ya kuiwezesha Mamlaka kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Haja ya Mabadiliko:
Mhe. Spika, miaka kumi na tano ya utekelezaji wa sheria iliopo sasa ya Mji Mkongwe imebainisha changamoto kadhaa, ambazo zinahitaji mabadiliko ya sheria kukabiliwa. Mojawapo ni kutokuwapo uwezo wa kuwalazimisha wamiliki binafsi kutengeneza majengo yao, yanapokuwa katika hali ya kuhatarisha usalama wa watumiaji wa Mji Mkongwe.

Marekebisho ya Sheria hii kifungu 33 yanaipa uwezo Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe kutwaa jengo liliyo katika hali mbaya kwa ajili ya kusimamia matengenezo yake na hatimaye kuirejesha kwa mmiliki baada ya kurejesha gharama za matengenezo.

Changamoto nyingine ni ya kulinda hadhi ya Mji Mkongwe kama Urithi wa Kimataifa. Hadhi hii imekuja sheria iliopo kutungwa, na kwa hivyo haikuwa imezingatia dhima na majukumu hayo mapya, licha ya kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikuwa imesharidhia Mkataba wa Urithi wa Kimataifa.

Aidha, wakati Mji Mkongwe unaingizwa kwenye Orodha wa Urithi wa Kimataifa, *UNESCO* kupitia Kamati yake ya Urithi wa Kimataifa ilionya kuwa majukumu ya kiusimamizi na kiuratibu ya Mamlaka ya Mji Mkongwe yalipaswa kuwekwa vyema zaidi ndani ya sheria, sambamba na kuiimarisha Mamlaka yenyewe. Kamati ilitaka hayo yafanyike kufikia 2001, lakini kutokana na sababu mbali mbali haikuwezekana. Kufuatia matokeo kadhaa yaliyolazimisha Kitengo cha Urithi wa Kimataifa cha *UNESCO* kufanya ukaguzi wake ndani ya Mji Mkongwe, shindikizo la marekebisho haya linazidi kukua na ulazima wake ni dhahiri.

Maoni ya Washirika wa Maandalizi ya Sheria hii:

Mhe. Spika, mapendekezo haya yalipata bahati ya kuchangiwa na washirika kadhaa wakiwamo wakaazi, masheha, taasisi za kijamii na zisizo za kiserikali, wakuu wa taasisi za serikali, wasomi na wataalamu wa fani mbali mbali hapa Zanzibar. Muundo wake wa sasa kwa kiasi kikubwa unawiana na maoni ya wengi wao, ambao kimsingi walikubaliana na mapendekezo ya marekebisho yanayokusudiwa.

Kodi ya Majengo ni mojawapo ya chanzo cha mapato ya Mamlaka ya Mji Mkongwe. Hata hivyo, kwa utaratibu tunaoupendekeza kwenu Waziri anayehusika na Mji Mkongwe atashauriana na Waziri wa Wizara ya Fedha na Uchumi kuangalia mgawanyo wa kodi hiyo kwa Utengenezaji, Uendelezaji na Uhifadhi wa Mji Mkongwe hayo yamo kwenye kifungu 42.

Marekebisho ya sheria kuhusiana na hilo yamesababishwa na ukweli kwamba mtekelezaji mkuu wa utunzaji wa majengo na milki za Mji Mkongwe ni Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe, ambayo kwa utaratibu wa sasa haina chanzo chochote cha mapato ndani ya eneo lake la majukumu. Vibali vya ujenzi havipaswi kuwa chanzo cha mapato kama lengo ni kushajihisha matengenezo ya majengo yenyewe.

Aidha, kwa vile kodi ya majengo hutozwa kulingana na thamani ya majengo yenyewe, na kwa kuwa majengo yaliyotengenezwa yanaweza kuongezeka thamani hata mara kumi zaidi ya awali, watu wanaweza kutotengeneza majengo yao, kwa kuhofia kulazimika kulipa kodi kubwa zaidi juu ya gharama walizokwishatumia kwenye matengenezo.

Ushirikiano wa mamlaka za uhifadhi na uwezo wao wa kushauri namna bora ya kupunguza gharama za matengenezo unaifanya Mamlaka ya Mji Mkongwe kuwa mshirika mkubwa wa Kodi hii. Kunufaika na kodi hiyo, kwa hivyo, ni jambo la msingi *(Makofi).*

Mhe. Spika, licha ya mafanikio yaliyokwishapatikana tangu kuanzishwa Mamlaka ya Mji Mkongwe mwaka 1985 na Sheria ya Mamlaka mwaka 1994, bado kuna changamoto nyingi zinazokabili Uhifadhi Endelevu wa Mji Mkongwe. Bado Mji Mkongwe unabaki na urithi mkubwa wa utamaduni, lakini wakaazi na watumizi wake wanakabiliwa na umasikini mkubwa wa kipato.

Bado Mji Mkongwe unaendesha biashara ya kutosha kuweza kukimu matengenezo yake, lakini uhifadhi wake unaendelea kutegemea sana washiriki wa maendeleo na wahisani wengine. Hadhi ya Urithi wa Kimataifa imeusaidia

sana Mji Mkongwe katika kuvuta hisia za watu wa mataifa yote, lakini bado kuna nafasi kubwa zaidi ya kutumia fursa hii kwa ufanisi zaidi kiuchumi. Haya yote yanategemea kuwa na mji halisi (*authentic*), uliohifadhika kwa ujumla wake na unaowahakikishia wageni na wenyeji usalama na furaha.

Matengenezo yaliyomalizika ya Bustani ya Forodhani, yanayokuja ya ukingo wake wa Pwani na ya taa za njiani, yatasaidia sana katika kuelekea huko. Lakini bila ya kuwa na sheria itayohakikisha uwezo wetu wenyewe katika kukabiliana na matatizo yaliyo ndani ya uwezo wetu, bila ya kuwa na mikakati madhubuti itayoshirikisha wanajamii wote, na bila ya kuwa na mwamko wa kutosha wa nafasi ya Mji Mkongwe kwa uhai wa nchi yetu. Kutokana na hali hiyo, hatutakuwa na uhakika wa kuwepo kwa Mji Mkongwe kama makaazi yetu asilia wala kama Urithi wa Kimataifa. Marekebisho haya ya sheria yanalenga kuepukana na hali hiyo.

Mhe. Spika, ni matumaini yangu kwamba hotuba hii imesaidia kufafanua hali halisi ya haja ya kuwa na Sheria mpya ya Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe, na kwamba maelezo yangu yatawawezesha wajumbe kutafakari na hatimaye kujadili mapendekezo yanayowasilishwa kwa upeo stahiki.

Vile vile ni imani yangu kuwa baada ya Kikao hichi cha Baraza hili Tukufu, sheria hii itakuwa na meno ya kukabili changamoto zilizopo, ili kuzaa yale ambayo tunayoyatarajia kutekelezwa na Mamlaka ya Uendelezaji na Hifadhi ya Mji Mkongwe kwa maslahi ya Wazanzibari.

Mwisho napenda kuchukuwa nafasi hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa wale wote waliotoa michango yao kwa njia moja au nyengine, shukurani maalum ziende kwa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu, kwa msaada wao mkubwa walionipa katika kipindi cha matayarisho ya Sheria hii kupitia vikao vya kamati hiyo na kuiwezesha sheria hii, sasa kuwa na sura yake ya leo hii kwa kupata baraka za Wajumbe wa Baraza hili Tukufu.

Mhe. Spika, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni sana kwa kunisikiliza.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba uniruhusu nitoe maoni ya

Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi juu ya Mswada wa Kufuta Sheria ya Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe wa Zanzibar Namba 3 ya 1994 na Kuanzisha Sheria Mpya ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe pamoja na Mambo mengine yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na afya njema na kunipa nguvu za kusimama mbele ya Baraza lako hili tukufu, kuwasilisha maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Mswada huu wa Kufuta Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Mji Mkongwe wa Zanzibar Namba 3 ya 1994 na kuanzisha Sheria mpya ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe.

Vile vile namshukuru Mwenyezi Mungu kunipa afya njema na kuwajaalia nyinyi wajumbe wenzangu kuendelea na afya njema na uzima.

Mhe. Spika, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi imeundwa chini ya Kanuni ya 108 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi na kwa hivi sasa Wajumbe wake ni 10 wafuatao:-

1.	Mhe. Ramadhani Nyonje Pandu	Mwenyekiti
2.	Mhe. Hamad Masoud Hamad	Makamo/ Mwenyekiti
3.	Mhe. Kamal Basha Pandu	Mjumbe
4.	Mhe. Ame Ussi Juma	Mjumbe
5.	Mhe. Zakiya Omar Juma	Mjumbe
6.	Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Mjumbe
7.	Mhe. Subeti Khamis Faki	Mjumbe
8.	Mhe. Ali Denge Makame	Mjumbe
9.	Mhe. Omar Ali Jadi	Mjumbe
10.	Mhe. Asha Moh'd Hilal	Mjumbe
11.	Ndugu Othman Ali Othman	Katibu
12.	Ndugu Rabia Juma Shaaban	Katibu

Mhe. Spika, suala la Kufuta Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe wa Zanzibar Namba 3 ya 1994 na kuanzisha Sheria mpya ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe ni la umuhimu, kutokana na sheria iliyokuwepo kuwa na mapungufu makubwa ukilinganisha na mahitaji ya Mji Mkongwe hasa baada ya kuingizwa katika Orodha ya Miji ya Urithi wa Ulimwengu.

Mhe. Spika, kuanzishwa kwa sheria hii kutaipa uwezo Mamlaka hii, ambayo itakuwa na jukumu, wajibu na uwezo wa kusimamia sheria ambayo itakuwa na

uwezo mkubwa wa kumchukulia hatua mwenye nyumba, ambaye anaishi au ameitelekeza nyumba hiyo bila kuishughulikia na kumpelekea taarifa rasmi na baadaye kama hajachukuwa hatua zinazofaa, Mamlaka itachukuwa hatua za kumshtaki.

Mamlaka ya Mji Mkongwe ilifanya tathmini ya hali halisi ya Uhifadhi katika Mji Mkongwe kama ilivyotakiwa kufanya hivyo, kila baada ya miaka sita baada kupata hadhi ya Urithi wa Ulimwengu. Mapungufu yameainishwa na Zanzibar imetakiwa kuchukuwa hatua za makusudi za uhifadhi ili Mji huu usije ukaingizwa katika orodha ya miji iliyo hatarini ya kupoteza Urithi wake wa asili (*World Heritage in Danger*).

Mhe. Spika, kamati imeunga mkono jitihada zilizochukuliwa na Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe kwa hatua ilizozichukua, kuwaondosha wafanyabiashara wadogo wadogo wasio na ruhusa katika maeneo ya wazi na katika vichochoro vya Mji Mkongwe, kung'oa mabango ya matangazo yanayoathiri haiba ya Mji, kuondosha gereji zisizokubalika kwa lengo lile lile la kuhakikisha mandhari ya Mji Mkongwe yanatunzwa.

Kufanyiwa marekebisho ya sheria ya mwaka 1994 ambayo ina mapungufu, itasaidia kutekeleza kazi za uhifadhi katika majengo ya serikali na ya watu binafsi, kuendelea kutoa vibali vya ujenzi na matengenezo katika eneo la Mji Mkongwe bila ya kubadilisha aina ya jengo wala mpangilio wa nyumba na kuweza kutekeleza kazi zake kwa mafanikio.

Mhe. Spika, sheria inayotaka kuanzishwa mapitio yake yalianza rasmi Disemba 2007. Wananchi mbali mbali walishirikishwa pamoja na wale wanaoishi Mji Mkongwe, ili kuhakikisha michango na maoni yao yanapatikana, katika masuala yanayowagusa yanapewa kipaumbele, kamati inazipongeza jitihada hizi zilizofanywa na Mamlaka kwa kushirikiana na wafadhili,Taasisi za Serikali na za Binafsi.

Katika kuupitia mswada kamati imefanya marekebisho ya lugha iliyotumika katika mswada huo na maneno mengi yamebadilishwa, ambayo yalitoholewa kwa kiingereza kwa mfano "notisi" kamati imelitafsiri neno hili na kutoa maana ya "Taarifa rasmi" ambacho ndicho Kiswahili fasaha.

Mhe. Spika, kamati inatoa pongezi kwa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi hasa kwa viongozi hususan Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake, kwa kushirikiana na kamati katika kufanikisha kazi ya kuupitia mswada huu.

Matayarisho ya sheria hii imesaidia sana Mamlaka kujenga mahusiano ya karibu zaidi na wakaazi na watumiaji wa mji huu, pia kuweza kuutambua

muonekano wake kwa jamii. Jambo hili litawasaidia kupanga upya, ili kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kama inavyostahiki na lengo la kuwepo Mamlaka linafikiwa.

Katika kuupitia Mswada huu baadhi ya marekebisho yaliyofanywa na kamati ni pamoja na kifungu cha 2 tafsiri ya neno Mwenyekiti itasomeka kama ifuatavyo:-

> " Mwenyekiti maana yake ni mtu aliyeteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi chini ya kifungu cha 11 cha sheria hii"

Mhe. Spika, kifungu cha 2 ukurasa 43 tafsiri ya maneno "Mji Mkongwe wa Zanzibar" yatasomeka kama ifuatavyo:-

> "Mji Mkongwe wa Zanzibar, maana yake ni eneo linaloanzia baharini na linajumuisha fukwe zote za magharibi ya barabara ya "*Creek road*" na viwanja vya Mnazi Mmoja, Bustani ya Jamhuri, kwa ukanda wa mita 50 wa pande zote mbili kati ya njia inayotoka mtaa wa Darajani, kupitia Mchangani kumalizika Mlandege na kwa njia inayomalizikia Mtendeni, viwanja vya Malindi na eneo la Funguni, kama inavyoonyesha ramani ya Jaduweli la pili.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 9 (2) kimeongezwa kifungu kipya na kitasomeka. Mtu hatofaa kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu mpaka awe (a) Mzanzibari

Kifungu cha 9 (5) kimeongezwa maneno na kitasomeka kama ifuatavyo:-

"Mkurugenzi Mkuu atakuwa ndiye msemaji mku wa Mamlaka"

Mhe. Spika, kifungu cha 28 (5) kitasomeka kama ifuatavyo:-
"Endapo Mamlaka itakuwa na sababu za kuamini kuwa kuna mtu anamiliki au anatunza nyaraka zozote ambazo zinaweza kuisaidia katika utekelezaji wa kazi zake, Mwenyekiti, Mkurugenzi Mkuu au mfanyakazi yeyote wa Mamlaka, anaweza kupeleka ombi Mahakamani la kupatiwa hati inayowaruhusu Mamlaka kuingia kwenye nyumba au kukagua nyumba hiyo kwa kushirikiana na taasisi husika kutafuta nyaraka anazomiliki mtu huyo au anazozitunza na Mamlaka itatoa nakala au kuchukua nyaraka hizo.

Mhe. Spika, marekebisho mengine yamefanywa katika kifungu cha 34 (2) na kitasomeka kama ifuatavyo:-

34(2) “Haki na wajibu unaohusiana na mkataba au hali ya matumizi ya ardhi ambayo ipo hadi tarehe ya ufutaji itaendelezwa dhidi ya Mamlaka kwa kuzingatia kwamba endapo kutajitokeza shauri ambalo Mamlaka ni mdawa wa shauri hilo, Mamlaka inaweza kumuunganisha mmiliki wa awali kama mdawa mwenza na mamlaka itakuwa na haki ya kumwita au kuchukua hatua yoyote ambayo itakuwa muafaka kumlazimisha mkaazi wa mwanzo kulipa gharama au hasara ambayo itakuwa imetolewa dhidi ya Mamlaka”.

Mhe. Spika, kifungu cha 41 (1) kisomeke kifungu cha 40(1) na kitasomeka kama ifuatavyo:-

40 (`1) “mtu yeyote anaetenda kinyume au anaeshindwa kutekeleza masharti ya sheria hii, atakuwa ametenda kosa dhidi ya sheria hii na atawajibika atakapotiwa hatiani kulipa faini isiyozidi shilingi laki tano au kifungo cha muda usiozidi miezi mitatu au vyote”.

Mhe. Spika, kamati inaunga mkono utaratibu wa uundwaji wa Bodi ambayo ndio muhimili wa taasisi yoyote inayojitegemea ili kuweza kufanya kazi zake vizuri zaidi na kuendeleza mbele Mamlaka kwa lengo la kuelekeza na kushauri vizuri kwa nia ya kupatikana ufanisi zaidi, baada ya kupitishwa sheria hii na kuundwa kwa bodi hiyo.

Mhe. Spika, hayo ni baadhi ya marekebisho ambayo kamati yangu imeyaona na kuyafanyia kazi kama nilivyokwisha kufafanua namna ya uchambuzi wa vifungu na ufafanuzi kwa namna ilivyokusudiwa kwa kila kifungu cha sheria hii, kupitishwa kuwa sheria hii, kutapatikana ufanisi na kuondoa migogoro iliyokuwepo kabla ya sheria hii.

Mhe. Spika, ikiwa sheria hii itapitishwa itakuwa na uwezo wa kuuendeleza zaidi Mji Mkongwe, wananchi kuhamasishwa zaidi katika utaratibu wa kuunda kamati ndogo ndogo za kuendeleza mji huu kwa lengo la kuitangaza nchi yetu katika medani ya Kimataifa,

Mhe. Spika, kamati inazipongeza jitihada zinazochukuliwa na Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe katika kuitunza bustani ya Forodhani kwa lengo lile lile la kuhifadhi Mji Mkongwe ili ubaki katika urithi wa kimataifa. Utaratibu uliopo hivi sasa unaridhisha kwamba kazi ya kuimarisha maendeleo yaliyokwishafikiwa yanaendelezwa.

Mhe. Spika, kamati imeelezwa mipaka ambayo inaihusisha Mji Mkongwe inapita ili kuweza kutofautisha eneo la Mji Mkongwe na lile ambalo halihusiki kwa kuangalia ramani ambayo inaonyesha hali halisi ya eneo hilo na hasa zile sehemu zinazotakiwa kuhifadhiwa na kubakia katika hali yake ya asili.

Mhe. Spika, kamati inaziunga mkono jitihada zilizochukuliwa na Mamlaka kuanzisha mpango mpya wa utumiaji wa barabara ya Mji Mkongwe (*Traffic Plan*) kutokana na wingi wa magari na utumiaji mbaya wa njia za Mji Mkongwe. Hii itasaidia kuuweka mji katika hali ya amani kwa majengo ambayo hayastahamili kishindo kikubwa, na kuwanasuru watembeaji wa miguu na watoto wanaoishi humo na vile vile kuimarisha utaliii ambapo suala hili ni zuri na ni muhimu kwa uchumi wa nchi, na kuyaimarisha maeneo ya wazi.

Mhe. Spika, kamati imeelezwa kwamba Mamlaka inaridhishwa na ushirikiano inaoupata kutoka Serikalini, katika kutekeleza majukumu yake na kuomba kuongezwa juhudi zaidi ili kupunguza matatizo yanayojitokeza wakati wa utendaji wa kazi zake.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii adhimu kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa kunipa mashirikiano ya kutosha wakati wa kuupitia mswada huu unaokwenda na wakati kwa maendeleo ya nchi yetu ili ufanisi upatikane na kuweza kuinua kipato cha wananchi kwa kutoa maamuzi ya kufaa kwa lengo la kujiendeleza.

Mhe. Spika, matumaini ya kamati ni kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wataujadili kwa lengo la kuuboresha na baadae kuupitisha kwa pamoja kwa lengo la kuanzishwa sheria.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Baada ya kuwasilisha maoni yangu Mhe. Spika, naomba uniruhusu nichangie masuala japo mawili matatu katika mswada huu kwa maoni yangu binafsi.

Mhe. Spika, naipongeza sana serikali kwa nia safi iliyoonesha kwa lengo la kuwatafutia wananchi sehemu za mapumziko hasa baada ya kazi, kwa maana ya kuweka maeneo wazi ambayo yatatumika si vyenginevyo lakini kwa mambo ya mapumziko na mambo ya starehe zinazostahiki. Kwa mfano, katika eneo la Forodhani ni pahala ambapo serikali imetengeneza kwa pesa nyingi sana na pamekuwa pahala pazuri na watu wanakwenda kupumzika wale wanaopata nafasi kwa muda wao.
Mhe. Spika, mswada huu unazungumzia pia uendelezaji wa maeneo ya wazi kwa lengo lile lile la kuwapa burudani na mapumziko wananchi wetu.

Mhe. Spika, hilo ni jambo zuri iwapo dhamira hasa ya kuwekwa maeneo ya wazi itatekelezwa na itatekelezeka, lakini nashauri kwamba utaratibu huu ni mzuri na uendelee isipokuwa nina wasi kuwa baadhi ya maeneo ambayo serikali imetenga kuyafanya kuwa maeneo wazi yataleta matatizo ndani ya Mji Mkongwe.

Mhe. Spika, kuna maeneo wazi ambayo yametajwa na serikali na mabango yamewekwa kwenye maeneo haya kwamba yamehifadhiwa. Lakini maeneo haya bado yanatumika vibaya. Mhe. Spika, maeneo hasa ya Mji Mkongwe labda niseme karibu na eneo la Tembo Hoteli na Starehe Club pale pahala pana eneo liko wazi na pamewekwa bango, lakini eneo lile linatumika kinyume na makusudio ya dhamira iliyokusudiwa kutumiwa eneo hilo. Kwa hivyo, maeneo kama haya yasigeuzwe vijiwe, vijiwe ni pahala watu wanapokwenda wakaa na mambo yao, lakini vijiwe vyengine vinatumika kwa nia mbaya vijiwe vya kuvuta bangi, unga na mambo mengine.

Kwa hivyo, eneo kama lile Mhe. Spika naishauri serikali kuona kwamba umuhimu wa eneo lile lisiwe wazi kama lilivyokusudiwa, ili kuondokana na mambo kama haya basi naishauri serikali kwamba eneo lile litafutiwe mtu ama mwekezaji ama serikali kama ina uwezo wa kupaendeleza kwa kujenga kitega uchumi ambacho kitasaidia. Kama serikali bado haina uwezo wa kujikurupusha basi ni vyema pasiendelee kuwa eneo wazi ila papatiwe mtuu anayeweza kuweka kutega uchumi na sisi tukaweza kuingiza mapato kwa njia nyengine.

Mhe. Spika, kwa sababu pale ni pahala ambapo tayari pana hoteli iliyo kubwa lakini pana na mkahawa ambao ni mkubwa kwa hiyo ni vyema pale akatafutwa mtu au serikali ikaingia ubia au vyenginevyo pakawezwa kuendelezwa kwa majengo ambayo yatasaidia kukuza uchumi wetu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo maoni yangu binafsi na sasa naomba kuwasilisha taarifa hii rasmi na baada ya hayo nasema nakutakieni kila la kheri na mafanikio muweze kuuchangia mswada huu . Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha maoni ya kambi ya upinzani juu ya Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe wa Zanzibar Nam. 3 ya mwaka 1954 na kuanzisha sheria mpya ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe na Mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, nianze kutanguliza shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu aliyeumba ulimwengu huu na vilivyomo na ambaye uwezo wake usiokuwa na kikomo wala mipaka ndio uliotuwezesha kukutana hapa leo kwa min-ajili ya kutekeleza majukumu tuliyopewa kwa heshima kubwa na Wazanzibari.
Mhe. Spika, sasa nikushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani makini na mahiri juu ya mswada nilioutaja hapo juu, nakushukuru sana. Ahsante.

Mhe. Spika, kwa niaba yangu na ya wananchi wa Jimbo la Ole, tunawapongeza viongozi wetu wakuu wa kisiasa hapa Zanzibar, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa BLM Mhe. Amani Abeid Karume na Katibu Mkuu wa The Civic United Front – CUF kwa kuingia katika MARIDHIANO ya kihistoria, maridhiano ambayo yameleta utulivu wa kisiasa na amani endelevu. Hata pale Wazanzibari walipokosa huduma ya umeme kwa miezi mitatu walibaki kimya kama wanavyonyolewa. Ni imani yangu kwamba sisi Wajumbe wa Baraza hili tukufu tutakuwa ni mbolea na maji kuimarisha maridhiano haya kwa maslahi na manufaa ya Zanzibar na Wazanzibar wenyewe.

Mhe. Spika, mbele yetu tumeelekewa na mvua za masika na ambazo tayari zimeanza kunyesha na kujaza viwanja vya Mnazi Mmoja. Tumuombe Mwenyezi Mungu azilete mvua hizi, bila ya maafa yoyote na zineemeshe ardhi, mimea na viumbe vyote na kumimina baraka na neema ya mavuno na maji mengi ardhini ili tupate maji ya kunywa. Amin.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, sasa niruhusu nifanye kazi mahsusi ya kujadili mswada huu.

Mhe. Spika, nakiri kwamba nafasi yangu yakuwa Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na ujenzi ya Baraza lako tukufu imezimua sana mchango wangu kama Waziri Kivuli na Msemaji Rasmi wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Hii imetokana na kushiriki kwangu kikamilifu na kwa niya ya kujenga katika mjadala wa Mswada huu katika Kamati yangu ambayo inashughulikia Wizara za Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Hivyo basi, marekebisho yote yaliyofanywa na Kamati yangu wakati wa kujadili mswada huu tukiwa pamoja na uongozi wa juu wa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi na watendaji wake wakuu na wa mamlaka yenyewe, nayawafiki na yachukuliwe kwamba ni sehemu ya mchango wangu katika mswada huu.

Mhe. Spika, sasa ni miaka 16 tangu sheria Nam. 3 ya mwaka 1994 ya kuanzisha sheria Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe (MHUMM) ilipotungwa na Baraza lako tukufu na kuanza kufanya kazi. Kipindi hiki si kidogo kwa Mamlaka kuona mapungufu na kasoro na kupima ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mhe. Spika, Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe (MHUMM) ilipoanzishwa rasmi na kisheria, Mji Mkongwe wa Zanzibar haukuwemo katika orodha wa “maeneo ya Urithi wa Dunia” na maeneo ya “Hifadhi ya Dunia”. Hivyo basi, kwa kuzingatia masharti ya hadhi hii kubwa ya Kimataifa

tuliyopewa duniani ni sifa kubwa kwa Wazanzibari na kwa hivyo basi haja ya kuleta mswada huu ni jambo la lazima.

Mhe. Spika, pia ni imani yangu kwamba hadi waziri alipoona haja ya kuleta mbele ya Baraza lako tukufu mswada huu, kazi kubwa na nzuri ya matayarisho yake imefanyika. Hii ni pamoja na kuwashirikisha washirika husika.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kuzishauri Mamlaka, Mashirika na Taasisi nyengine za serikali nazo kufanya hivyo kwa madhumuni ya kukalafati, kuondoa kasoro na mapungufu yanayokwaza utekelezaji wa majukumu na shughuli za Taasisi hizo.

Mhe. Spika, baada ya mchango wangu katika kamati ninayoifanyia kazi, naomba niongeze mambo machache yafuatayo:

Mhe. Spika, imesuudi kwamba tunajadili mswada huu wakati huu wa mvua za masika na kwa mvua ya siku mbili tu, tayari viwanja vya Mnazi Mmoja vimeshajaa maji, na kwakuwa viwanja hivi sasa navyo ni sehemu ya maeneo ya Mji Mkongwe. Nashauri kwamba, Mamlaka katika mipango yake ya kuuendeleza na kuutunza Mji Mkongwe na mandhari yake, ibuni mipango na mikakati inayotekelezeka kupata ufumbuzi wa kudumu kuhakikisha kwamba tatizo hili linaondoka.

Mhe. Spika, athari na madhara kutuama kwa maji kwa muda mrefu katika viwanja hivi ni pamoja na kuzaliana kwa wingi kwa mbu wanaosababisha malaria, wana michezo kukosa viwanja vyao kwa kipindi kirefu, kuchafua mandhari nzuri ya mji wetu na kadhalika.

Mhe. Spika, ni bahati njema kwamba Zanzibar tuna wingi wa wasomi na wataalamu wazalendo katika fani mbali mbali na kwa viwango vikubwa vya elimu. Hivyo ni jambo la nadra kukosa msomi/mtaalamu mzalendo anayeweza kuongoza au kuendesha Mamlaka, Mashirika na Taasisi kubwa kubwa ziwe za kitaifa na kimataifa. Hivyo basi, hoja au pendekezo la kuwa Mzanzibari awe ni mtendaji mkuu (*CED*) wa taassi za hapa nchini ni la lazima.
Mhe. Spika, katika kifungu Nam. 38 nashauri kiongezwe kijifungu kidogo cha 38 (b) na kisomeke hivi:-

“38 (b) atakuwa na uwezo wa kupiga marufuku matumizi ya jengo au eneno lolote la Serikali katika Mji Mkongwe endapo ataona matumizi hayo yanaharibu sifa ya Zanzibar.”

Hivyo sasa kama kifungu cha 38 kiwe na vifungu vidogo vinne (a), (b), (c), (d).
Mhe. Spika, kwa kuwa sheria Nam. 3 ya mwaka 1994 sasa inafutwa na na sasa

kunaanzishwa sheria mpya ya mwaka 2010 kuchukua nafasi ya ile ya 1994, na kwa kuwa Kanuni na amri za Sheria Nam.3 ya 1994 zinaendelea kama zilivyo, nashauri kwamba waziri anayehusika na mamlaka afanye uharaka wa kutunga Kanuni za Sheria hii mpya ili sheria hii mpya tunaijadili hapa leo iende na wakati.

Mhe. Spika, nataka nichukue fursa hii kuumshukuru uongozi wa juu wa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi na watendaji wake wakuu kwa ushirikiano wao mkubwa na wa dhati wanaonipa kama Waziri Kivuli na Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi katika kutekeleza majukumu ya wizara hii. Naamini nami nimekuwa msaada mkubwa kwao katika kukosoa, kushauri, kuelekeza na kutekeleza yale ambayo yanaonekana yana manufaa kwa taifa hili.

Mhe. Spika, kabla sijasoma hizi *paragraph* mbili za mwisho nataka niungane na Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi.

Mhe. Spika, jingo la Starehe Club ni miongoni mwa majengo ya Mji Mkongwe, sasa hivi club ile haitumiki inavyotakiwa itumike na matumizi yanayofanywa sasa hivi ni sawa sawa na mtu aliyekalia jiwe la almasi, lakini anakwenda miayo kwa njaa. Starehe Club kama itapata mwekezaji madhubuti anaweza akaigeza club ile ama kwa kuvunja na kujenga upya kwa kufuata sheria za mamlaka ya Mji Mkongwe. Naamini kabisa inaweza ikawa ni kitega uchumi kama ambavyo sasa hivi Serena ilivyo. Serena Inn ni hoteli ambayo inaitangaza sana Zanzibar na ni imani yangu kwamba inajaza mifuko ya Mhe. Mwinyi Haji Makame.

Mhe. Spika, si hilo tu lakini sehemu iliyo Kaskazini mwa Starehe Club nayo ni sehemu la eneo lilokuwa wazi la Mji Mkongwe. Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima wakati umefika eneo lile kutafutwa matumizi madhubuti ambayo yatachangia sana uchumi wa Zanzibar na uwezekano huo nina hakika upo. Kwa hivyo, mimi nashauri kwa kupitia Baraza lako waziri anayehusika na Starehe Club kibiashara atakuwa ni Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji, lakini anayehusika na jengo la Mji Mkongwe ni Mhe. Mansour Youssuf Himid mawaziri hawa wawili wakae kitako waandae utaratibu ambao si muda mrefu tutapata habari nzuri za kufurahisha kwamba sehemu zile mbili zimetumika ipasavyo hasa ukiangalia kwamba uchumi wetu ni dhaifu na kumbe tunaweza kuuboresha kwa kutumia maeneo hayo mawili ambayo nayazungumza.

Mhe. Spika, mwisho, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii, nawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Ole kwa kuelewa na kuthamini juhudi zangu za kuwaletea maendeleo, na jinsi wanavyothamini michango yangu katika Baraza hili na zaidi namna wanayvoshirikiana nami katika utekelezaji wa majukumu

yangu. Aidha, nawashukuru sana Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza.

Mhe. Spika, kwa mara ya kwanza katika historia ya Baraza hili naunga mkono mswada huu na naomba kuwasilisha.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii kuwa mchangiaji wa mwanzo baada ya Mhe. Waziri, Mwenyekiti na Waziri Kivuli. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako hili tukufu kuchangia mswada huu wa sheria.

Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi pamoja na watendaji wote wa wizara hii kwa kazi zao nzuri hasa tukizingatia kwamba katika nchi yoyote duniani hakuna jambo zuri kuliko kuhifadhi miji yake au historia za mambo yake aliyokuwa nayo.

Mhe. Spika, mimi niseme tu kwamba kila sababu na haja ipo ya kutekelezwa haya juu ya sheria hii ya Mamlaka ya Hifadhi ya Uendelezaji wa Mji Mkongwe hasa tukizingatia kwamba sheria hii itawapa uwezo wenzetu kwa kusimamia vyema taaluma na sheria na kazi mbali mbali ambazo zitawagusa kwa kila siku.

Mhe. Spika, hapa kwetu Zanzibar Mji Mkongwe umekuwa ni kivutio kikubwa kwa watalii na hata wenyeji wa nchi hii. Kwa mfano, tukizingatia umaarufu wa mji huu Mamlaka inajitahidi kuhakikisha kwamba kila kilichoelekezwa wanakifuatilia na wanakiweka vizuri ili kuwa kivutio kwa wageni wetu wanaoingia katika nchi hii.

Mhe. Spika, mgeni yoyote anayetoka nje kama yuko kwenye boti kwanza atavutiwa na ile mandhari nzuri anayoiona katika upeo wa macho yake. Lakini akiingia katika mitaa atafuata ile historia halisi ambayo inajuulikana kama ni majengo ya hifadhi ya Mji Mkongwe. Mhe. Spika, hili ni suala zuri na la muhimu na sheria hii wenzetu watapewa nafasi ya kufanya kazi zao vizuri ili kuuendeleza mji wetu.

Mhe. Spika, mimi napenda sana kuangalia mambo mbali mbali katika ulimwengu kwa njia yoyote ile nitakayoweza kuitumia hasa tukiangalia mambo ya televisheni. Wenzetu wa TVZ wanakipindi kimoja ambacho ni muhimu sana kuonesha taaluma kwa wananchi juu ya kuhifadhi miji mbali mbali duniani. Kwa mfano, hivi karibuni wameonesha Mji wa Egypt wameonesha mambo mengi sana ya kale na wameonesha jinsi inavyohifadhiwa na tumeona mtiririko wa watalii wanavyoingia ili kuhakikisha kwamba uhifadhi una historia kubwa na uhifadhi una malengo ya kuzuia kile kilichokuwepo ili waliokuwa wageni waje wakione.

Kwa hivyo, mimi napongeza haya yote yaliyozungumzwa katika mswada huu na hasa tukizingatia kwamba bila ya haya hatuna kitu chengine chochote cha kivutio katika nchi yetu. Mhe. Spika, ukiacha ukanda mzuri wa *beach* katika sehemu zetu za pwani kuanzia Kaskazini hadi Kusini na baadhi ya Magharibi ya nchi yetu. Kwa hivyo, mimi nachukulia hifadhi ya Mji Mkongwe ni endelezo la maisha ya kila siku kwa sisi wenyewe na vizazi vyetu vijavyo, lakini hata kwa wageni wanaokuja katika nchi yetu kushuhudia hifadhi hizo.

Mhe. Spika, kwa kuwa kuna mambo mengi ya kuvutia katika mji huu mimi ningeishauri serikali kupitia wizara husika jambo la kwanza likaangalia majengo kama ilivyosemwa katika mswada huu kwamba majengo yatapitiwa. Lakini hivi sasa tulipo kuna baadhi ya majengo yamo katika hatari kubwa sana kuanguka, Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi tulifuatana siku moja katika maeneo fulani basi tuliona jengo moja ambalo limewekewa mwega ili lisiporomoke. Mhe. Spika, jengo hilo liko barabarani lakini wanafunzi wanapita kila wakati kwa hivyo mimi ningeishauri mamlaka hii pamoja na kwamba sheria hii haijawekwa saini ikalifuatilia lile suala na likaliangalia na kulipatia ushauri wa haraka kwa kunusuru maisha ya wananchi wetu ambao wengi wao wanapita usiku na mchana katika njia hiyo kubwa. Tukizingatia pia mchezo wa wanafunzi wanacheza pale pale karibu, pia wageni wetu wanaokuja ni hatari.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri hili tusingojee sheria hii itiwe sahihi, hii sheria itatiwa sahihi na kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu itapita tu haina tatizo, lakini tunaloliona sasa hivi basi tusione sheria itiwe sahihi.

Mhe. Spika, suala jengine katika suala la mamlaka ya Mji Mkongwe. Mimi nimeona mipaka yetu, hifadhi hii ina mipaka mingi ambayo barabara za Michenzani, yaani ukichukulia Michezani na barabara ya Bwawani iliyokwenda Kinazini na sehemu za Mnazi Mmoja na kwengineko. Basi mimi ningeishauri tena serikali kwamba kuna maeneo muhimu na maeneo hayo kama yatafanyiwa kazi na kupatiwa ushauri mzuri wa wataalamu tuliokuwanao basi naamini itakuwa ni kivutio pia kwa watalii katika nchi yetu.

Mimi ningeishauri serikali eneo la Hoteli ya Bwawani lililokuwa wazi kabisa lililotaka kujengwa bwawa na Marehemu Mzee Karume lakini alipotangulia mbele ya haki limeshindikana mpaka leo haikupatikana fursa ya kutembelea watalii katika eneo lile. Ningemshauri Mhe. Waziri yeye mwenyewe binafsi kupitia wenzetu wa Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji kwa sababu pia ni sehemu yao likafanyiwa maarifa eneo lile kwa kupatiwa miundombinu mizuri, naamini Mhe. Spika, litakuwa kivutio na uchumi wa nchi yetu na mazingira mazuri ya mji wetu yatapatikana.

Eneo lile ni mali sana kwa wenzetu kama tunaangalia nchi za wenzetu. Mimi nilibahatika kuiona Msumbiji, Msumbiji ni eneo zuri, ni eneo la mji wa kale unalingana na huku kwetu. Lakini pia nilichokigundua mimi kila hifadhi inayohifadhika utaikuta.

Kwa mfano, Mhe. Spika, nitakuja katika mambo ya historia kwa sababu hifadhi ya Mji Mkongwe ni historia. Sisi kwa hapa kwetu Zanzibar nchi yetu tuliipindua kwa marungu na mapanga, lakini bahati mbaya leo tukienda kwenye makumbusho zile zana tulizozitumia sijui kama zipo, sina uhakika. Lakini Msumbiji Mhe. Spika, walichokitumia cha kupiga risasi ya mwanzo wakasema tunaikomboa nchi yetu wamekiweka katika makumbusho yao.

Mhe. Spika, *radio call* walitumia, gari walizotumia, mizinga waliyotumia enzi hizo yote unaikuta imehifadhiwa katika makumbusho na imepambwa vizuri sana. Kwa hivyo, watalii wa nchi mbali mbali wanakwenda kusoma katika maeneo yale. Sasa mimi niiombe serikali kwa maeneo yetu mengi na tusingojee kuwa wizara gani inahusika na nini na nini, wao Mamlaka ya Hifadhi ya Mji Mkongwe ndio kivutio, ndio wawekezaji sasa hivi na wao ndio watakaoona hili linafaa na hili halifai.

Kwa mfano, tuna kanisa kuu hapa Mkunazini. Mhe. Spika, katika historia ya nchi yetu lile eneo ni muhimu sana, kama kuna waliopata fursa ya kwenda kusoma mle kwa sababu kuna mambo mawili katika nchi yetu, kuingia katika kanisa sio kugeuza dini, lakini katika kusoma utatafuta. Hata wenzetu Wakiristo wanaingia katika baadhi ya taasisi za Kiislamu kwenda kutafuta kuna nini na maelezo gani ya kihistoria. Kwa hivyo, mimi ningeishauri hali ya kanisa lile lilivyo na watalii wengi wanakuja basi hapa haja ya kufanyiwa ukarabati wa asili ili likawa kivutio zaidi kwa watalii wetu wanaokuja katika nchi yetu.

Mhe. Spika, ukiacha hayo, *Tumekuja Secondary School* ndio hifadhi ya Mji Mkongwe hiyo na kivutio kwa watalii, halkadhalika hayo hayo. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri kupitia wizara zinazohusika washirikiane katika taasisi mbali mbali zinazohusika watizame kitu gani cha Mji Mkongwe ambacho kitaleta manufaa na faida katika nchi yetu.

Jengine Mhe. Spika, bahati nzuri katika ramani ya Mji Mkongwe makumbusho yetu yote ya asili ya Mnazi Mmoja yamo katika Mji Mkongwe. Ningemuomba tena Mhe. Waziri ile ni alama tosha kwamba Wazanzibari wana kumbukumbu zao zinakaa katika sehemu zile. Lakini hivi sasa kidogo kutokana na hali za makumbusho yetu zilivyo, niseme tu kwamba haziko katika mwelekeo mzuri. Kwa hivyo, kupitia wenzetu wa Mji Mkongwe wanaweza kutoa rai yao na utaalamu wao yakafanyiwa ukarabati na matengenezo mazuri ilimradi wenzetu

wale wakikaa vizuri na wanaohusika na taasisi hizo basi tutakuwa na historia nzuri na watalii wataongezeka.

Kilichonifurahisha zaidi Mhe. Spika, nimeona kwamba wajumbe wa bodi mmoja ni Mkurugenzi wa Nyaraka na Mambo ya Kale. Kwa hivyo, yeye moja kwa moja anahusika na mambo haya niliyoyataka katika mambo ya historia. Sasa nimuombe na hili Mhe. Waziri waliangalie ili kuuweka mji wetu katika hali nzuri.

Mhe. Spika, katika nchi yoyote ulimwenguni baada ya kazi vijana, wazee, watoto hutakiwa wakae katika vikundi wafurahi. Mzee Aboud Jumbe, rais mstaafu Mwenyezi Mungu amuweke, alifanya kazi moja kubwa ya kutujengea viwanja vyetu vya sikukuu, kwa Unguja tuna viwanja vya Kariakoo na Pemba tuna viwanja kule Tibirinzi. Bahati nzuri alisema kwamba viwanja hivyo madhumuni yake kuwafurahisha watoto wetu siku za sikukuu na siku za mapumziko.

Mhe. Spika, viwanja hivyo vinaendelea lakini hivi sasa serikali baada ya kukaa na kutafakari kwamba kila rika watu wanahusika na kutembea au kukaa pahala wakapumzika, ndio maana serikali kupitia Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi na Mamlaka ya Mji Mkongwe tukabahatika kufanyiwa matengenezo makubwa sana eneo letu la Forodhani.

Hivi sasa kama anakuja mgeni yoyote ukimpeleka Forodhani anajiona kama yuko Ulaya, kitu chochote kutengenezwa na kusimamiwa. Mimi nawapongeza wenzetu hawa kwa kusimamia vyema na kuhakikisha kwamba usimamizi wao umeleta tija.

Mhe. Spika, binadamu yeyote ukimfahamisha anaweza kufahamu na akiwa hataki kufahamu ana lake. Mwanzo ulikuwa mgumu wananchi mtavaa hivi, mtapanga vitu vyenu hivi wakaona kama wanaonewa, lakini leo kama mtu kaivaa shati yake anaona ina doa atatafuta ile safi zaidi ili iwe kivutio kwa biashara yake.

Mhe. Spika, ningemshauri Mhe. Waziri lakini na wewe kama ni Spika wetu kwa haya tunayoyazungumza siku moja ukapata nafasi ukapita pale hasa wakati wa usiku ukenda kuangalia ile hali halisi ilivyo. Hali imebadilika na utasahau kama uko Zanzibar utajisikia kama uko wapi sijui. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri hili liendelezwe na lifanyiwe kazi.

Lakini bahati nzuri Mhe. Spika, Mkurugenzi wa Manispaa ni Mjumbe wa bodi hii itakayokuja, pia nimelifurahia. Kwa hivyo, kutokana na viwanja hivi vinavyosimamiwa na wao Manispaa kupitia Mji Mkongwe basi ningeshauri na

hapo *Jamhuri Garden*.

Mhe. Spika, *Jamhuri Garden* ni sehemu muhimu sana, ni mali, ni sehemu ambayo kama itapata mwekezaji kama Forodhani wenzetu wataingiza fedha nyingi na hapa hatutizami fedha tu, tunatizama mapumziko ya watu wetu baada ya kazi. Mhe. Spika, kuna burudani za aina mbali mbali, wengine hupenda taarab, wengine *Bongo Flavor*, kuna wengine kandanda na wengine wanapenda kukaa kupumzika tu na familia zao.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, hili ni suala ambalo litatusaidia sana katika mji wetu kuuweka katika haiba. Kwanza tumesema tunataka haiba ya mji wetu, basi kila eneo lenye mwelekeo basi lifanyiwe kitu ambacho kitasaidia kutokana na mwelekeo wa uboreshaji hasa tukizingatia wageni na wenyeji wana haki ya kutembelea katika maeneo hayo.

Mhe. Spika, kuna suala jengine nalo kwa upande mwengine ni muhimu vile vile, suala la usafi. Suala la usafi ningeiomba Mamlaka na ninaiomba kwa moyo wangu safi kabisa simuonei aibu mtu wala nisimuogope mtu, usafi ni chanzo cha afya njema, usafi ni kuweka mandhari safi, hiyo haiba tunayoitaka inakuja na usafi wa maeneo.

Mhe. Spika, kuna wageni wakifika kwanza wanaangalia mambo mawili tu, vipi njia hii safi? Vipi eneo hili usafi wake? Watu wanafuata mazingira tu.

Labda nitoe mfano mwengine Mhe. Spika. Kwa wenzetu kule Rwanda, kule watalii hawafuati kitu chochote baada ya usafi tu wa maeneo, kuanzia mjini mpaka vijijini na kule imewekwa siku maalum ya operesheni, kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi siku hiyo inaitwa siku ya operesheni usafi. Kila mwananchi nyumbani kwake hana haki ya kutembea kuanzia saa 12 asubuhi au saa 11 alfajiri mpaka saa 4 za asubuhi, ufanye usafi wako na mazingira yako yawe safi.

Sasa kule wenzetu wanapata faida mbili tu, kwanza ni huo usafi lakini pili Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu atuepushie isitokee kwetu labda kuangalia yale mambo ya vita yalivyotokea na ile halaiki ya vichwa vya wenzetu ambao wamefariki (mabaki). Mhe. Spika, hiyo si nzuri wala mimi siipendelei lakini ndio tuseme wenzetu wameweka historia tu, lakini kwa sisi sio nzuri.

Mhe. Spika, kama tutakwenda katika mwelekeo huo basi mafanikio yatazidi kuimarika hatua mbali mbali ambazo zinatuhusu katika mji wetu yatanufaisha.

Naamini kwa nia njema kabisa mswada huu ni muhimu na ni mzuri, kama tutafuata huu ushauri japo mawili matatu nilioutoa na mengine watayotoa

wenzangu basi tutapiga hatua kubwa sana katika kuuweka na kuhifadhi mji wetu huu katika sheria mpya ambayo itawapa nguvu wenzetu juu ya kuendeleza maisha yao ya kuenzi mji wetu huu kwa sisi tuliyopo na vizazi vyetu vijavyo.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache niseme kwa heshima kabisa na taadhima naunga mkono mswada huu mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani kwa asilimia mia moja na sina matatizo nao, naomba wenzangu nao wauchangia na tuupitishe. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza na mimi kuchangia katika mswada huu. Katika mchango wangu utakuwa ni wa jumla jumla.

La pili niseme kwamba mswada huu wa kufuta Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Uendeshaji na Uendelezaji wa Mji Mkongwe wa Zanzibar Nam. 3 ya mwaka 1994 na kuanzisha Sheria Mpya ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, tunataka kuanzisha mamlaka na mimi zaidi nitazungumzia juu ya mamlaka. tunataka kuanzisha Mamlaka ya Hifadhi ya Mji Mkongwe wa dunia pamoja na kuuendesha huu Mji mkongwe. Kwanza tujue tu kwamba huu Mji Mkongwe ni mji mkubwa sana, una eneo kubwa. Kama ulivyozungumzwa umeanzia tangu huko ulikoanzia Forodhani pwani yote *costal area,* ikipandisha moja kwa moja mpaka sehemu za Hospitali ya Manazi Mmoja mpaka makumbusho moja kwa moja kufuata barabara kuu kufikia Darajani, mpaka kuunganisha Malindi mpaka kwenye Bandari ya Malindi.

Hiyo sehemu ni kubwa sana na inahitaji kushughulikiwa vya kutosha. Kwa hivyo, hii ni mamlaka mpya ambayo tunaichagua, kwamba mamlaka hii iwe na uendeshaji mzuri katika Mji Mkongwe. Kwa hivyo, kama tukichagua mamlaka hii kuipa dhamana na dhamani ni kitu kikubwa sana, kinahitaji uadilifu, kinahitaji usimamizi, kinahitaji mambo yote ambayo yanatakiwa katika Mji Mkongwe, hakuna suala la kupuuza ndani yake.

Kwa hivyo, kwa ufupi nitasema kwamba mamlaka hii itakuwa na majukumu makubwa sana tena mengi na ya ulazima. Lakini pamoja na mamlaka hii kuna kitu muhimu ndani yake ambacho ni lazima kitu hicho kiwezeshwe, hii mamlaka inahitaji kuwezeshwa. Kwa sababu ndani yake kunataka kufanywa kitu kizuri na ndani yake kunaingia gharama, gharama nyingi zinahitajika kwa hivyo ni lazima mamlaka hii ipewe uwezo, mbali ya uwezo wa kuiwezesha, lakini pia uwezo wa kuwa na fedha za kutosha kuweza kukamilisha mahitaji yake yote.

Mamlaka hii ina kazi kubwa ya kulinda utamaduni, huu mji ni mkongwe mji wa asili, ni mji ambao wa kihistoria, una *culture* zake, mila zake, desturi zake, una kila kitu chake na una tamaduni zake. Kwa hivyo, hii mamlaka itakuwa na kazi kubwa sana ya kuweza kulinda utamaduni wa Mji Mkongwe. Mamlka hii itakuwa na kazi nyengine ya kukuza huu utamaduni pamoja na utamaduni uliopo lakini utamaduni huu ni lazima uendelezwe, ni lazima ukuzwe utamaduni huu. Kwa hivyo, hilo ni jukumu la mamlaka vile vile.

Mamlaka inataka kuendeleza shughuli zote zilizoko ndai ya Mji Mkongwe, basi hapana suala hapa la kutegea mamlaka hii iseme ifanye inavyotaka wao vyenginevyo utakuwa ile historia badala ya kuiendeleza inazidi kuporomoka.

Mamlaka hii inahitaji vile vile kutoa huduma, huduma ni kitu cha lazima, kwenye mji kama huu wa hifadhi ya Mji Mkongwe huduma ni lazima zipatikane mara kwa mara. Kwa hivyo, mamlaka hii ina kazi kubwa sana ya kutoa huduma ambazo huduma hizo zitahusiana katika suala zima la hifadhi ya Mji Mkongwe.

Vile vile kuna suala katika mamlaka hii ambalo wanatakiwa ni suala zima la miundombinu ni juu ya mamlaka hii kuendesha ndio hapo niliposema kuwa, pamoja na uwezo wa bodi, mkurugenzi mkuu na mkurugenzi mdogo, wote hawa watatakiwa kuishughulikia na kuandaa mbinu kadhaa wa kadhaa kwa sababu ya kuendeleza huu Mji Mkongwe.

Mamlaka hii pia inahitaji kusimamia maeneo yaliyo wazi. Mhe. Spika, katika sehemu ambazo nimezitaja ziko sehemu nyingi sana ambazo ziko wazi katika mji huu, si vizuri kwa muda wote sehemu hizi zikaachwa wazi.

Niseme tu kwa mfano, hapo tulipokubaliana kipindi cha nyuma cha kutengeneza bustani tu, ambapo chini ya uongozi wa Manispaa. Tumeona jinsi gani wameweza kutengeneza bustani Forodhani, bustani ambayo ni nzuri, ya kuvutia na bustani hii inaonesha kwa uwazi kwamba imetengenezwa kwa hali ya juu kabisa, gharama kubwa imepita katika matengenezo yake. Lakini vile vile utaona ni moja ambayo ni kivutio kizuri cha maendeleo ya Mji Mkongwe.

Katika huduma ambayo imekwishafanywa katika bustani ile vile vile inaonekana kwamba kunapatikana mapato ndani yake. Sasa hayo ni katika mambo ya mamlaka kuona kwamba vitu kama vile, zamani palivyokuwa pamoja na kuwa tulikuwa tunapiga kelele siku zote bustani ile itengenezwe, lakini sasa hivi bustani imekuwa ni nzuri sana yenye kupendeza na sasa hivi inatia *in come*, *madukhuli* yanaingia katika eneo lile. Kwa hivyo, hiyo ndio kazi ya mamlaka. Hivyo mamlaka wanayo kazi kubwa sana ya kuuendeleza Mji Mkongwe.

Katika maeneo yaliyo wazi kuna maeneo mengi yaliyo wazi na maeneo hayo yanahitaji yasiachwe kama yalivyo. Kama nilivyokwishazungumzwa kwamba kuna watu wanayatumia maeneo haya katika njia ambazo haziridhishi. Kwa hivyo, mamlaka hii ina kazi kubwa sana ya kuhakikisha maeneo hayo yaliyo wazi kuyaweka katika hali nzuri na kuweza kupata *madukhuli* ndani yake, isiwe wazi kwa sababu ya wazi. Ikiwa ni sehemu ambazo za uwazi zimewekwa *parking* bilashaka *parking* tunajua na faida zake zinazopatikana. Tumeona hapa Manispaa imeandaa sehemu mbali mbali za *praking* na *madukhuli* yanapatikana katika parking hizo.

Kwa hivyo, katika Mji Mkongwe kama kuna sehemu zilizokuwa wazi zinahitaji kufanyiwa *parking* basi *parking* hizo zitaweza kuleta *madukhuli* kwa ajili ya Mji Mkongwe. Mji Mkongwe una kazi kubwa sana, unahitaji matengenezo mengi.

Mhe. Spika, mimi ninachotaka kusema kwamba mamlaka hii imepewa uwezo kisheria wa kuweza kusimamia masuala hayo. Ni chombo chenye hadhi ya kisheria. Kwa hivyo, kama chombo hiki kimepewa mamlaka hayo basi kiweze kutumia mamlaka yake kwenye sheria hii.

Jambo jengine muhimu ambalo nalihisi mimi kwenye mamlka hii ni usimamizi mzima wa suala zima. Kwa sababu unaweza kuwa wewe ni kiongozi kama ni Mkurugenzi au bodi fulani imechaguliwa kuendesha pahala, ikiwa hakuna usimamizi basi hii hali haiwezi kupatikana ikawa nzuri.

Tunasema Mji Mkongwe tunataka tuuendeleze uwe mzuri, kama mamlaka hii imewekwa kisheria na itashindwa kufanya kazi zake kama ilivyopangiwa, kwa hivyo, nasema mamlaka hii itakuwa imeshindwa, ndio pale wenyewe labda walivyojipangia kwamba baada ya muda fulani mkurugenzi aondoke aingie mwengine, inaonesha hii ni kwamba labda kutakuwa hakuna *stability* ya wakurugenzi, ina maana waondolewe kutoka muda fulani kutokana na maendeleo yao wanayoendesha.

Kwa hivyo, kusimamia jambo ni kazi kubwa sana, inahitaji *perseverance* katika usimamizi, inahitaji kufuatilia katika mambo ambayo yameandaliwa. Sasa mamlaka hii ina kazi kubwa sana, bodi nzima wote wanahitaji kukaa sawa na kujipanga vizuri katika kuhakikisha kwamba maendeleo yanapatikana.

Kuna suala zima ambalo ni muhimu zaidi Mhe. Spika. Huu Mji Mkongwe ni wa kihistoria, una haiba yake. Sasa kama hii haiba tuliyoipata hatukuweza kuiendeleza huu hautokuwa Mji Mkongwe, yaani kama utaachwa ovyo bila ya kuangaliwa, bila ya kusimamiwa, bila ya majengo yake kufanyiwa ukarabati basi tutapoteza haiba. Kulinda haiba hii ni muhimu sana.

Vile vile kuna suala jengine ambalo nahisi linahitaji kuunganishwa. Katika Mji Mkongwe ni lazima ipatikane kamati ya wazee ambao katika mji ule kuweza ku-*share* taarifa mbali mbali, kuweza kukaa kitako wakaangalia ni kitu gani muhimu katika mji huu. Kwa hivyo, hapa nasema jamii iweze kushirikishwa kikamilifu ili nayo ijisikie katika mji wao Mkongwe kuwa na wao wameshirikishwa kikamilifu katika masuala yote. Kwa sababu katika Mji Mkongwe kuna hayo majumba, Mji Mkongwe na majumba yake ni makongwe, kuanguka wakati wowote yanaweza kuanguka, lakini na ukarabati unahitajika. Sasa usimamizi wa shughuli hii ni muhimu sana.

Halafu Mhe. Spika, kuna suala ambalo ni muhimu vile vile kuliangalia, huu Mji Mkongwe una sharti zake. Kuna wakati ambao wizara au manispaa inakuwua na uangalifu sana kwenye magari ambayo yanapita katika mji huu, sidhani kwamba katika mji huu utaruhusu aina yoyote ya magari kuingia, kwa sababu mji huu ni mkongwe na nyumba zake ni kongwe, haiwezekani kupitisha magari ambayo yana uzito mkubwa sana kwa sababu yanapopita magari makubwa sana yanaathiri majengo haya ya asili. Kwa hivyo, hilo nalo liangaliwe na lichunguzwe.

Mhe. Spika, unajua unapopewa dhamana, unapopewa kazi, bila shaka utakuwa na sera ambayo itakuwa inakuongoza kufikia pale katika malengo. Sasa tuangalie hii mamlaka sera yake ikoje? Na kweli hii sera ambayo wataipanga mamla hawa kweli itaweza kufikia kwenye malengo yake? Hili ni suala muhimu liangaliwe vile vile.

Mhe. Spika, katika Mji Mkongwe huu tulionao kuna majengo ya namna kwa namna, kuna majengo madogo na kuna makubwa. Mimi ninachokifikiria kwenye majengo haya ni lazima hii mamlaka iweke utaratibu maalum wa kuweza kuyapitia majengo haya kuangalia jengo gani ambalo sasa hivi kwa mujibu wa umri wake linahitaji baada ya muda fulani kufanyiwa ukarabati. Mimi siamini kwamba mamlaka hii ikae kitako iseme kweli mji huu upo na watu wanaishi ndani bila ya kuweza kupita katika nyumba na kuangalia jambo gani ambalo linaweza kuleta athari haraka haraka.

Kwa hivyo, mimi nafikiri ndani ya huu Mji Mkongwe haya majengo ambayo karibu kuweza kuanguka na kuna majengo karibu na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kama alivyozungumza Mhe. Ali Suleiman, kweli jengo lile kwa muda mrefu limewekewa mwega na watu hawaishi ndani ya jengo lile. Lakini pia linahitaji kufuatiliwa na kuweza kurekebishwa.

Mimi ninachokifikiria labda katika suala moja muhimu, katika huu Mji Mkongwe bila shaka tunapata hii Forodhani watoto ambao jioni jioni wanakwenda kupumzika na watu wazima na kuweza kupata vitu vya

kuburudisha roho zao. Lakini tuangalie unajua, tunapoweka *master plan* ya mji ni lazima tuhakikishe kwamba kuna skuli ndani yake, kuna afisi, kuna binadamu watu wazina na binadamu ambao tunawaita binadamu lakini ni watoto, wanahitaji mahala kuweza ku-*release* ile *energy* yao wakati wa jioni, watoe lile joto lao la kitoto. Ni lazima wapate mahala pa kuweza kujiburudisha. Je, hao watoto tumewawekea sehemu gani ambayo wanaweza kwenda wakati wa jioni wakafanya angalau *exercise* au kucheza cheza.

Kwa hivyo, katika Mji Mkongwe pamoja na ukongwe wake kila mahapa ziko sehemu zilizokuwa wazi wanaweza kutengewa watoto wakaweza kujiburudisha.

Halafu katika huu Mji Mkongwe ili kuipa haiba mji huu baada ya kukarabatiwa majumba na kuangaliwa, kupigwa *brash* kila baada ya muda, kuwekwa usafi wa mji huu, lakini usafi mkubwa zaidi ni usafi wa barabara zenyewe ambapo barabara nyingi haziwezi kupita magari ni barabara za miguu, pikipiki na vespa. Hizi sehemu za ndani zinahitaji mamlaka hii iwe makini sana kuhakikisha kwamba sehemu hizo zinapitiwa vizuri na zina usafi wa kutosha. Si vyema kwamba taka zinakaa siku tatu bado hazijaondoshwa, unajua harufu mbaya, tunaita *abominable stanch* kama vile harufu mbovu, uchafu.

Harufu hizi bwana katika miji hazifai, tuangalie hapo Darajani taka zinakaa siku tatu ambapo ni kazi ya Mamlaka ya Mji Mkongwe, ile ni *abominable stanch* unafumba pua, huwezi kustahamili harufu mbovu iliyoko pale. Kwa hivyo, hii iko katika mamlaka ya mji huu huu, hali ya mji ule taka zinakaa siku tatu mpaka zina-*decay*, zina-*decompose* pale pale taka zile jambo ambalo zinatakiwa ziondoshwe kwa haraka. Hili ni suala muhimu katika Mji Mkongwe, hatupendi kuona katika mamlaka hii inaacha uchafu kwa siku tatu mpaka taka zinaoza harufu mji mzima, unaingia ndani ya gari unafumba pua. Hii naisemea kabisa ili wakati wa kuingia katika shughuli zao waweze kuelewa nini cha kufanya.

Halafu kuna suala zima la malipo. Katika sehemu nyengine kuna mambo ya ada. Haya mambo ya ada tuyaweke vizuri na kumbukumbu za ada ziwekwe vizuri. Vyenginevyo itakuwa ada zinazopatikana katika majengo haya zinapita katika mfuko unaovuja. Maana kuna mifuko ya serikali mengine inavuja, haitiwi mwahala pake sawa sawa. Kwa hiyo, nasema hizi ada za malipo ambazo zinapatikana kumbukumbu zake ziwekwe vizuri na hesabu zake ziwekwe vizuri ili huu Mji Mkongwe uweze kusaidia katika fedha.

Wakati gani mwenye nyumba anaweza kuambiwa sasa unatakiwa uhame. Kuna wakati watu wenye nyumba zao wanazibomoa nyumba zao bila ya amri ya wizara hii. Kwa hivyo, ni suala muhimu kwamba hapa tunachokizungumza

kuwaelimisha wananchi kwamba kuna hili au likitokea hili mnatakiwa mfanye hivi. Kwa hivyo, itakapokuwa baada ya maelekezo ya muda mrefu, nafikiri hatua za kisheria zinaweza zikachukuliwa iwapo mtu amefanya ukaidi kwenye eneo ambalo ametakiwa mtu ahame kwenye jengo lile na bado akaendelea kukaa.

Mhe. Spika, katika mamlaka yetu hii tumetajiwa kuna Waziri, Mkurugenzi Mkuu na Bodi. Hawa wote ni watu muhimu katika suala zima la Mji Mkongwe. Haya ambayo tunayazungumza hapa hayakumhusu mtu mmoja tu, hata na sekta nyengine vile vile zinahitaji kusimamia Mji Mkongwe. Kama tulivyoona tunapochangia kwenye *cluster* za kilimo watu wanashiriki, wizara hii na sekta hii na ile. Hapa kwenye Mji Mkongwe ningelipendelea kwamba sekta kadhaa wa kadhaa ziingie ndani yake katika kusaidia hifadhi ya huu Mji Mkongwe. Kwa sababu Mji Mkongwe ni mji ambao una wageni wanakuja wakiuangalia na sisi tunapata madukhuli ndani yake.

Kwa hivyo, huyu Mkurugenzi Mkuu ni lazima awe mtengenezaji mzuri na aweze kuleta ufanisi. Vyenginevyo bodi hii ambayo iliyopo hapa kusimamia Mji Mkongwe pamoja na mkurugenzi, hawa wanahitaji kuangalia sera zao vizuri, wanahitaji kuangalia mipango yao vizuri na kuweza kuleta ufanisi wa Mji Mkongwe.

Lakini vile vile nilitaka nishauri kwamba labda waweke muda maalum wa kuweza kuzikagua hizi nyumba za Mji Mkongwe, zifanyiwe *follow up* halafu zifanyiwe ukaguzi. Ni wakati gani ambao wanapanga kuzikagua nyumba kwa sababu tusingoje nyumba imeshaanguka tukaja tukasema bahati mbaya au ndio siku yao imefika. Hii mamlaka, mkurugenzi pamoja na bodi wapitie waone kwamba panafanyika ukaguzi labda baada ya miezi sita au baada ya kila mwaka au wakati wowote wenyewe watakaohisi kufanya ukaguzi. Lakini ukaguzi lazima uwepo.

Kwa sababu nyumba hizi za kihistoria nyumba kongwe hazikujengwa kama nyumba zetu za kisasa kwa kutumia saruji kwa wingi. Nyumba hizi za sasa zinatumia saruji nyingi na zina uimara mkubwa sana. Lakini majengo ya majumba makongwe hayana saruji ya kutosha, ni udongo na majiti yaliyomo mle ndani katika dari zao na kuta zao. Ingawa ni jiwe lina *fitness* ya futi mbili upana au unene wake, lakini angalia dari yake. Dari yake ni ya majiti ingawa zimepangwa pacha pacha, pia inaweza ikaanguka mara moja.

Mhe. Spika, ningelishauri kwamba katika mamlaka hii iweze kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa majengo yake. Jambo la pili ninaloshauri kwamba ipatikane kamati ya wazee shirikishi iweze kushiriki katika mtandao mzima wa eneo lile la Mji Mkongwe.

Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa kuweza kutoa yangu japokuwa machache lakini nafikiri nimeeleweka. Mhe. Spika, naunga mkono mswada huu mia fil mia, ahsante sana.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, nakushukuru. Mimi sina mchango mkubwa sana lakini nataka niunge mkono kwa kutoa mawazo, nisiunge mkono bila ya kutoa mawazo.

Mhe. Spika, nataka nianze kifungu cha 3. Mhe. Spika, katika kifungu hiki kumefanywa masahihisho, nimeona tumepata asubuhi hii karatasi ya masahihisho. Lakini mimi bado nina mashaka na masahihisho yaliyofanywa. Masahihisho yaliyofanywa pale kunaanzishwa mamlaka, wao wamesema "inaanzishwa mamlaka". Sasa nafikiri wametafsiri Kiswahili, wamekwenda katika lugha ya kawaida hawakwenda katika lugha ya kisheria. Nadhani ni lugha iliyotumika kunaanzishwa kwangu mimi naona sahihi, kuliko kusema inaanzishwa. Lakini wanasheria wapo watatusaidia zaidi. Hayo ni mawazo yangu.

Halafu Mhe. Spika, nije katika kifungu cha 4 "Majukumu ya Mamlaka". Hapa Mhe. Spika, kitu ninachokibaini katika majukumu yaliyotajwa kuna jukumu la kukuza utamaduni wa Mji Mkongwe. Sasa suala ambalo mimi najiuliza, huu utamaduni wa Mji Mkongwe kwanza ni upi. Utamaduni huu tuuchukulie uliojengeka kuanzia lini. Maana utamaduni unakwenda sambamba na historia. Sasa unapozungumzia mimi napata shida sana kuujua utamaduni hasa wa Mji Mkongwe tukisema tunaanzia wapi. Tunaanzia baada ya mapinduzi au kabla ya mapinduzi. Mhe. Spika, hapa kidogo inanipa shida kuujua hasa utamaduni wa Mji Mkongwe ni upi.

Sasa hili labda Mhe. Waziri atakapokuja kufunga mjadala huu atanisaidia kwa kweli inanipa shida sana. Kwa sababu ukiuchukua utamaduni wa Mji Mkongwe kabla ya mapinduzi ni tofauti na utamaduni uliopo sasa. Maana utamaduni unajumuisha mambo mengi, ni kitu kipana. Inajumuisha kazi za watu, lugha za watu, tabia za watu, desturi za watu. Sasa desturi za watu waliokuwa wakiishi Mji Mkongwe kabla ya mapinduzi zilikuwa tofauti na waliopo leo.

Kabla ya mapinduzi Mji Mkongwe ilikuwa hakuuzwi vinyago, sasa kunauzwa vinyago. Ndio nikasema neno utamaduni ni neno pana sana, linajumuisha mambo mengi sana. Sasa huu utamaduni tunaotaka kuudumisha wa Mji Mkongwe ndio nasema ni wa kipindi gani. Hili suala naomba Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie kwa sababu linanipa shida kidogo kulitofautisha.

Mhe. Spika, jengine katika huu huu utamaduni wa Mji Mkongwe sijui kama nitakuwa sahihi au sio sahihi, maana yake mimi siku za nyuma Mji Mkongwe nilikuwa siujui. Hawa wanaotwambia sijui wanatwambia ukweli au wanatudanganya Mhe. Waziri utanisahihisha na wewe pengine utafanya *research*.

Mhe. Spika, watu wazima waliotuzidi ambao waliujua Mji Mkongwe zamani wanasema haukuwa utamaduni wa Mji Mkongwe kuwa na uchafu, kuwa na majaa, lakini leo umekuwa ni utamaduni wa Mji Mkongwe kuwa na majaa. Haukuwa ni utamaduni wa Mji Mkongwe majumba yakaachiwa yakaporomoka, leo kuna majumba kibao yameporomoka, kumeota magugu, magururu yapo. Sasa huu wote haukuwa utamaduni wa Mji Mkongwe.

Mhe. Spika, haya ilikuwa niyazungumze kwa sababu neno utamaduni ni neno gumu sana hasa kulitafsiri, lakini nasema baadhi ya watu wanasema kwamba utamaduni huu sio utamaduni wa Mji Mkongwe. Sasa sisi pengine tunaweza tukasema ni utamaduni wa Mji Mkongwe kwa sasa kuwa na magugu na machaka, lakini kwa zamani kweli haukuwa utamaduni. Maana utamaduni ni kitu ambacho kinakwenda na mabadiliko.

Mhe. Spika, jengine ni kifungu cha 6 ambacho kinazungumzia "Majukumu ya Mamlaka". Mhe. Spika, ukiangalia kifungu cha 4 kinazungumzia "Majukumu ya Mamlaka" na kifungu cha 6 kinazungumzia "Majukumu ya Mamlaka". Sasa ikiwa vifungu viwili hivi vinazungumzia kitu kimoja, kwa nini tuwe na *marginal note* mbili ambazo zote zinasomeka sawa sawa, mtiririko si ungekuja pale pale tu. Au sasa itabidi hiki kifungu cha 4 tukipe jina jengine na kifungu cha 6 tukipe jina jengine. Lakini haiwezekani ndani ya sheria moja una *marginal note* mbili ambazo zinasomeka sawa sawa. Mhe. Spika, sijui hili Mhe. Waziri atatusaidia vipi.

Lakini halafu nashindwa kutofautisha majukumu na kazi. Maana kuna "Majukumu ya Mamlaka" yametajwa kifungu cha 4, "Majukumu ya Mamlaka" yametajwa kifungu cha 6, halafu kuna "Kazi za Mamlaka" kifungu cha 7. Nini tofauti kati ya majukumu na kazi, labda watu wa lugha Mhe. Mohamed Ali Salim (Mulla) yupo atatusaidia maana yananichanganya mimi.

Mhe. Spika, suala hili nadhani wa kunisaidia zaidi ni Mwenyekiti wa Kamati kuliko Waziri. Lakini kwa sababu waziri ameyakubali marekebisho na mwenyekiti hana nafasi ya kuja kunijibu, basi Mhe. Waziri atabeba dhima ya kunijibu.

Katika kifungu cha 9(2)(a) kuna marekebisho yamefanywa "Sifa za Mkurugenzi Mkuu". Katika mswada inasema "Awe na digrii ya kwanza au

inayofanana nayo". Lakini hapa marekebisho yamefanywa "Angalau awe na shahada ya kwanza na inayofanana nayo". Hilo sina tatizo nalo, nayapokea marekebisho ya kamati. Lakini pameongezwa sifa nyengine "Awe Mzanzibari".

Mhe. Spika, ni sheria chache sana tunazozipitisha katika Baraza hili ambazo tunampa Mkurugenzi sifa ya Uzanzibari. Nadhani ni katika sheria ya vikosi ndio tuliyosema kwamba lazima wapiganaji wawe Wazanzibari. Lakini sikumbuki kama kuna sheria nyengine, kama zipo nitakuwa nimesahau, kwa hawa wateule tuliowapa sifa ya kuwa wawe Wazanzibari. Pengine inawezekana tumesahau na wenzetu hawa wamekumbuka.

Sasa Mhe. Spika, ushauri wangu kama hakuna sababu ya msingi ya kuiweka hii kwamba awe Mzanzibari basi tuifute. Kama hakuna sababu ya kipekee basi nadhani tuifute. Kwa sababu inawezekana tukahitaji Mkurugenzi mtu mwenye uzoefu wa mambo haya lakini tukamkosa Mzanzibari, tukampata mtu ambaye si Mzanzibari, pengine Mtanzania lakini ana taaluma sana tukapoteza hii fursa.

Lakini pia tukiona sasa hivi nafasi kubwa kama hizi lazima tushike sisi wenyewe tumejitawala, basi nadhani vile vile ningeshauri hii iwe kwa miswada yote tunayoileta katika Baraza iletwe ianishe kwamba *post* kuanzia mkurugenzi kwenda juu katika sheria hizi basi tuainishe. Lakini ikiwa sheria nyengine hazitaji sifa ya Uzanzibari, nyengine zinataja, itakuwa haipendezi. Mhe. Spika, nasema labda kuwe kuna sababu ya kipekee, kama kuna sababu ya kipekee nitakubali, lakini kama hakuna nitakuwa sikubali hili suala.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 11(2) mtiririko wake hautapatikana vizuri mpaka nisome juu. Hii inazungumzia juu ya "Wajumbe wa Bodi". Sasa wametajwa Wajumbe wa Bodi wameanzia Mwenyekiti, Mkurugenzi na wengine. Halafu kifungu 11(1)(d) "Wajumbe wawili watakaoteuliwa na waziri ambao watakuwa na ufahamu na uzoefu juu ya maeneo yaliyojengwa na uhifadhi".

Lakini kifungu (2) anasema "Angalau mjumbe mmoja wa bodi awe ni mkaazi wa Mji Mkongwe ambaye atateuliwa na waziri". Sasa swali langu, hii *sub section (2)* ya kifungu cha 11 ina uhusiano na hiki kifungu 11(1)(d) hapa juu au haina uhusiano. Kwa sababu kama ina uhusiano sasa sioni sababu ya kuwa na hiki kifungu kidogo cha (2). Nadhani ingeunganishwa na ya (d) tu ikasomeka tu kwamba Wajumbe wawili watakaoteuliwa na waziri na angalau mmoja awe anaishi katika Mji Mkongwe. Lakini tukifanya kama ni kifungu kizima kwa kuzungumzia tu kwamba awe anaishi Mji Mkongwe naona itakuwa haina maana.

Sasa kama huyu mjumbe mwengine ni tofauti na hawa wawili wanaozungumziwa katika (d) atakaoteua waziri sawa. Hata kama ni hivyo, basi itakuwa hakuna haja ya kuweka (2), ilikuwa badala ya ile (d) iwe (e) katika mtiririko. Lakini kama huyu mmoja ambaye anazungumzwa hapa atoke Mji Mkongwe ni hawa wawili atakaoteua Rais, basi ilikuwa iunganishwe tu itafutwe lugha nzuri iunganishwe tu katika ile ile (d). Nadhani ingesomeka vizuri zaidi kuliko hivi ilivyo.

Halafu Mhe. Spika, hapo hapo kifungu cha 11(3) mimi kinanipa shida kukifahamu naomba ufafanuzi wa Mhe. Waziri, labda nikisome hicho kifungu chenyewe.

Kifungu cha 11 (3):

> "Wajumbe wa Bodi watalipwa maposho kama ambavyo itakavyoamuliwa na waziri kwa mashauriano na mamlaka kwa mujibu wa kifungu cha 10 cha Sheria ya Mitaji ya Umma".

Mhe. Spika, kuna mambo mawili kwamba bodi ishauriane na waziri, lakini vile vile wazingatie kifungu cha 10 cha Sheria ya Mitaji ya Umma. Sasa kama mitaji ya umma, bahati mbaya sina Sheria ya Mitaji ya Umma tukaona inaelekeza nini hapa. Lakini kama kuna mashauriano na waziri ikiwa hiyo Sheria ya Mitaji ya Umma inamuelekeza waziri ilikuwa sioni haja tena kuitaja hapa. Lakini labda Mhe. Waziri atakapokuja atanisaidia imekusudiwa nini hasa. Kwa sababu hapa mamlaka itashauriana na waziri lakini vile vile kwa mujibu wa kifungu cha 10 cha Sheria ya Mitaji ya Umma. Kidogo inanichanganya sijui hasa kwa kweli nini kilichokusudiwa.

Mhe. Spika, kifungu cha 12 (2) naomba kukinukuu halafu nipate ufafanuzi.
"Bodi haitatoa uwezo wake kupitisha bajeti ya mwaka, karatasi ya mizania au maelezo ya hesabu zake".

Sasa hapa napo vile vile nimeshindwa kuifahamu vizuri kwa hivyo naomba kusaidiwa na wenzangu walioifahamu vizuri.

Mhe. Spika, nafikiri vile vile katika marekebisho nimeangalia tuliyoyapata asubuhi sijui ni kwamba nimekwenda mbio mbio. Lakini pia katika kifungu cha 14 "Makamo Mwenyekiti" naomba kunukuu.

Kifungu cha 14 (1):

> "Wajumbe watamchagua kutoka miongoni mwao kuwa Makamo Mwenyekiti".

Kifungu cha 14 (2):

> "Isipokuwa kwa uteuzi uliofanywa chini ya kifungu cha 12 (2) cha sheria hii, mtu hatofaa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti au Mjumbe wa Bodi mpaka:
>
> (a) awe na digrii ya mwanzo au inayofanana".

Nadhani hapa sahihisho hili sijaliona katika masahihisho tuliyopewa, bora tungekuja pale pale angalau shahada ya kwanza.

Mhe. Spika, nije katika kifungu cha 16 "Katibu" naomba kunukuu. "Bodi itateua Mwanasheria kuwa Katibu wa Bodi". Nayo kidogo hii lugha inanipa shida. Yaani inakusudiwa mtu mwenye taaluma ya Sheria awe Katibu, au mtu aliyeajiriwa katika serikali labda ni *State Attorney* au imekusudiwa vipi. Sasa naomba ufafanuzi kwa Mhe. Waziri kipi hasa kilichokusudiwa.

Mhe. Spika, kwa kumalizia mimi nina msisitizo juu ya mambo yafuatayo. Kwanza Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri akawa na mpango mahsusi wa kuyashughulikia majumba mabovu na majumba ambayo tayari yameporomoka muda mrefu, kuna mafusi yamekaa miaka na miaka ambayo yanaleta haiba mbaya katika Mji Mkongwe.

Lakini la pili uchafu Mji Mkongwe ni mwingi nadhani hauendani na utamaduni wake. La tatu biashara ya vinyago. Mhe. Spika, biashara ya vinyago si utamaduni wa Mji Mkongwe.

Mhe. Spika, jengine kuna ukuta pale bandarini hii gati mpya tunayoingilia kwenye maboti. Pale pana maegesho ya magari lakini kwa taarifa za juu juu sijui kama ni kweli Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi yupo atanisaidia kwamba wale Shirika la Bandari wametaka kujenga maegesho pale lakini nasikia wamekatazwa kuwa ule ukuta wakivunja pale wataharibu mandhari ya Mji Mkongwe.

Sasa ikiwa hili ni kweli mbona naona kidogo hakuna sheria iliyokuwa haina *exception*. Mimi nadhani hapa kidogo mngeregeza masharti ule ukuta ukavunjwa ikapatikana parking. Kwa sababu sasa ukiingia na gari mpaka uingilie katika mlango wa huku Shirika la Bandari. Sasa sio kila gari pale inaruhusiwa kuingia mpaka iwe gari ya mtu maalum. Mimi naona mambo mengine tufumbieni macho tusilete usumbufu uliokuwa hauna maana. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Ali Denge Makame: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia mswada huu wa Sheria ya Mamlaka ya Mji Mkongwe. Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mkurugenzi pamoja na watendaji wake kwa kuliona hili kutuletea mswada huu ili kupata kuuchangia na kutia baraka zake.

Mhe. Spika, kuundwa kwa Mamlaka ya Mji Mkongwe hii itasaidia kuhifadhi mji huu na majengo yake na kuleta faida kwa wananchi na serikali.

Mhe. Spika, kwa kweli baadhi ya nchi za wenzetu walikuwa na haiba hii ya Mji Mkongwe, lakini tu bila ya kutazama wala kutamathari wao waliyaporomosha majengo yao ili kuleta majengo mapya ya kileo yanayojulikana kama ma-*scraper* (maghorofa). Lakini sisi ule ustahamilivu wetu tumekaa nayo haiba hii na tukastahamili mpaka ikajulikana ni hifadhi ya Mji Mkongwe ya kitaifa ya ulimwengu.

Kwa hivyo, hili niwapongeze kwa ustahamilivu wao wote wafanyakazi wa Mamlaka ya Mji Mkongwe kwamba mpaka leo huu mji wetu tukawa nao na kuutunza ili kutuletea faida kwa wananchi na serikali kwa jumla.

Mhe. Spika, kwa kweli kama alivyozungumzia hapa Mhe. Ali Suleiman Ali, Mji Mkongwe unaleta haiba nzuri. Kama unatoka Bara ukiingia katika chombo tu basi ile unalala hata ukiamka ukiutazama mji wetu unakubabaisha na hasa maeneo ya Hospitali ya Mnazimmoja, Ikulu mpaka *Serena Hotel* jinsi ya vile majumba yalivyokarabatiwa na kuwekwa rangi nyeupe yanapendeza sana. Kwa hivyo, katika kuhifadhi Mji Mkongwe kutaleta maslahi mazuri kwa ananchi wetu.

Mhe. Spika, majengo yetu yote ya Mji Mkongwe kwa kweli sasa hivi yanahitaji kufanyiwa ukarabati na matengenezo mbali mbali, ili kupata kuongeza haiba zaidi ya kivutio.

Mhe. Spika, kwa kuwa mswada huu umeletwa nami nitauchangia. Kwa kuwa nilikuwa Mjumbe wa Kamati hii ya Mawasiliano na Ujenzi mengi nimeshayachambua na kuyaangalia, kwa hivyo nitauchangia kiufupi tu ili na mimi niongezee yale machache ambayo nilikuwa nimekusudia kuwa nayo.

Mhe. Spika, ni vyema kuhifadhi maeneo ya majengo, maeneo ya njia zile zilizokuwemo katika majengo. Mpaka sasa hivi kuna baadhi ya njia nyingi kipindi cha nyuma zilijengwa kwa *tiles*, lakini utakuta katika njia hizo ambazo zilikuwa zimekaa vizuri tu watu kwa makusudi wanazing'oa *tiles* wanafanya mambo yao mengine waliyoyakusudia. Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri watu waliokuwa na mtindo huo wakawajibishwa ili kuondosha matatizo haya ya kuharibu haiba ya barabara zile.

Mhe. Spika, kwa kweli katika mji wetu huu Mji Mkongwe, katika ukurasa wa 53 kifungu cha 32 kinazungumzia masuala ya majumba yaliyohamwa. Utakuta katika mji wetu mkongwe kuna majumba mengi yamehamwa na mengine mabovu. Sasa baadhi ya watu yale majumba mabovu wameyafanya kama ni majaa, badala ya kukusanya taka zao na kupeleka kwenye majaa basi wamekuwa wanayatumia majumba yale kwa kuweka taka na kuyafanya majaa. Jumba limehamwa basi linatolewa madirisha, utakuta ndani yake mnatupwa mapolo na taka mbali mbali. Kwa hivyo, ile inaharibu haiba ya mji wetu na ambapo mji wetu huu tumeshautangaza kuwa ni wa kimataifa.

Kwa hivyo, ningewaomba wahusika wa mji mkongwe wakajaribu kuzitembelea nyumba zile ambazo zimehamwa au zimefanywa majaa ili kuwajua wamiliki wao na kuzungumza nao na kufanya utaratibu wa kuzuia masuala yale ya kuyafanya majaa majumba yale.

Vile vile Mhe. Spika, mji wetu mkongwe kwa kweli kuna baadhi ya majengo mengi ni mabovu, lakini wakaazi huwa hawajali ubovu uliokuwemo wao wanakaa tu, mpaka itokee ajali mtu limporomokee au limwangukie, kwa hivyo pale ndio wanashtuka namna ya kutafuta ukarabati au utengenezaji.

Kwa hivyo, ni vyema mamlaka hii mpya ambayo tunataka kuipitisha hapa, basi ishirikiane na wahusika wa maeneo, wakiwemo masheha au wajumbe wa sheha ili kuyatambua majumba hayo ambayo yaliyokuwa katika hali mbaya kuyapitia na kuyafanyia ukarabati kwa kushirikiana nao au kutafutwa wafadhili, ufanywe ubia ili kuyaweka katika hali ya usalama na kuondosha maporomoko yatakayowatokezea wale wakaazi wanaokaa katika majengo yale. Kwa hivyo, ni vyema mamlaka ikapanga taratibu zake ikiwa kwa mwaka mara moja au kwa kila ikikaribia misimu kama hii ya mvua kuwatembelea katika majengo hayo ili kutizama usalama wa majengo yale yalivyo.

Mhe. Spika, kwa sababu kuna majengo ambayo ukipita utayakuta yamekuwa na nyufa kubwa au yameinama kwa kuelekea katika maeneo ya njia ambayo wanapita watu wa aina mbali mbali, kwa hivyo baada ya kutokea matatizo yale ya ubovu basi kuna hatari ya kuwahatarishia maisha wapita njia au wale wakaazi wanaokaa mule ndani. Kwa hivyo, ikiwa mmiliki hali zake zimekuwa ngumu za kulifanyia ukarabati au matengenezo, kwa hivyo aitwe na kushauriwa ili wakitokea wahisani kama nilivyozungumza kufanywe ubia ili yafanyiwe ukarabati majengo yale.
Mhe. Spika, kwa kweli huu mji tumeshautenga kuwa ni mji wa historia na mji mkongwe ambao utaleta maslahi kwa nchi yetu. Kwa hivyo, ni vyema majengo yale tukayabadilisha angalau kwa miaka mitano mara moja kwa kuyawekea rangi nyeupe, kwa kila mmiliki akawa na taratibu hizo kwa majengo yale kuyabadilisha kwa kuyatia rangi.

Mhe. Spika, leo utapita baadhi sehemu nyengine *tiles* nzuri lakini jengo utakuta limefanya mwamba na kuota miti ya aina mbali mbali. Kwa hivyo, kuwekwe utaratibu maalum kati ya miaka mitano angalau mara moja lifanyiwe ukarabati wa kutiwa rangi. Itizamwe tu rangi ambayo inaweza kuvutia ikiwa ni nyeupe au rangi yoyote ambayo itaonesha kuwa hii ni mamlaka ya mji mkongwe. Hilo ningemshauri Mhe. Waziri akaliangalia pindi atakapokaa na washauri wake wakalifanyia ukarabati.

Mhe. Spika, mara nyingi wananchi hapa ukiwaambia masuala ya mji mkongwe, wengi huwa tunafikiria kutoka barabara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja mpaka Malindi Polisi, ukitoka huko hospitali maeneo ya mkono wa kushoto yote ni majengo ya mji mkongwe, lakini baada ya maongezeko na matanuzi yamefika mpaka Michenzani, Mkamasini. Kwa hivyo, utakuta katika maeneo hayo kuna nyumba vile vile za zamani ambazo ni kongwe nyumba ndogo ndogo tofauti na majumba ya ghorofa.

Kwa hivyo, kwa kuwa tunahifadhi majengo ya mji mkongwe hata mule kuna baadhi ya maeneo kuna nyumba zile za zamani ambazo zimejengewa miti, kwa hivyo kuna haja zikawepo kama sehemu maalum kama nyumba tano au kumi zikawa zinahifadhiwa ili katika wanaokuja kutembelea mji mkongwe wakaoneshwa na mazingira ya nyumba zile ndogo ndogo ambazo zimejengwa katika hali ya miti. Kwa hivyo, nalo hili Mhe. Waziri kama itawezekana basi aliangalie.

Halafu Mhe. Spika, katika mji mkongwe wetu huu kihistoria tunaambiwa kisiwa ambacho kilikuwa kimezungukwa na bahari ambapo miji huu uko kwenye mwamba ambao unaelea kwenye bahari. Lakini humu sikuona pahala ambapo kumeidhinishwa kuwa mji mkongwe huu mwanzo wake ulikuwa kama kisiwa. Kwa hivyo, hilo kama linahitajika ni vizuri kulieleza ndani ya maelezo haya ili kupata uelewa zaidi kwa wale wageni ambao wanatembelea mji mkongwe huu.

Mhe. Spika, kwa kweli mimi kama nilivyoeleza mwanzo kuwa katika mswada huu sitokuwa na mchango mkubwa sana, kwa kuwa nilikuwa ni mjumbe wa kamati. Kwa hivyo, naunga mkono mswada huu kwa kushirikiana na wenzangu tuupitishe bila pingamizi yoyote. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Ahmed Nassor Mazrui: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuongea katika kipindi hiki na kutoa mchango wangu juu ya hoja hii muhimu ya mabadiliko ya sheria katika mji mkongwe.

Mhe. Spika, mimi nimekulia katika mji mkongwe, nimekaa muda mrefu kwa hivyo nina uzoefu wa kutosha katika mji huu. Vile vile nina vitega uchumi

katika mji mkongwe na pia ni mkandarasi. Kwa hivyo, afisi hii ya mji mkongwe ni moja katika afisi ambazo kila mara huwa naipitia. Kwanza kabla ya kuanza naomba nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na kikundi kizima cha wasanifu katika wizara yake kwa kuweza kufikiria suala hili muhimu kabisa hasa kwa wakati huu ambao imeletwa mbele yetu tuijadili.

Mhe. Spika, kwa kweli wamejitahidi sana kuangalia vipengele mbali mbali na pembe mbali mbali ambazo zitaweza kuweka sheria hii na kuibadilisha ili iende kwa wakati na vile vile iweze kukidhi haja ya hadhi ya mji mkongwe hasa unavyotakikana.

Mhe. Spika, mji mkongwe kwa sasa hivi ni pahala muhimu sana, kwani imekuwa tukiongea suala la Zanzibar basi tunaongelea mji mkongwe. Watalii wote wanakuja hata ikiwa wamekaa Kiwengwa na kwengineko basi watakuambia tutakwenda *tour* katika mji mkongwe. Mji mkongwe wetu una hazina kubwa sana. Una hazina ya kuwa na majumba ya kale ambayo ndani yake muna mahospitali, ikulu, mahoteli, masoko, maduka, misikiti, makanisa, makumbusho, maofisi, maskuli, vitalu, makaburi. Vile vile tuna Chuo Kikuu na mambo mbali mbali. Lakini zaidi kuna suala muhimu sana la kiuchumi la bandari ya Zanzibar. Bandari ya Zanzibar imo katika mji mkongwe wetu. Kwa hivyo, kwa kweli mji mkongwe ni pahala muhimu sana katika uchumi wa Zanzibar na katika shughuli za kila siku za Zanzibar.

Mhe. Spika, ningependa kuchangia machache katika hoja hii kwani nahisi kwamba mambo mengi sana yametiliwa mkazo na yameangaliwa, lakini nahisi kuna mambo madogo madogo ni heri tukaboresha ili hali ikawa ni nzuri zaidi.

Mhe. Spika, nianzie katika ukurasa wa 46. Kuhusu kazi za mamlaka mwenzangu ameshaziongelea kwamba mamlaka na majukumu zinarudia hizo kwa hizo. Lakini ukenda katika ukurasa wa 46 muundo wa mamlaka.

Mhe. Spika, katika ukurasa huu wa 46 lakini unajadiliwa ukurasa wa 47 ni kuhusu mkurugenzi mkuu, ambao unasema;

Kifungu cha 9(2)

> “Mtu hatofaa kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu mpaka awe;
> (a) Na Digrii ya kwanza au inayofanana nayo;

Mhe. Spika, halafu katika ukurasa huo huo katika kifungu cha 10(5) na (6) naona zinapingana, vinasema;

Kifungu cha 10(5)

> "Bodi itateuwa mawakala, washauri waelekezi, na wataalamu wa mamlaka kwenye maeneo tofauti kwa vipindi na masharti ambayo mamlaka itaangalia mara kwa mara".

Kifungu cha 10(6)

> "Bodi itaanzisha utaratibu mzuri wa uchaguzi wa wafanyakazi wote, mawakala, washauri waelekezi na wataalamu".

Mhe. Spika, sasa huku kwenye nambari 5 kuna kuteuwa na nambari 6 kuna uchaguzi na mawakala, washauri waelekezi na wataalamu wamerudi tena yaani kwenye vifungu vyote wamo.

Mhe. Spika, kifungu nambari 8 kwa kweli nataka niwapongeze sana kwa kuona kwamba suala hili ni muhimu sana na limetiliwa mkazo. Kwa kweli kifungu hiki ni kizuri sana na naomba kibakie kama kilivyo.

Mhe. Spika, tukija kwenye ukurasa wa 48 kifungu cha 11(d) na kifungu cha 11(2). Mhe. Spika, ukija kuangalia hapo na ukiangalia katika ukurasa huo huo kwenye kifungu cha 14(2) ambacho kinasema;

Kifungu cha 14(2)

> "Isipokuwa kwa uteuzi uliofanywa chini ya kifungu cha 12(2) cha sheria hii, mtu hatofaa kuteuliwa kuwa mwenyekiti au mjumbe wa bodi mpaka;
> (a) Awe na digrii ya mwanzo au inayofanana;"

Mhe. Spika, kwa sababu kifungu cha 11(2) kinasema;

Kifungu cha 11(2)

> "Angalau mjumbe mmoja wa bodi awe ni mkaazi wa mji mkongwe ambaye atateuliwa na waziri".

Sasa huku chini kwenye kifungu cha 14(2) kinasema kila mjumbe mpaka awe na digrii. Mhe. Spika, naona hapa pataleta matatizo makubwa sana.

Halafu ukurasa huo huo wa 48 kifungu cha 12(2) ambacho kinasema;

Kifungu cha 12(2)

> "Bodi haitatoa uwezo wake kupitisha bajeti ya mwaka, karatasi ya mizani ya mwaka au maelezo ya hesabu zake".

Mhe. Spika, hii mimi sijaielewa, kwa sababu ukenda katika ukurasa wa 57 kifungu cha 46, 47(1)(a)(b) na 47(2) vinapingana na kifungu hicho cha 12(2).

Mhe. Spika, tukienda katika ukurasa wa 49 kifungu cha 20(2) ambacho kinasema;

Kifungu cha 20(2)

> "Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hichi maamuzi ya bodi yanaweza kuamuliwa bila ya kufanyika kikao kwa kusambaza nyaraka husika kwa wajumbe wa bodi, na mtazamo wa wajumbe wengi wa bodi ndio yatakayokuwa maamuzi ya bodi, lakini mjumbe yeyote atakuwa na haki ya kuomba maamuzi ya bodi yatenguliwe na shauri hilo lijadiliwe kwenye kikao cha bodi".

Mhe. Spika, kifungu hiki mimi nina mashaka nacho naomba kiangaliwe tena. Halafu ukurasa wa 50 ambapo kuna sehemu ya nne ambayo inasema, 'Uwezo na Shughuli za Mamlaka'. Katika kifungu cha 26(1) ambacho kinaeleza kwamba,

Kifungu cha 26(1)

> "Kwa uwezo uliotajwa hapo juu, Mamlaka inaweza baada ya kutoa notisi ya saa isiyopungua ishirini na nne (isipokuwa kwenye hali ya dharura) kuingia kwenye jengo lolote, makaazi au eneo ndani ya eneo la hifadhi kwa kufanya ukaguzi na kuangalia hali ya jengo au nyumba na kutoa au kuacha kwenye jengo au nyumba notisi ya maandishi kwa mmiliki wa jengo au nyumba inayomuelekeza miiliki wa jengo au nyumba kufanya kazi za hifadhi ndani ya kipindi kilichoelezwa ndani ya notisi hiyo".

Mhe. Spika, mimi nasema kwa muda huu wa masaa 24 na kwa mji mkongwe ninavyoujua ni muda mdogo sana kufanya shughuli hiyo na kwa kweli itakuwa tumemnyima fursa na kuvunja haki za binadamu. Angalau huyo mmiliki au huyo mwenyewe apewe masaa 72 au kuwe na jambo la dharura, lakini kama hakuna jambo la dharura basi masaa 24 ni madogo sana, ningeomba Mhe. Spika, yaongezwe angalau yawe masaa 72.

Kifungu cha 26(2) Endapo;

Kifungu cha 26(2)(a)

> "Mamlaka itakuwa na mawazo kuwa kuna jambo lolote linafanywa kinyume na ilivyoelekezwa kwenye notisi

iliyotolewa kwa mujibu wa kifungu cha 27(1) au kifungu chengine chochote cha sheria hii au amri au kanuni zilizofanywa chini ya sheria hii mamlaka kwa haraka itatoa notisi ya kujulisha kosa kwa mtu kwenye dhamana ya kosa hilo".

Kwa hapo Mhe. Spika, naona kama kuna kosa.

Mhe. Spika, halafu nikienda katika ukurasa wa 51 kifungu cha 26(2)(c) ambacho kinasema;

Kifungu cha 26(2)(c)

"Ikiwa amri ya kusimamisha haijatekelezwa mamlaka inaweza bila ya kutoa taarifa nyengine yoyote kuchukua hatua muafaka ambazo zitajumuisha kubomoa, kuharibu au kuangusha chini umbile lililotengenezwa kinyume na amri ya kusimamisha na mamlaka itakuwa na haki ya kurudishiwa gharama zake".

Mhe. Spika, hapa mimi ningeomba kwamba angalau huyo mkosa angepewa nafasi ya kujitetea katika jopo lolote lile kabla ya kuvunjiwa hicho alichojenga.

Mhe. Spika, tukiendelea mbele katika ukurasa wa 53 kifungu cha 30(4) ambacho kinasema;

Kifungu cha 30(4)

"Kwa madhumuni ya kifungu hiki, itakuwa ni jukumu la mamlaka kuanzisha na kutambua makundi ya watu na taasisi za kufanya nao ushauri".

Mhe. Spika, kama hili ni jukumu nafikiri ni vyema likaachwa kule katika majukumu ya bodi, kuliko kuletwa huku mbele.

Mhe. Spika, katika sehemu ya tano, kifungu cha 33(1) ambacho kinasema;
Kifungu cha 33(1) "Endapo waziri ataridhika kuwa;

(a) "Notisi iliyotolewa chini ya kifungu cha 27(1) haijatekelezwa; au

(c) "mmiliki wa jengo ndani ya eneo la hifadhi hataki kutekeleza notisi iliyotolewa kwake chini ya kifungu cha 27(1)"

Mhe. Spika, nikiangalia katika kifungu cha 27 sioni totisi, ambapo kifungu hiki kinasema;

Kifungu cha 27

> "Bodi itatakiwa kufanya mapitio ya mara kwa mara ya viwango, malipo yaliyoainishwa chini ya kifungu cha 8 cha sheria hii".

Sasa Mhe. Spika, sielewi hii pengine imekosewa au vipi, lakini waziri hakuna notisi huko.

Vile vile napenda nikipongeze kifungu hiki cha 33(4) katika ukurasa wa 54 ambacho kinasema;

Kifungu cha 33(4)

> "Maeneo yote ya hifadhi yaliomo ndani ya eneo la hifadhi itapoanza kutumika sheria hii yatasimamiwa na mamlaka, na mamlaka itapewa mkataba wa ardhi hizo".

Mhe. Spika, hili ni suala muhimu sana, lakini vile vile na majumba yote ambayo yako chini ya mji mkongwe ningeomba nayo yapewe nyaraka za kumiliki majengo hayo. Kwa sababu kuna sehemu nyingi sana hata mawizara wana majengo, lakini hawana miliki wa majengo hayo. Kwa hivyo, suala hili la kwamba hivyo vikataa au vitalu vikitolewa na mji mkongwe itapatiwa sheria ya kuwa na nyaraka hizo ni suala muhimu sana na mimi nalitilia mkazo sana. Sio vitalu tu, lakini hata majengo vile vile.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningeomba kuchangia hapa ni katika ukurasa wa 55 kifungu cha 38(a) ambacho kinasema;

Kifungu cha 38(a)

> "Waziri anaweza kwa kuchapisha tangazo kwenye gazeti kutekeleza yafuatayo:
>
> (a) kutoa sehemu ya uwezo wake wowote kwa mamlaka;

Mhe. Spika, suala hili mimi ningeomba mulifikirie mara mbili mbili, kutoa sehemu ya uwezo wake wowote kwa mamlaka. Huwenda suala hili likaleta matatizo sana kwa mamlaka ya waziri kuyapeleka kule na akayatia kwenye gazeti.

Jengine Mhe. Spika, ningeomba kwenda katika ukurasa wa 57, nafikiri nimelizungumza hilo kwamba, huku kuna suala la malipo ya kodi jengo au

kwenda kwenye fedha za hifadhi. Ukiangalia vifungu vya 44, 45, 46, 47 vinakwenda kinyume, bodi haitakuwa na uwezo wa kupitisha bajeti ya mwaka katika Tanzania imalize hesabu zake. Wakati huku bodi inatakiwa kupokea matumizi ya fedha yanayofanywa na mamlaka na shughuli za mamlaka. Mbali na madeni ya mamlaka ambayo tunakutana nayo kila mwaka wa fedha na mizani ya fedha inaonesha taarifa za mapato na matumizi na madeni yote ya mamlaka. Kwa hivyo, ukiangalia kipengele hiki hapa na kile kule cha ukurasa wa 48 kina matatizo. Ningeomba Mhe. Spika, haya yaangaliwe na zaidi ya hapo ningeweza kuchangia zaidi mambo matatu au manne.

La kwanza Mhe. Spika, nataka niwapongeze sana kwa namna bustani ya Forodhani inavyotunzwa. Bustani ile siku iliyofunguliwa kila aliyehojiwa katika TV alisema hapa bwana tunafikiri kwa muda wa wiki moja itakuwa hali ni mbaya sana, kwa hivyo ilikuwa ni *challenge.* Kwa kweli mji mkongwe wameutengeneza, pale pahala pako safi, bustani imeimarika na hali ni nzuri ya kutosha.

Mhe. Spika, linalovunja moyo mji mkongwe ni manispaa yetu ya Zanzibar. Manispaa ya Zanzibar utendaji wake wa kazi ni mbovu sana, na ndio maana unapelekea kuona kwamba mji mkongwe unanuka, mji mkongwe ni mchafu na kwa vile mji mkongwe hauna mamlaka ya kuingia katika sehemu zile, basi utakuta kuna tofauti kubwa sana baina ya ile *park* ya Forodhani na sehemu nyengine za mji mkongwe. Sikuona katika hoja hii jukumu lote la mji mkongwe kuhusiana na suala la usafi. Kwa kweli ikiwa mji mkongwe utauachia suala la usafi baraza la mji, basi nafikiri hiyo *cultural* ya Zanzibar itakuwa ni uchafu na ambapo sio.

Mji mkongwe bwana ninavyofahamu mimi asubuhi una harufu yake, mchana una harufu yake na usiku una harufu yake. Hizi harufu tatu mbali mbali. Leo harufu zimechanganyika, ukenda hapa utasikia harufu hii ukenda huku harufu hii. Kwa hivyo, mji mkongwe umebadilika kabisa. Kwa hivyo, mimi ningeomba kwamba suala la usafi wa mji mkongwe kuwaachia baraza la manispaa ni kuudhulumu mji huu na kuutoa hadhi yake yote ya usafi wa mji mkongwe.

Mfano mzuri tuangalie *Forodhani Park* inavyoangaliwa. Ikiwa baraza la mji hawawezi kuiga hali ile, basi nahisi mji mkongwe ungechukua nafasi ya kuweza kujua namna gani itaweza kuchukua nafasi ya kusafisha mji wake. Vyenginevyo huu mji hiyo mila yake itakuwa ni ya uchafu na ambayo sio mila ya Mzanzibari na sio mila ya mji mkongwe.

Mhe. Spika, nikiendelea mbele nasema kwamba siku za skukuu ya iddi au sikukuu nyengine, hasa skukuu ya iddi. Siku ya skukuu ya iddi ukija Forodhani

imejaa na watu wako pacha pacha kama chana ya ndizi vile, hamna nafasi hata ya kwenda hapa na hapa. Hii inaonesha kwamba sehemu imependwa na imependeza, lakini ni ndogo sana ukiangalia na hali halisi ya idadi ya watu waliokuwepo katika mji huu.

Mhe. Spika, ingawaje kuna mnazi mmoja, ukenda mnazi mmoja mpaka leo baraza la mji wameshindwa kuboresha ile hali ya skukuu zaidi. Tangu enzi za mkoloni ukija wewe mabanda yale ya magunia na vipolo mpaka leo hali ni ile ile hakuna maendeleo kwa hili. Kwa kweli hali ile inatudhalilisha sana sisi. Kuona kwamba kwa muda wa miaka 40 kabla ya mapinduzi *festval* zetu ambazo zinasimamiwa na serikali, zinashindwa na *festival* zinazosimamiwa na NGOs. Tuangalie *festval* ya Sauti ya Busara na *festval* nyengine ni nzuri tu. Lakini *festval* inayosimamiwa na baraza la mji hapo mnazi mmoja haitamaniki ni aibu na fedheha, magunia, vipolo na makuni tafrani moja kwa moja. Sasa kwa kweli hii mnazi mmoja iko katika mji mkongwe loo! Mbona hatari, siku za skukuu ndio wageni wanakuja kutoka kila pahala kuja kuangalia *festval* yetu ile, wakifika mnazi mmoja eeh! Hapatamaniki.

Kwa hivyo, mimi ningeomba suala hili lingeangaliwa tena ili kuona kwamba vipi tunaweza kupata maeneo mengine. Kwa mfano pale mkabala na Afrika House palikuwa kwanza ni kituo kidogo, lakini ni kituo kizuri sana kile cha ku-*establish* sehemu nyengine ya Forodhani. Pale penye sehemu ya uwazi baina ya Hoteli ya Tembo na Starehe *Club*, vile vile ni eneo zuri sana la kufanya pahala pa kupumzika. Tukiweza kutengeneza sehemu nyengine, nafikiri itapunguza ile *pressure* ya watu wote kuhamia Forodhani, *provide* wanapata huduma sawa sawa na kila mtu ataangalia urahisi wake wa kwenda.

Mhe. Spika, ningeomba suala hili likaangaliwa kwani mji mkongwe unaingia wageni wengi sana, ingawaje matatizo madogo madogo yapo lakini sio ya mji mkongwe ni ya usalama ambayo haya yatatungwa siku yake, siku ya masuala ya usalama.

Jengine Mhe. Spika, kuna ukuta wa jiwe ambao ulijengwa miaka mingi sana huu, umeanzia Forodhani mpaka umemalizikia Ikulu na umeachia hapo Kizingo. Ukuta ule Mhe. Spika, hapo zamani nasikia wazee wanavyozungumza kulikuwa na timu moja inapita na mawa na saruji inachapia kila panaponyofoka mwanzo mpaka mwisho, kwa hivyo baada ya miaka hakuna miporomoko wala mimong'onyoko ya sehemu za ardhi kuanguka chini. Lakini siku hizi kwa bahati mbaya suala hili limezoeleka sana, hizi sehemu zinabokolewa zinachukuliwa na ardhi inakwenda zake.

Alhamdulillah Forodhani pamejengwa na pametengenezwa ambapo palikuwa panakabiliwa na suala hilo hilo, lakini Alhamdulillah pametengenezwa. Lakini

kuanzia Forodhani kwenda mpaka Maquree pale bado mmong'onyoko upo na hali ni ya hatari. Ukitoka huku sehemu za Afrika House huku kote kumemong'onyoka mong'onyoka na wageni wote wanaosafiri kwenda katika visiwa ndio bandari yao ya kushukia pale. Kwa hivyo, sehemu hizi mji mkongwe waziangalie kama kutafuta wafadhili au kama kutengeneza wenyewe, lakini hali inatisha huwenda yote ikachukuliwa.

Mhe. Spika, majengo yote yaliokuwepo pwani. Kwa mfano Skuli ya Tumekuja, pale kuna jengo sijui la JKU lile, kuna jengo la Wizara ya Mipango mpaka kuendea Ikulu. Majengo haya vile vile kila siku yanagongwa na maji, lakini majengo yale yako katika hali mbaya, hakuna matengenezo yanayofanywa katika sehemu zile pale, kuna hatari siku yoyote yakamong'onyoka na yakaanguka na tukaanza kuutoa shepu mji wetu.

Vile vile suaja jengine ninaloliomba kwa mamlaka hii kuona kwamba katika mamlaka hii kuna majengo ambayo kwamba hayakutaifishwa na serikali, sijui ilikuwakuaje tu yakabadikwa tu msajili wa majumba watu wakakodishwa, wakahamia, yanavunjika nusu na wamiliki wapo wenyewe nchini hawajaondoka, uwezo wanao wa kuyatengeneza. Mimi nasema kwamba majengo ambayo hayana umiliki wa serikali, hayakutaifishwa na wenywe wapo, basi majengo yale warudishiwe wenyewe wapate kuyatengeneza. Kuliko kuwakodisha watu serikali inachukua kodi, majengo hayatengenezwi yanaporomoka nusu nusu mpaka yatapotea kabisa.

Jengine Mhe. Spika, ninaloliomba ni kwamba zamani tulikuwa na utamaduni kwa sababu ilikuwa nafikiri majengo yote ya mji mkongwe au mengi yakipakwa chokaa, siku hizi watu wanapaka *ant fungus paint* ambayo ni ghali sana. Rangi nyengine ambayo inapakwa katika majumba haya angalau ni zile ambazo kuta zinavuta pumzi, kwa hivyo imekuwa ni kitu ghali sana. Lakini chokaa ukipaka katika ukuta wa mji mkongwe unapata kutoa jasho na unapata kutoa pumzi.

Mhe. Spika, siku hizi imekuwa na mila ile ya kupaka rangi za siku hizi katika majengo mengi na mji unazidi kuwa majengo hayapendezi. Kwa hivyo, ningeomba kwamba angalau kuwe na *funds* fulani za kuweza kutengeneza ile mitaa muhimu ambayo watalii wanapita. Mtaa wa Hurumzi utafikiri ule mji ni giza, kumbe sio giza, lakini majumba hayajapakwa rangi kwa muda wa miaka 50 sasa au 40, kwa hivyo ndio mji unauona giza kwa sababu hayajapakwa rangi. Kwa hivyo, ule utamaduni wa kupaka rangi katika mji mkongwe bado haupo kwa hivyo mji mkongwe ushajihishe suala la kupaka rangi na matengenezo madogo madogo.

Jengine Mhe. Spika, katika hoja hii imetiwa habari ya kutoa elimu na kutoa vitabu, makabrasha na mambo mengine. Lakini nasisitiza kwamba mji mkongwe Alhamdulillah wametoa mafunzo mengi sana kwa mafundi wetu. Tumepeleka mafundi wetu wamekwenda kufundishwa namna ya kupika chokaa, namna ya kupiga plasta, namna ya ku-*reserve* zile *arch* na mambo mengine.

Kwa hivyo, ningeomba katika suala hili mji mkongwe watenge fedha maalum za masuala haya ya kuendeleza. Kwa sababu mwanzo ilianza vizuri, lakini siku hizi wameacha nafikiri kulikuwa kuna wafadhili na sasa hivi hakuna. Lakini ni suala muhimu sana na nafikiri wangelifanyia kila utaratibu kwamba mafunzo ya mafundi waashi, mafundi seremala na mafundi wote ambao wanafanya kazi za mikono za mji mkongwe wapewe mafunzo ya mara kwa mara ili mafundi wetu waweze kuwa na ujuzi zaidi.

Mhe. Spika, baada ya michango yangu hiyo naomba niunge mkono hoja hii mia fil mia na kuwapongeza wote walioshughulika na hoja hii, ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nafikiri tumefarijika na mchango huu, mimi nilikuwa sijajua katika maisha yangu kwamba kuta kumbe huwa zinavuta pumzi na kutoa jasho. Lakini kwa manufaa ya kuwa na mkandarasi kama huyu nafikiri hiyo ndio faida yake moja kubwa sana tumeipata. Pia kumbe hizi rangi zina namna yake na ufundi wake. Tunakushukuru sana Mhe. Mazrui.

Sasa tutaendelea na michango jioni kwa kuwasikiliza Mhe. Najma Khalfan Juma, Mhe. Said Ali Mbarouk, Mhe. Zakiya Omar Juma, Mhe. Samia Suluhu Hassan, Mhe. Haji Mkema Haji na kumalizia na Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni leo)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kama tulivyokubaliana wakati wa kipindi cha asubuhi kwamba wakati tutakapoingia tutaanza na Mhe. Najma Khalfan Juma ambaye namkaribisha sana na baadaye Mhe. Said Ali Mbarouk.

Mhe. Najma Khalfan Juma: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo nami kuchangia machache juu ya mswada huu unaohusiana na mambo ya Mji Mkongwe.

Mchango sitokwenda kifungu kwa kifungu isipokuwa nitazungumzia kijumla jumla.

Mimi binafsi nimelelewa Mji Mkongwe tokea mtoto mpaka nimekua, nimeolewa, nimezaa na mpaka najukuu hivi sasa ndani ya Mji huu. Kwa hivyo, mimi ni mwana wa Mji Mkongwe.

Kwa kweli Mji huu hivi sasa umo kwenye Urithi wa Kimataifa, tena Mji huu Mhe. Spika fedha zimo, yaani unaingiza fedha sana. Kwasababu ni Mji ambao watalii wengi wanakuja katika Mji huu kwa ajili ya kuutembelea, pia tunazo hoteli nyingi sana kwenye Mji huu. Kwa hivyo, Mji huu unaingiza fedha, yaani mapato yanaingia.

Lakini umekuwa uchumi mndu, yaani ni mkongwe na Wapemba wanasema uchumi mndu na kwa Waunguja panga. Kwa mfano, unapotaka kulima basi utakwenda kulichukua na kukatia masiki na vitu vyengine na halafu utauweka kipembeni kwenye mlango, sasa wakati unapopita kwenye mlango na ule mndu ukakuparaza basi haufai tena. Kwa sababu kwenye shamba tayari umeshaandaa mazingira mazuri, lakini mndu unapokugusa tu, unasema unataka kunikata.

Kwa maana hiyo, Mji Mkongwe umekuwa uchumi mndu, kwani Mji unachuma fedha, lakini fedha hizi hazigaiwi hata kidogo kwa ajili ya kutengenezewa. Kwa mfano, utaona Nyumba za Mji Mkongwe hazing'ari, yaani hazitiwi hiyo chokaa, pia kuchafu au maji machafu kila siku yanatiririka utafikiri kuna mto wa mafuta na hasa ukipita mitaa ya Hurumzi, yaani kila siku huna siku unayopita usikutane na maji machafu.

Kwa kweli kila siku unapopita mtaa wa Hurumzi basi ukunje nguo kama Balkis ameona Nyumba ya Nabii Suleiman wakati huo, kutokana na maji machafu ya karo yanayotiririka kwenye mtaa huo. Kwa ujumla Mji wote hauko katika hali nzuri na Mji huu unajichumia.

Kwa hivyo, naiomba serikali Mhe. Spika kupitia kwako, kwa sababu Mji huu unajichumia wenyewe basi nao utengewe kwenye zile fedha kama zitatiwe kwa hawa wanaoshughulika na Mji Mkongwe, kama walivyosema wenzangu Manispaa hawajiwezi kwenye mitaa mingine na kwa upande wa kuusafisha Mji Mkongwe nadhani kazi kubwa sana. Nadhani hawa waweze kununua vifaa na kufanya mambo mengine, lakini wakaweza kuuweka Mji Mkongwe katika hali ya usafi.

Vile vile fukwe zilizomo Mji Mkongwe zinahitaji nazo ziwe katika hali ya usafi. Kwa mfano, wale wenye mazoea ya kutupa vitu vichafu katika fukwe za Mji Mkongwe basi ziweze kusafishwa. Pia kuhusu ukarabati wa majengo

uwepo katika Mji Mkongwe, kwa sisi tunaokaa kwenye zile nyumba au za serikali na tunalipa kodi, basi wanaohusika na Mji huu basi wayatengeneze majengo haya, kwa sababu tunawalipa kodi, lakini hawatutengenezei mpaka mtu atengeneze mwenyewe.

Mhe. Spika, kwa upande wa watu wanaofanyakazi katika Mji Mkongwe, yaani wale wanaoshughulikia wanahitaji elimu ya kutosha, kwa sababu huu ni Mji ambao unatakiwa uchukuliwe kama yai au mtoto mchanga ulelewe, ili upate kukua vizuri kwa lengo la kubakia na uendelee kurithiwa na vizazi vyetu vitakavyokuja baadaye.

Kwa hivyo, nashauri kwamba wale watendakazi kama hawa elimu ya kutosha basi wapelekwe sehemu mbali mbali ambazo zina mji kama yetu, kwa ajili ya kupata elimu ya kuutunza Mji Mkongwe nao waweze kuutunza Mji huu *(Makofi)*.

Mhe. Haji Faki Shaali alisema kwamba gari nzito zinapita katika mitaa ya Mji Mkongwe, jambo hili ni kweli kwa sababu mimi ni mkaazi na kwa bahati nzuri naona zile gari zinavyopita. Kwa mfano, ukitembelea sehemu nyingi za Mji Mkongwe ambazo ziko njiani hasa pale kwangu karibu na Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora, basi utaona nyumba nyengine zimefanya nyufa kwa kupitiwa na gari kubwa ambazo ni nzito.

Mhe. Spika, kwa bahati mbaya gari hizi hazipiti mchana zinapita usiku na mizogo mikubwa ambayo ni mizito, yaani utahisi hasa kama uko ndani kwamba nyumba yote inatikisika.

Kwa hivyo, tunaiomba wizara inayohusika kupitia kwako Mhe. Spika, wazungumze na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, ili kuhakikisha kwamba gari kubwa ambazo ni nzito hazipiti kwenye Mji Mkongwe na kusababisha athari kwa nyumba zilizo karibu na barabara.

Mhe. Spika, haiba ya Mji Mkongwe inaanza kupotea, kwa sababu tumeambiwa kwamba Mji huu unao utamaduni wake, silka pamoja na mambo yake mengi. Lakini kama walivyosema wenzangu kwa sababu na mimi nilikiweka kipengele hiki nikizungumze.
Kwa kuwa Mji Mkongwe tokea utakapoingia mwanzo hasa mitaa ya Hurumzi, Gizenga *Street* yote mpaka juu, basi ni vinyago tu. Sasa hata huo utamaduni wa Mzanzibari hauonekani, yaani ni vinyago kwenda mbele, angalau wangekuwa wanaweka mashua, matundu ya ndege, makawa, mikopa pamoja na kazi nyengine za Zanzibar vikiwemo viatu vya makubadhi na mambo mengine ambayo yangeleta haiba na kuonesha kwamba huu Mji Mkongwe uko Zanzibar *(Makofi)*.

Lakini leo ukiingia Mji Mkongwe sehemu ya Hurumzi, Gizenga *Street* yote utadhani uko Kilimanjaro, michoro ya tingatinga, badala ya kuona samaki au ndege wakiruka unaona ndovu, simba, twiga na mambo kama hayo. Vile vile huoni akinamama wamesuka nywele zao au wamevaa mtandio ama baibui, isipokuwa utaona Wamasai wanaruka.

Sasa kutokana na hali hii utamaduni wa Mzanzibari unahifadhi vipi katika huu Mji Mkongwe, wakati Mji huu unayo historia, mila pamoja na utamaduni wake, ambapo kwa pamoja ndizo zinazofanya huo ustaarabu wa Zanzibar kwa pamoja.

Mhe. Spika, pia Mji Mkongwe huu kwa sababu umo kwenye utalii, yaani Mji huu hauwezi kwenda peke yake bila ya kushirikiana na wizara nyengine. Kwa hivyo, umo kwenye masuala ya utalii, lakini watembezaji watalii pengine wengi wao si Wazanzibari, basi utaona wanatoa *history* ambayo si ya kweli.

Kwa hiyo, nawaomba watu wa Mji Mkongwe wafanye utafiti katika nyumba mbali mbali ambazo zilikuwa zikitumika kama historia, basi waeke ile historia angalau kuonekana. Kwa mfano, wageni wanapokwenda pale wasipate tabu, yaani mtu akifika anasoma tu kama ilivyofanywa Tip Tip *House*, kuweza kufahamu kwamba nyumba hii historia yake iko hivi.

Lakini hawa wanaotembeza watalii wengine si watu wa hapa na wala hawatoi historia ya ukweli ya ule Mji Mkongwe, kwa hivyo wanapoteza ile *history* yote ya Zanzibar. Kwa sababu historia kubwa ya Zanzibar iko kwenye Mji Mkongwe.

Kwa hivyo, nadhani ni vyema kufanya utafiti na kule Idara ya Nyaraka ziko bila ya shaka yako maandiko mbali mbali, basi watu waache kazi na kwenda kufanya utafiti na kujua hasa historia vizuri. Kwa mfano, Nyumba ya Mambo Msiige ilikuwaje ikaitwa vile pamoja na historia yake inabandikwa na nyumba nyengine nyingi.

Nafikisi si busara kuwaachia watu kupita katika Mji Mkongwe na kutoa elimu ambayo si sahihi, kwa kweli wanatuharibia historia ya Mji Mkongwe na ile ya Zanzibar kwa ujumla.

Vile vile vipindi vya redio vinahitajika sana tena redio zote sio Sauti ya Tanzania Zanzibar peke yake, yaani vipindi vya redio, televisheni na magazeti. Kwa kweli kuna haja ya kufanya vipindi hivi, kwa ajili ya kuitangaza Zanzibar kupitia Mji Mkongwe na watu wakaona.

Kwa mfano, kuna kipindi kwenye televisheni *TBC_1* ambacho kinaitwa Zamadam, lakini ukitizama ndani ya kipindi hicho utachefukwa na moyo. Kwa sababu wanaweza kuelezea ukanda wa pwani mpaka wa kiingia Zanzibar waiunganishe basi pale wanaikata au itakuwa historia ambayo si sahihi itakuwa inaelezwa.

Kwa hivyo, umefika wakati kwa watu wanaohusika na Mji Mkongwe kama zamani walikuwa na vipindi basi na hivi sasa wafanye vipindi kweli, ambavyo vitakuwa na utafiti mkubwa zaidi kuhusiana na Mji Mkongwe pamoja na historia ya Zanzibar kwa jumla. Kwa sababu Mji Mkongwe huu wa Zanzibar, lakini unavyo vitoto vyake huko mashamba ambavyo vimetokana na Mji huu *(Makofi)*.

Mhe. Spika, leo utaona mambo ya Zanzibar kupitia televisheni nyengine, kusema kweli hali hii inauma. Kwa maana hiyo, tunataka kuona mambo ya Zanzibar kupitia hata kama kwenye televisheni nyengine, lakini viwe vimefanya hapa Zanzibar tena na Wazanzibari wenyewe na watu wenyekuhusika na Mji Mkongwe au wazee wanaojua historia ya Mji huu na kueleza vizuri, kwa ajili ya kuvijuza vizazi mambo ya Mji huu pamoja na vitoto vyake vilivyokuwepo.

Kwa sababu Mji Mkongwe ni mji unaotembelewa na watalii, barabara za ndani nyingi zimechafuka. Kwa mfano, ziko zile ambazo zimetiwa *tiles* lakini bado nyengine hazijatiwa *tiles*. Kwa hivyo, tunaomba na hizi barabara nazo, kwa sababu Mji huu unajichumia wenyewe basi barabara zitengenezwe, ili barabara hizi zisituwame maji wakati wa mvua. Kwa maana hiyo, watalii wanapopita wasipate kero kwa kuwa wao tunawategemea kwa ajili ya kutupatia fedha za kigeni.

Vile vile naiomba wizara hii kupitia kwako Mhe. Spika, najua kwamba kuna Siku ya Utamaduni wa Mzanzibari, kwa sababu tunataka kuukuza na kuutangaza Mji Mkongwe katika dunia, basi kuwe na Siku ya Mji Mkongwe. Siku hii utatangazwa utamaduni wa Mji Mkongwe ambao ndio ule wa Mzanzibari, lakini itakuwa *special* kwa Mji Mkongwe tu, yaani ndiyo yale ya Mzanzibari isipokuwa tutayahamisha na kusema haya ya Mji Mkongwe, kwa kuwa tunatafuta fedha ambako kuna njia nyingi.

Kwa mfano, mavazi, mapishi, kazi, elimu iliyokuwa ikitolewa wakati huo na tunaweza kurudi Ukutani na wala hakuna tatizo, kwa ajili ya kutafuta historia ilivyokuwa na watu kuelezea kwa sababu zipo zimeandikwa, basi ikawa japo siku moja au mbili na ikawa *Festival* ya Mji Mkongwe. Kwa kweli jambo hili linaweza kutupatia fedha kwa kuwa watalii wataingia na wala hatuwafanyii bure, taarab zitapigwa na watu watakuja wataalikwa.

Kwa hivyo, fedha zitapatikana na lile jina la Mji Mkongwe tutalikuza, yaani tutakuwa na siku maalum ya Mji Mkongwe, tunaweza kualika wenzetu kutoka Mji Mikongwe mingine na kuja hapa, kwa ajili ya kuona mambo yetu pamoja na Zanzibar kwa jumla ilivyo. Kwa maana hiyo, hapa tunaweza kuutangaza Mji wetu Mkongwe pamoja na Zanzibar kwa jumla.

Mhe. Spika, nadhani tunaweza kuomba fedha kutoka *UNICEF* kama sisi wenyewe hatuwezi, vile vile watu wanaohusika na Mji Mkongwe kwa kushirikiana na watu wa utalii basi wanaweza kulifanya suala hili, yaani Siku ya Mji Mkongwe. Kwa sababu Mji Mkongwe unatoka Mnazimmoja mpaka unaishia Malindi kwenye Ras-el-Khaima, lakini bahari inatumaliza. Kwa mfano, kule Ras-el-Khaima bahari inaingia Malindi kwa nguvu. Kwa hivyo, watu wanaohusika na Mji Mkongwe wafanye kila njia, ili wairudishe bahari nyuma kidogo, kwa sababu Mji Mkongwe wenyewe wote wa kujaza taka tu, yaani kilikuwa kisiwa na hivi sasa *alhaldulillah* Darajani na Vikokotoni kumeunga pamoja.

Sasa tusiiache bahari na maji siku moja yakaja kupanda Funguni kwa Wachina Tambi. Mhe. Spika, mimi wakati wa utoto wangu nilikuwa nikikaa nyuma ya *National Bank of Commerce* na bahari ilikuwa chini kabisa, lakini leo bahari iko barabarani.

Kwa hivyo, tufanye kila linalowezekana bahari tuirejeshe nyuma. Kwa kweli ni fedha nyingi lakini tutakuwa na miradi na huu ni mradi. Nadhani ni vyema tutengeneze mradi na tuandike *paper* na kupeleka nje na kuonesha hali halisi ilivyo na jinsi bahari inavyokula kisiwa chetu watusaidie kitaalamu pamoja na kifedha, kwa ajili ya kutusaidia kuisukuma bahari nyuma kidogo kwa lengo la kuhifadhi huu ukanda wa Mji Mkongwe kwa ujumla tuhifadhi na kisiwa chetu kisiliwe na maji kama hivi.

Mhe. Spika, watu wanaokaa kwenye mitaa wa Ras-el-Khaima, Malindi na Funguni pamoja na Forodhani pia wasaidiwe kama vile kuta zinazomong'onyoka. Kwa mfano, siku nyengine mawimbi yanayopuwa makubwa yatakuja mpaka juu yatufunike.

Kwa hiyo, tusaidiwe katika kuutunza huu Mji Mkongwe, ili usiliwe na maji na hii mitaa ambayo tayari iko ndani ya maji hasa Malindi kule, basi na wao tuandike *paper* na kuangalia hali ilivyo na kuomba misaada kutoka nje, ili watusaidie wenzetu kwa ajili ya kuhifadhi huu Mji Mkongwe.

Mhe. Spika, Mji Mkongwe unavyo vitoto vyake, yaani hii miji mingine midogo midogo ambayo ni mikongwe nayo tutaifanya vipi. Kwa mfano, kuna mambo

mengine makongwe makongwe nayo, ambayo pengine yaliungana na Mji Mkongwe hapo zamani tutayafanya vipi, kama vile Maruhubi.

Kwa sababu Maruhubi iliungana na Mji Mkongwe wanapotoka wenzetu jioni wanapokwenda kustarehe, yaani ni *part of Stone Town* tutaifanya vipi nayo, ili tuitie kwamba hii nayo ni sehemu ya Mji Mkongwe, kwani watu waliokuwa wakiishi wakati huo wakitumia nyumba za mashamba au zile zilizomo fukweni kwa ajili ya kupumzika ambazo ni za miaka mingi, sasa tunafanya vipi. Mhe. Spika, tunahifadhi huu mzunguko wa Mji Mkongwe tu au na zile tutazitia, ili tuweze kuzipatia misaada kwa ajili ya kuzihifadhi na kuzitengeneza *(Makofi)*.

Mhe. Spika, nilisema kwamba sina mchango mkubwa sana. Isipokuwa la mwisho ni kuhusu nyumba nyingi za Mji Mkongwe ni mbovu. Kwa hivyo, naiomba wizara inayohusika kupitia kwako Mhe. Spika, ikiwa hizi nyumba zinazo wenyewe basi waambiwe wazitengeneze, vile viwanja ambazo nyumba zimebomoka na sasa vinaota magugu na siku moja nyoka wanaweza kufanya makaazi pamoja na chatu, yaani Mji Mkongwe na chatu.

Kutokana na hali hii kama wapo watu wenye uwezo wa kivinunua basi wauziwe na kujenga katika *style* ile ile ingawa watajenga kwa kutumia vifaa vya kisasa, lakini *style* ya Mji Mkongwe madirisha madogo hata kama atatia kumi, milango iliyochongwa vizuri na hivi na vile ingawa usasa utakuwemo. Lakini jambo la msingi la kuzingatia ni ile mandhari ya nje ionekane kwamba huu ni Mji Mkongwe na wala haikuharibiwa ile *structure* ya Mji wenyewe, kuliko kuviacha vile viwanja na kuota magugu na kugeuza majaa.

Hivi sasa kwa bahati mbaya Mzanzibari ameacha utamaduni wake wa kufyagia uwanja asubuhi, kwa hivyo taka wakati wa asubuhi ukipita njia zimejaa ambazo zimeangushwa na paka usiku. Kwa kweli husikitika sana kwa sababu wakati mwengine mdomo wangu siuwezi, basi nikipita chini ya nyumba ya mtu kama kuna taka namwambia hata hizi huwezi kuzoa na kutia kwenye debe, ili mchukuzi wa taka anapokuja kuchukua na kuondoka mbona tunauacha utamaduni wetu.

Mhe. Spika, utamaduni wa Mzanzibari ni kuamka asubuhi kufyagia ndani na nje hiyo ni lazima. Lakini sasa vijana wa leo wanatupa ile silka, yaani imekuwa mji wote mchafu wanasubiri Manispaa waje wafyagie ndio kazi yao, lakini hata chini ya kizingiti chako.

Kwa hivyo, nadhani watu wa Mji Mkongwe kama watakabidhiwa wenyewe kusafisha mji wao, vile vile wawambie na kuwe na sheria maalum za kuwaambia wakaazi wa Mji Mkongwe lazima kila mtu asafishe sehemu yake anayokaa. Kwa mfano, wauza maduka wenzangu utakuta makaa yametupwa

kwenye tiles, anauza duka basi ametupa makaa, mafuta ya taa, nazi, almuradi huo uchafu hata pakupita hupajui, basi inyeshe mvua ndio kabisa hapapitiki.

Kwa hivyo, naomba ikiwa Manispaa tunahisi hawawezi kusafisha Mji Mkongwe, basi iundwe timu kupitia wenyewe watu wa Mji Mkongwe, yaani hao wanaoshughulika na Mji Mkongwe na kuteua vijana wao ambao watakuwa wakisafisha Mji Mkongwe na wakaazi wa Mji wawalipe na wala sio kusafishiwa bure walipe.

Kwa sababu tunataka usafi na sisi wenyewe maami, kama tunavyojua dasturi za watu wa Mji Mkongwe saa 2 hawajaamka, basi walipe kwa ajili ya kusafishiwa mitaa yao *(Makofi)*.

Mhe. Spika, watu wa Mji Mkongwe wenyewe wakipewa watajua namna gani ya kufanya kwa sababu wao wenyewe wanajuana na watajua namna gani wafanye, ili mji wao uwe safi na kuepukana na uchafu.

Vile vile naungana na wenzangu na ninawapa pongezi wale waliotoa wazo la kutengeneza ile Bustani ya Forodhani. Kwa kweli ni kivutio kizuri ingawa wengine humu ndani ya Baraza walikuwa wakikataa kidogo na kuwa na mashaka. Lakini matokeo yake tumeona leo Forodhani palivyo na pia tunaona jinsi palivyo safi.

Mhe. Spika, pia naomba na Mji Mkongwe kwa sababu Bustani ya Jamhuri nalo ni eneo lao nayo waitengeneze kwa sababu ni Chuo Kikuu cha Skuli zote za walioko sekondari na vyuo wote wanakaa kwa ajili ya kujisomea hasa karibu na mitihani, basi utaona makundi ya wanafunzi.

Kwa hivyo, na wao watengenezewe, ili pale pahala pazidi kuvutia na kuwa pazuri na wale wanafunzi wanapokuwa pale wazidi kutafakari vizuri masomo yao. Kwa upande wa wale wanaokwenda kupumzika basi wapate pahala pazuri pa kupumzika.

Vile vile Mji Mkongwe ubuni sehemu nyengine kama walivyosema wenzangu. kwa mfano, Forodhani ilipohama kwa muda ilihamia mkabala na *Africa House*, yaani palikuwa pazuri tena pakivutia. Kwa maana hiyo, kama inawezekana kwa sababu kule kunajaa sana hasa siku za sikukuu, basi na pale patengenezwe na wengine watakuwa wakiuza biashara pale, mtu atakwenda pale ambapo karibu yake.

Mhe. Spika, sehemu nyengine zote za bustani za Mji Mkongwe zitengenezwe, ili tuweze kuweka mandhari ya Mji Mkongwe iwe nzuri na iwe kuvutio kizuri kwa sisi wenyewe tunaokaa kwa sababu macho yanapenda kuona kitu kizuri na

wageni watakaokuja, kwa ajili ya kuitangaza Zanzibar katika jina zuri.
Ahsante sana Mhe. Spika na naunga mkono hoja kwa asilimia mia mbili *(Kicheko/Makofi).*

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia machache katika mswada huu wa Mamlaka ya Hifadhi wa Mji Mkongwe.

Mhe. Spika, mimi ni mwakilishi ambaye ninayetoka katika jimbo la shamba kidogo, sasa mambo haya ya Mji Mkongwe ndio kwanza najifunza. Kwa hivyo, madhumuni hasa ya huu mswada nimeshindwa kuyafahamu na nimejaribu kuusoma vizuri sana.

Lakini nimeshindwa kufahamu hasa yale ambayo yanapendekezwa katika mswada huu yatatuondoa vipi katika hali halisi ya Mji Mkongwe tuliyonayo, yaani ile hali halisi ya Mji Mkongwe ulivyo wakati tunapopita. Kwa hivyo, yataondoshwa vipi na marekebisho au uanzishwaji wa sheria hii mpya, kwa kweli hilo ni jambo ambalo linanipa matatizo kidogo.

Zaidi huwa ninajiuliza hivi tumefanya utafiti wa kutosha, kweli tunahitaji Hifadhi ya Mji Mkongwe sijui. Nadhani tungelifanya utafiti mkubwa na kuweza kuangalia faida na hasara ya kuwa na Mji Mkongwe. Mhe. Spika, nasikia wako wenzetu walikuwa na Mji Mkongwe nimeambiwa Muscat au wameona kuendelea na Mji Mkongwe basi wao si maslahi.

Sasa na sisi tufanye tathmini Mhe. Spika na kama ingefanywa ingekuwa ni vizuri Baraza likaambiwa kwamba faida ya kiuchumi, kihistoria pamoja na mambo mengine mbali mbali na halafu tukaraghabika kuona kwamba kwa tathmini iliyofanywa *ofcourse* tunahitaji. Lakini kwa namna ambavyo tunaletewa inaonekana kama tumeingia kwenye mkumbo Mji Mkongwe na sisi tunafuata, binafsi sijaona.

Mhe. Spika, hali halisi ilivyo na marekebisho haya ambayo yapo, basi sioni kwamba kuna tunayo njia nzuri ya baadaye. Nilisema nianze hapo kwa sababu Mji Mkongwe kama ulivyo unakabiliwa na matatizo mengi. Kwa mfano, wakati nikipita huwa naona nyumba nyingi zimeekewa miunda au miega.

Sasa sioni katika mswada huu kwa hali ilivyo tutaondoka vipi kutokana na hali halisi hii. Nadhani haya ni mambo ya kuyangalia na kuweza kuyafanyia utafiti na kuona je tunahitaji Mji Mkongwe wa aina ile, ili tuondokane na pale tunafanya nini, tunabadilisha sheria au mtazamo ama vipi.

Mhe. Spika, wapo wenzetu masikini sana kama sisi na wao wanayo Miji Mikongwe, lakini ukifika utapenda uone, mara moja nilitembelea nchi moja inayoitwa Yemen ya Kaskazini wanao Mji Mkongwe ambao wanauita Sanaa. Rafiki yangu aliniambia twende ukatembee Mji Mkongwe, basi nilimuuliza Mji Mkongwe, aliniambia naam, Mji Mkongwe wao unaitwa Babu-ll-Yamani.

Ukikaa huku Sanaa kwenyewe na ukienda mule Babu-ll-Yamani utadhani uko nchi tofauti, kwa sababu wale wame-*conserve* Mji Mkongwe hakika. Kwa kweli usafi wake au mazingira yake ni ya ajabu, nyumba zilivyohifadhiwa ni ajabu kabisa.

Lakini sisi Mji Mkongwe nyumba nyingi zina miega na huo ni mtihani tutauana, ikiwa tunahifadhi mpaka nyumba zile naona si sahihi. Mhe. Spika, ikiwa tumeshindwa bora tuseme hatuwezi kuendelea na utaratibu ule. Kwa sababu kila mwaka kuna nyumba zinaekewa miega, kwa sababu nyumba hazitengenezwi, basi itakuwa ni mji ambao unahifadhiwa kwa miega hatuwezi *(Makofi)*.

Mhe. Spika, tunahitaji lazima tuwe makini na kwa kweli tupangilie vizuri mambo yetu.

Ushauri wangu ni kwamba Mamlaka ambayo inayoundiwa sheria basi iwe ni mamlaka kweli na wala isiwe nusu mamlaka na nusu mambo mengine. Kwa kweli tunahitaji Mamlaka ambayo yenye uwezo wa kufanya shughuli zote, kama vile masuala ya ujenzi, ukarabati, uuzwaji, kuingia ubia na mwenyewe, kumtafutia ubia mwenye jengo.

Lakini suala kubwa ambalo hata wenzangu wamelizungumzia kuhusiana na taka. Utaratibu wa taka lazima liwe ndani ya mamlaka yenyewe na wala hatuwezi kuwa na mamlaka halafu shughuli nyengine tunategemea mamlaka nyengine, hiyo itakuwa ni mchezo. Kwa sababu mamlaka yenyewe inazo kazi nyingi na wala hakuna jambo linaloweza kupatikana.

Mhe. Spika, jambo jengine katika mswada huu ambalo nimeliangalia ni kuhusu mpangilio wa vifungu vyake haukunifurahisha sana. Kawaida wizara hii inao utaratibu mzuri wa kuleta miswada Barazani, lakini labda Afisi ya Mwanasheria Mkuu imewaangusha mara hii.

Kwa kweli kuna vifungu ambavyo mwenzangu asubuhi amevitaja Mhe. Haji Faki Shaali kifungu 4 kinachozungumzia Mamlaka ambacho kina (a), (b), (c), (d) na (f), halafu hapo kuna kifungu chengine 6 kimeruka baada ya kifungu kile cha Majukumu ya Mamlaka mpaka f, kifungu 5 Hifadhi ya Kisheria ya Mamlaka. (6) imejirudia majukumu ya mamlaka tena kwa hivyo huu sio

utaratibu mzuri wa *drafting* ya mswada. Pia kuna kifungu ambacho kinazungumzia kuanzishwa kwa muundo wa Bodi ya Mamlaka kifungu cha 11 (a), (b) na (c) halafu kimekuja kifungu cha 12 kuhusu uwezo wa bodi, kifungu cha 13 kuvuliwa ujumbe, kifungu cha 14 imerudia tena muundo wa bodi. Mhe. Spika, nahisi kwamba kifungu hiki kingeliingia katika kifungu kile cha 11 ambacho kuna masuala yanayozungumzia Wajumbe wa Bodi na namna ambavyo wanaweza kupatikana na mambo mengine. Kwa hivyo, naona kidogo mara hii mambo hayakuwa vile ambavyo kawaida miswada ya wizara hii inakuwa iwe.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 13 © naomba ufafanuzi kidogo mjumbe atakuwa mkosa kwa tabia mbaya au kwa ukosefu wa nidhamu. Ujue kwamba suala la ukosefu wa nidhamu lina tafsiri kwa mujibu wa mtu, wakati mwengine ukivuta sigara anakutafsiri wewe huna nidhamu, kuna wengine ukilewa tembo anakuona huna nidhamu, kuna wengine ukifanya mambo ya ajabu anakuona wewe huna nidhamu. Kwa hivyo, tafsiri ya ukosefu wa nidhamu inatakiwa iwekwe vizuri usije ukampa mtu namna ya kutafsiri kama ambavyo anataka mwenyewe.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 16 bodi itateuwa mwanasheria kuwa Katibu wa Bodi. Mimi hapa ningeshauri kwamba kifungu hiki kijengwe kwa lugha ambayo ni nzuri, kwamba kutakuwa na mwanasheria wa mamlaka ambaye awe ndiye Katibu wa Bodi. Lakini hivi ambavyo kimewekwa kama walivyosema wenzangu ni kwamba bodi itateuwa mwanasheria kuwa Katibu wa Bodi. Kwa hivyo, inawezekana kwamba huyu asiye mfanyakazi wa bodi, lakini akawa mtu mwengine nje isipokuwa ameteuliwa kuwa Katibu wa Bodi. Kwa hivyo, mimi ningeshauri kwamba huyu mwanasheria awe ni Mwanasheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Mji Mkongwe ambaye yeye pamoja na kazi nyengine lakini pia awe ndiye Katibu wa Bodi hii.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo na mimi sijalifahamu ni kifungu cha 26 (a) endapo mamlaka itakuwa na mawazo kuwa kuna jambo lolote linafanywa kinyume na ilivyoelekezwa kwenye notisi iliyotolewa kwa mujibu wa kifungu wa kifungu cha 27 (1) au kifungu chengine chochote cha sheria hii. Nilipoangalia kifungu cha 27 hakizungumzii mambo hayo, halafu kuna 27 tu ambayo inazungumzia uwezo wa kufanya mapitio. Kwa hivyo, lugha ya kifungu hiki cha 26 (a) na 27 inatofautiana sana. Kwa hivyo, hapo kidogo naomba nipate ufafanuzi juu ya namna ambavyo Mhe. Waziri alikusudia.

Mhe. Spika, kifungu chengine ambacho naomba nifahamishwe zaidi ni kifungu cha 33 naomba kunukuu.

> “Endapo waziri ataridhika kuwa jengo ndani ya eneo la hifadhi lipo kwenye hatari ya kuanguka na haitawezekana kwa mmiliki wa jumba kulirudisha jengo hilo kwa matumizi ya binadamu”.

Mhe. Spika, ikiwa ni hivyo basi inaelekezwa katika vifungu vinavyofuata kwamba iwezekane jengo hili liweze kuhodhiwa, *notice* ya kuhodhi itaanza kutumika siku 90 baada ya kutolewa *notice* hiyo kwa mmiliki. Mhe. Spika, mimi ningeomba sana kwa Mhe. Waziri kwamba watu wetu wana matatizo mengi ya kiuchumi na hakuna mtu ambaye anataka kwamba nyumba yake ianguke. Lakini kwa hali halisi za watu wetu hufika pahala ikabidi ama ahame au auze. Sasa katika hali hii tukisema kwamba majengo yote ambayo mwenyewe ameshindwa kuyatengeneza tuyahodhi itafika wakati majengo mingi ya Mji Mkongwe wenyewe wa asili yatakuwa yamewashinda.

Mhe. Spika, mimi ushauri wangu kwa serikali kwa sababu watu wetu tunawapenda sana na lengo letu ni kuwainua kiuchumi. Kwa hivyo, wizara pamoja na mamlaka ingefanya utaratibu kwamba majengo ambayo yako katika hali mbaya na yale ambayo yanaonekana kuwa yanaweza yakasababisha hatari ya maisha ya watu. Majengo haya yasihodhiwe na serikali badala yake serikali na mamlaka itafute namna ya kumsaidia mwananchi kumtafutia ubiya baina yake na mamlaka ili ikatengenezwa nyumba halafu wakaangalia namna ya kurudisha kidogo kidogo gharama za na ikishakuwa nzuri akarejeshewa mwenyewe.

Kama serikali haina uwezo basi kutafutwe mwekezaji ambaye naye ataingia ubiya yeye na mwananchi. Hivi ndio namna ya kuwasaidia wananchi wetu, lakini hatuwezi kuona kama nyumba ya mwananchi imeshaanza kumshinda tukasema tuichukue, kwa kweli hii itakuwa hatuwasaidii watu itakuwa tunawasuru mtu nyumba imeshamshinda tunaichukua. Mhe. Spika, hilo silo lengo, lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuona kwamba maisha ya watu wake yanaimarika. Namna ya kuimarika ni hivyo ama serikali, mamlaka na mwenye mali waingie ubiya ili watengeneze halafu kidogo kidogo serikali imkabidhi mwenyewe, au itafute mwekezaji ambaye yuko tayari kuja kuekeza katika jengo lile kwa makubaliano yao halafu wakishakuwa tayari watakubaliana.

Mhe. Spika, tukiwa hivi kwa kweli wananchi wetu tutawasaidia na kuna nchi nyingi zinafanya hivi tunajaribu kuwatafutia wawekezaji na serikali yenyewe inaingia na wananchi kwa ubiya ili kuona kwamba serikali inapata na mwananchi na yeye anapata faida.

Mhe. Spika, naomba nipate ufafanuzi katika kifungu cha 45 (1) na (2) naomba ninukuu.

"Mamlaka itahifadhi kwenye akaunti maalum fedha zote za ziada ndani ya siku 90 baada ya kila mwisho wa mwaka wa fedha.

Fedha za ziada zitatumika kwenye bajeti ya mwaka ujao wa fedha na kwa namna yeyote hazitotumika kama bajeti ya ziada".

Mhe. Spika, hapa naomba ufafanuzi wa namna ambavyo akaunti maalum ya mamlaka hii itakuwa. Nasema hivi kwa sababu uzoefu umeonesha kwamba kuna baadhi ya taasisi ikishapitishwa sheria kama hii wao hufikiria kwamba tayari wameshapata mamlaka ya ufunguaji zile zinaoitwa *special account*. Kwa kweli hii husababisha matatizo makubwa baina ya wakaguzi wa hesabu za serikali na tasisi husika na hufikia pahali wakalazimishwa kuzifunga *account* hizo. Mimi katika hili naomba ufafanuzi lakini pia ningeshauri sana kwamba wakati tunalizungumzia suala hili basi tujaribu sana kujielekeza kuangalia kwamba sheria ya fedha ya serikali ya mwaka 2005 inazingatiwa sana, tusije tukafika pahala tukapata matatizo kama ambavyo taasisi zimepata.

Mhe. Spika, kwa kweli mimi sikuwa na mchango mkubwa ila nilitaka nizungumze hayo na zaidi katika kifungu cha 27 (2) nataka nimpongeze Mhe. Waziri kwa kukiweka kifungu hiki ambacho kinazungumzia umuhimu wa bodi wa kuweka utaratibu mzuri wa ukaguzi wa ndani wa fedha na Mkurugenzi Mkuu kuwa na dhamana ya utaratibu uliowekwa unafuatwa na wahusika wote. Mhe. Spika, hili jambo zuri na muhimu sana kwa sababu taasisi nyingi za serikali zina utaratibu mbovu wa *internal control* ya fedha. Kwa hivyo, nilipoona Mhe. Waziri amekiweka kifungu hiki cha 47 (2) na (3) kwa kweli nimpongeze na anaonekana kwamba yuko makini kuona udhibiti wa fedha za ndani unawekewa *security* sana.

Mhe. Spika, kama nilivyoanza kwa kusema kwamba ikiwa tunahitaji Hifadhi ya Mji Mkongwe wa Zanzibar basi tunahitaji kuona kwamba tunajifunza kutoka kwa wengine kama tunaohitaji *analysis* yetu inaonesha kama tunahitaji basi tuwe makini kuona kwamba tunaohitaji kweli. Kama hatuhitaji basi tuondoe tufanye mambo ambayo wenzetu wanafanya. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kwa kunipa nafasi ya kutia baraka zangu katika mswada huu. Mhe. Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati kwa hiyo tulipata wasaa wa kutosha kwa sababu siku ambayo tulifanya hii kazi tulifika mpaka saa 11. Kwa hivyo, tulifanya kazi moja kubwa sana. Pia nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mhe. Waziri na watendaji wake kwa jukumu ambalo tuliwaachia kwenda kufanya marekebisho katika mswada huu kama tunavyoyaona.

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema nimeona na mimi nitie baraka zangu lakini niligundua kuna kasoro ndogo pengine sote tulipitikiwa tukawa hatukuiona na bado hata kwenye marekebisho pia haimo. Kwa hivyo, ningeomba nianze na hapo katika ufafanuzi kifungu cha 2 kuna tafsiri ya neno mamlaka na inasomeka kama mamlaka maana yake ni mamlaka ya hifadhi ya uendelezaji wa Mji Mkongwe iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4, hapo ndipo alipokosea. Mhe. Spika, kwa mujibu wa huu mswada ni kifungu cha 3 na sio cha 4 kidogo imetupitikia na ndio mambo ya kibinadamu. Kwa hivyo, ningeomba hapo tufanye marekebisho kwamba ni kifungu cha 3 kwa mujibu wa huu mswada kama itakavyojulikana kwa ufupisho (MHUMM).

Mhe. Spika, aidha na mimi niseme kwamba kama maoni ya wenzangu waliotangulia ni kwamba hali halisi ya usafi wa mji inaonekana wenzetu wa Baraza la Manispaa sijui kazi imewashinda au tuseme inakuwaje? Lakini kupitia sheria hii basi nadhani Baraza la Manispaa litakuwa limepata msaidizi kama wenzangu walivyotangulia kusema. Wamependekeza kina Mhe. Najma na wengine na mimi ningependa kusema kwamba kupitia Shehia za Mji Mkongwe basi wanaweza wakaunda kamati za usafi na wakaona namna gani wanaweza kufanya kazi zao au mamlaka itaajiri kampuni kwa ajili ya kufanya usafi na wananchi wakaendelea kuchangia, nadhani hilo halitakuwa jambo baya.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nilikuwa napenda sana kukadhia kwani wenzangu wameshasema lakini kwa sababu ya umuhimu na madhumuni ya huu Mji Mkongwe kupewa hadhi ya urithi wa kimataifa. Mhe. Spika, hakuna shaka ni kwamba ile haiba ya mji huu ni lazima tuiwekee mkazo wa uhakika, lakini ni kwamba tuwe tuko katika hali ambayo tumekusudia hili jambo kweli kweli.

Mhe. Spika, Mji Mkongwe sasa hivi wengine wanasema kwamba pamoja na mambo mengine ni kwamba tumo katika hali ya kiutalii, labda ndio maana imepelekea kukawa kuna vinyago na bahati nzuri au mbaya kuna vinyago mpaka kwenye baadhi ya vibla vya misikiti. Bahati mbaya zaidi kuna vinyago wenye roho na wasio roho, inasikitisha sana. Kwa hivyo, nasema hivyo kwa sababu mimi binafsi nimezaliwa katika Mji Mkongwe, hapo Mnazi Mmoja na nimekuliwa pale penye Posta Kongwe na sasa hivi katika hali ya kurekebisha mji au kukua kwa mji naishi hapa Michezani nayo nadhani itakuwa imo katika mamlaka ya Mji Mkongwe kwa mujibu wa huu mswada wetu.

Mhe. Spika, kwa kweli kule tunakotokea hali haikuwa hivyo, amesema hapa Mhe. Nassour kwamba Mji Mkongwe una mpaka harufu zake na kila harufu ina ainisha wakati. Kwa hivyo, kuna harufu za asubuhi, kuna harufu za mchana, kuna harufu za jioni na kadhalika. Leo ukenda harufu ni moja ambayo huwezi

ukatambua ni kitu gani na bahati mbaya sana ni harufu ambazo hazipendezi. Mhe. Spika, mimi ninachokusudia kusema hapa katika hili ni kwamba sababu za Mji Mkongwe kuwa ni urithi wa kimataifa ni pamoja na hali halisi ya muonekano wa ule mji na vivutio vyake vilivyomo ndani yake, yakiwemo majumba ambayo yana ufundi wa aina yake wenye varanda za mbao, milango iliyopambwa vizuri, kuna vichochoro vya Mji Mkongwe, kuna kivazi cha hao wakaazi wa Mji Mkongwe.

Pia kuna vitu ambavyo wenzetu watalii mara nyingi wanapofanya kitu hawafanyi tu kwamba kaamka afanye ndio anafanya. Wenzetu wana kawaida wa kusoma utamaduni ambao kwa kweli na sisi tunapigiana kelele sana kwamba tuwe nao. Kwa hivyo, anapokuwa na *interest* ya kuona hivi katika hii miji yenye urithi wa kimataifa hii Zanzibar ikoje huwa anapitia kwenye vitabu kwanza, anaona vitu vilivyoanishwa mle. Kwa hivyo, anapotoka kwao anakusudia kuja kuona mabwawa yaliyoko Hamamni, anakusudia kuja kuona vitu vyengine tofauti ikiwemo na iliyokuwa gati yetu ya mvungu nayo ilikuwa katika masuala haya.

Mhe. Spika, wanapokuja watalii badala ya kuona vitu hivyo inabidi wapate kazi ya kutafuta kwa sababu unapoingia Mji Mkongwe kunakuwa hakuna tofauti sana na Arusha na nadhani kwa ukereketwa wangu mimi ni kwamba ile haiba inakuwa inafunikwa na utamaduni mwengine usiokuwa wa Mji Mkongwe na zaidi usiokuwa wa Zanzibar. Kwa sababu unapokutana na picha za Mmasai anaruka tulitegemea tuone picha ya mtu anacheza ng'ombe, tulitegemea tuone mtu kama sio yeye mwenyewe amebeba mdeli wa kahawa basi japo picha yake, kama sio mama aliyetia ushungi kama wangu basi angalau tungeona picha.

Mhe. Spika, niliwahi kuona wakati fulani picha za Bikidude amejitanda vizuri vimebandikwa mpaka Kiembesamaki, sijui kwa nini zisiwekwe picha kama zile Mji Mkongwe. Mhe. Spika, sasa hivi kidogo tumeacha vazi lile la buibui la zamani la Kiswahili. Hizo ndio picha ambazo tungetegemea watalii watakapokuja katika Mji Mkongwe wazikute badala ya zile zilizopo kwa sababu zile zilizopo hazioneshi haiba ya mji lakini hata utamaduni na silka na desturi ya Mzanzibari. Kwa sababu picha zenyewe saa nyengine unaweza kumkuta mtu yuko hivyo hivyo kainama huku anapiga ngoma.

Mhe. Spika, katika majukumu au malengo tuliyatafsiri ya hii mamlaka basi hili lipewe mkazo wake tena katika kupewa kipaumbele ili yale malengo na madhumuni ya kuonekana kama kweli Zanzibar kupitia Mji Mkongwe imepewa ile hadhi ya kuwa na urithi wa kimataifa, basi iwe inajionesha wenyewe hata ikiwa ni picha za kuchora, hata ikiwa ni vifaa ambavyo vitakuwa viko pale basi viwe vinaonesha kwamba hii ni Zanzibar.

Mhe. Spika, basi ikiwa haikufanywa hivyo basi mtu atamalizia Arusha kwa sababu kule anaweza kinyago cha twiga na twiga mwenyewe, atamkuta mbuni, atamkuta tembo mwenyewe na kinyago cha tembo. Hata hawa wamasai wanaoruka kwenye picha lakini kule atawakuta wanaruka wenyewe na kadhalika. Mhe. Spika, jambo hili nilikuwa naona ni mambo ambayo kwa sasa na hususan kupitia sheria hii ambayo katikati ya mchango wangu nasema naiunga mkono mia juu ya mia kwani hili ni suala ambalo halifai kuwepo katika Mji Mkongwe linapunguza haiba ya mji huu.

Mhe. Spika, hii ni *challenge* ambayo tunaomba sana ikishapitishwa sheria hii ili tuanze kuona ile aliyoieleza Mhe. Said Ali Mbarouk kwamba hata pale Sanaa ukenda unapoingia kwenye hilo eneo ambalo liko *reserved* basi unaona kama kweli hiki kitu kiko hivi. Mhe. Spika, tofauti na sasa hivi kwa huku kwetu inakuwa bado tumeifunika haiba ya mji huu kwa vitu ambavyo havihusiani na Zanzibar. Mhe. Spika, ikiwa ni masuala ya utalii iko Kiwengwa na ukanda wote wa Afrika Mashariki kule nafikiri kuna maeneo makubwa na mazuri yakuweza kueka hivyo vitu kama vitakuwa vinahitajika vikae kwa upande ule lakini bado tuweze kuithamini hii kwamba Mji Mkongwe imefanywa ni urithi wa kimataifa.

Mhe. Spika, mimi kupitia mchango wa Mhe. Najma Khalfan Juma nilikuwa nataka kuona haya maeneo ambayo yako nje ya mji huu na pengine yamekuwa nje zaidi hata lile eneo linaloitwa Bafazone ambayo inajieleza katika huu mswada. Mhe. Spika, hapa tunakusudia kufanya nini kwa sababu hata hawa wenzetu wanapokuja kufuatilia mambo ya mji huu bado wana kitu kinachowafanya waendelee na wanafika mpaka Kijichi na maeneo mengine kama hayo kwa sababu haya yote yanambatana na wale wale wa Mji Mkongwe. Kwa hivyo, nilikuwa nataka kuona na haya tunayachukua kivipi kwa sababu yanataka nayo kuendelezwa panapoharibika panataka kutengenezwa sasa je, mamlaka itakuwa inahusika vipi katika masuala na maeneo kama haya.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nilikuwa nataka niseme suala hili la kuendeleza na kusimamia maeneo ya wazi ya bustani. Mhe. Spika, wenzangu wameshasema mengi kuhusu hili lakini katika kuweka mkazo maana yake ndio tunataka haya mambo tuone yanakwenda kwa haraka hasa tumefurahi kwamba hii sheria imekuja hapa Barazani. Mhe. Spika, kwa kweli Jamhuri Garden inatutia aibu sana na imekuwa aibu kubwa zaidi baada ya hawa wawekezaji wa Benki ya *FBME* wao wametengeneza pale jirani na bustani na wameweka parking basi wenzetu wa manispaa wameidaka sasa hivi imekuwa yao wao.

Mhe. Spika, siku hizi ukisogea pale mtu wa manispaa anataka ulipie, kumbe wenyewe watu wa *FBME* wameweka wewe mteja unapokwenda pale usihangaike na gari lako uweze kuliweka pahala pazuri, lakini mara lile eneo limeshachukuliwa na manispaa. Hili wanaliweza sana na ninawapongeza kwa hilo, lakini uchafu kwenye mji umewashinda, bustani ya Jamhuri Garden ambayo pengine ina historia yake kubwa nisiyoijua mimi mna jaa ndani ya bustani kama lililokuwepo Saateni itakuwa tofauti yake la Saateni lilikuwa ni kubwa la pale ni dogo. Hiyo ndio hali halisi.

Mhe. Spika, ikiwa mamlaka itahodhi maeneo haya na wengine wamependekeza kwamba hata lile eneo baina ya Tembo Hoteli na Starehe Club pia pafanywe hivyo. Mhe. Spika, bado hivyo havijatosha kwa sababu mote humo mkishatengenezwa na mimi nasisitizwa kwamba mtengenezwe basi sisi tu wa Mji Mkongwe na Bafazone yake hapajatutosha na wanaokuja wengine na wao huwa wanakuja huku huku Forodhani. Kwa kweli watakaokuwa wanahusika na wao itabidi waisaidie mamlaka kuona kuna maeneo nje ya Mamlaka ya Mji Mkongwe ambayo yatakuwa yanawapa muda watu ambao wana nafasi ya kusema wanataka kupumzika kama mfano ambao umefanywa pale katika majumba ya Mombasa kuna pahala panaitwa Miniforo. Mhe. Spika, kitu kama kile kinaweza kikafanywa sehemu za Fuoni, Tunguu ambako sasa hivi waheshimiwa wengi wanajenga kwa sababu ukitoka Tunguu ukaja Mji Mkongwe kidogo inakuwa matatizo.

Mhe. Spika, nilikuwa napenda nimalizie kuona kwamba kwa maeneo ambayo yamo ndani ya Mji Mkongwe basi mamlaka ichukue hilo jukumu. Lakini na wale ambao walikuwa na jukumu hilo basi katika maeneo yao ambayo yako nje ya Mji Mkongwe na wao waone kwa namna moja au nyengine wanapunguza kazi ya wale ambao wako mbali ili waweze kupata maeneo mazuri yakupumzika na kupumzisha akili. Pia waangalie sana suala zima la usafi kwa sababu usafi sio tu unatakiwa katika Mji Mkongwe ambao wageni wengi ndio wanakuja kutembea, lakini sasa hivi wageni wanakuja zaidi ya kutembea kwa sababu mitaani huko utawakuta wapo. Mhe. Spika, sio vyema waondoke hapa wakapeleke hadithi tofauti kwamba nchi ya Zanzibar iko hivi wakaisifia kwa sifa mbaya kama alivyozungumza Mhe. Nassor asubuhi kwamba badala ya kutajwa Zanzibar katika hali halisi tukaja tukataja kinyumbe chake kwa sifa ya kuwa ni wachafu.
Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa nafasi kuchangia Mswada wa Kuweka Sheria ya Hifadhi ya Mji Mkongwe. Mimi huu mswada kabla sijasema lolote nasema nauunga mkono, kwa sababu nitakuwa na mengi nitakuja kusahau. Kwa hivyo, mimi nauunga mkono kabisa.

Mhe. Spika, nauunga mkono kwa sababu vifungu vilivyotajwa humu pamoja na shughuli za vyombo ambavyo vinaundwa kwa mujibu wa sheria hii vinafanya kazi au vitafanya kazi nzuri kwa lengo la kuhifadhi. Lakini mswada wenyewe Mhe. Spika, nimeuunga mkono haraka kwa sababu unakubaliana na wazo la Baba wa Taifa. Na katika mazungumzo yangu Baba wa Taifa mimi nakusudia Mzee Abeid Amani Karume.

Mhe. Spika, yeye alitia mkazo sana mji huu mkongwe uhifadhiwe, tulifanya sheria Nam. 3 ya mwanzo na hivi sasa ile tunaiweka kando tunatengeneza mpya pia kutilia mkazo wazo la Mzee Karume kuwa mji wetu huu mkongwe wa Zanzibar uhifadhiwe. Kwa hivyo, mimi namshukuru sana na kumpongeza Mhe. Waziri kwa kutekeleza wazo la Baba wetu wa Taifa Mzee Abeid Amani Karume.

Sasa katika mji humu nakusudia kuchangia vifungu vitatu tu Mhe. Spika, kifungu cha 7, 8 na 10 lakini mengi yatakuwa ya ujumla katika kuboresha hivi vipengele vyote vilivyotajwa.

Mhe. Spika, Mji Mkongwe hivi sasa kuna mambo matano muhimu ambayo yanafanyika, umuhimu wa mambo hayo yameangukia kwenye utalii, kwenye mambo ya historia, biashara, uvuvi pamoja na mawasiliano. Mambo haya ni makuu yako katika Mji Mkongwe. Sasa baada ya sheria hii Mhe. Waziri atakuwa na kazi, lazima wenzake wanaohusika na mambo haya niliyoyataja wampe msaada wa kutosha washirikiane ili aweze kukamilisha kazi za mamlaka hiyo.

Katika kuhifadhi kuna mambo ya majengo, yamezungumzwa na wajumbe hapa. Sasa majengo tunahifadhi yale yaliyopo, tunahifadhi usanifu wake, tunahifadhi vifaa vilivyotumika kwa majengo hayo, nafikiri haya yote ya kuzingatiwa.
Mhe. Spika, hivi sasa majengo mengi yameanza kuanguka na wenye uwezo wao wameanza kuyatengeneza, lakini wameanza kutengeneza kwa mambo ya saruji na matufali, madirisha mengine wametoa vioo ingawa wametia *design* kama ya mbao. Hii kweli watakuwa wanahifadhi kwa sababu watakuwa wamejenga nyumba, lakini bado haitaleta sura ya Mji Mkongwe. Mji Mkongwe umejengwa kwa udongo, chokaa, mawe, boriti zake za miti na pia imezungumzwa kuwa utamaduni wake zile kila baada ya muda huwa zinafanyiwa ukarabati, kila baada ya miaka miwili zinatiwa boriti mbili kwanza, anaacha fundi anakuja baada ya wiki tatu mpaka anamaliza, yaani kazi ile ya ukarabati inakuwa ni ya kudumu katika mji wetu mkongwe na hivyo ndivyo ilivyokuwa.

Lakini hivi sasa ujenzi mtu anakuwa anajenga jengo la kudumu, sakafu zege, nguzo za kangiriti. Kwa hviyo, nafikiri hili Mhe. Waziri katika utekelezaji lizingatiwe, yale majengo yenyewe yawekwe wazi kwenye hiyo kanuni namna gani majengo haya yanajengwa, yanajengewa udongo kama vile yalivyokuwa zamani au usanifu tu *design* iwe vile vile, lakini mtu anaweza kutumia vifaa vyovyote. Hili Mhe. Waziri liwekwe wazi.

Lakini pia historia ya mji ule, yamezungumzwa hapa mambo ya mapishi, mavazi, sijui harufu, mimi nitazungumzia kwanza hii harufu kwa sababu nimeona imetajwa sana. harufu ya Mji Mkongwe mimi natafautiana na wajumbe waliozungumza, harufu ya Mji Mkongwe inatofautiana na mahala penyewe.

Funguni Mhe. Spika, historia yake kule kuna sifa, saa zote unaziba pua, tumekwenda nunua kwa kupakia madau na ngalawa kwa Tumbatu sisi watu wa Kikungwi na wengine. Ile haisemwi asubuhi wala jioni, wote wanaojua Mji Mkongwe Funguni harufu yake Mhe. Spika, ni sifa, yale mafuta ya kupakia ngalawa, matumbo ya papa yanawekwa pale yanarowekwa. Ras-el-khaima kuna mabanda ya papa pale wakati wowote unapokwenda unasikia harufu ya papa, ukienda *CG* pale kuna harufu ya karafuu. Kwa hivyo, sasa hivi usitarajie labda hii harufu ya asubuhi hii ya jioni, harufu ya asubuhi na jioni kwa funguni ni sifa ya matumbo ya samaki. *CG* karafuu wakati wote utaikuta.

Kwa hivyo, nafikiri mimi nitofautiane nao, ingawa utapokuja sehemu za Baghani kutakuwa na harufu yake, nayo pia kwa siku hizi imebadilika kutokana na wakaazi walioko. Kwa sababu sasa hivi wako Wamasai utategemea harufu kama ile iliyopita Baghani ukaipate? Kwa hviyo, ndugu yangu Mhe. Mazrui alivyozungumza hiyo itakosekana kutokana na mabadiliko. Wale wakaazi wa Baghani na Shangani waliokuwa na harufu hiyo uliyoikusudia ya uturi na mawardi sasa wako wamasai hawatii, wanja wanajipaka udongo kweli utaipata harufu hiyo?
Kwa hivyo, Mhe. Spika, hayo tunayazungumza lakini yatakwenda kwa mujibu wa mazingira tuliyonayo. Hivyo Mhe. Spika, hilo lilikuwa sehemu ya kwanza.

Lakini kwenye majengo yamezungumzwa kuwa majengo makongwe yaweze kufanyiwa ukarabati. Katika mswada huu wameshirikishwa wadau, nafikiri wadau wakubwa walikuwa wamiliki. Kwa kweli hali ya ujenzi hivi sasa gharama zimekuwa kubwa. Kwa hivyo, mimi nakubaliana na wazo kuwa hivi sasa waorodheshwe wote wenye majengo yale, wanaweza basi watafutwe wabia yatengenezwe namna mamlaka itaona inahisi na yeye apate sehemu yake. Kwa sababu kuingia ubiya si ubaya, tutakuwa tunamsaidia yeye, tutaisaidia serikali lakini bado tutakuwa na utaratibu wa kuutunza ule mji wetu namna tunavyotaka.

Jengine kuna majengo muhimu hivi sasa, kama pale Darajani pana jengo moja refu sana sijui kama la serikali au la mtu binafsi. Hivi sasa pale halipendezi, lakini lina shughuli nyingi. Upande wa barabarani ulikuwa ndio upande wa nyuma lakini sasa hivi kumetolewa maduka, na upande wa usoni wa kwendea kwa Salehe Madawa nako pia kuna maduka, jengo kama lile la zamani ukarabati wake hauna uhakika hili Mhe. Spika, lifanyiwe uhakiki mapema. Kwa sababu nalo linaweza kutoa haiba nzuri kwa vile liko kwenye njia kubwa ya Mji Mkongwe wetu, sisemi upande wa Forodhani huku tumeshampata Aghakhan keshasema anazungumza, lakini upande mwengine huu lazima tuhakikishe na sisi wenyewe tunafanya njia zetu za kufanya utafiti na kutafuta fedha za kuweza kuyaokoa yale majengo.

Lakini eneo la Mji Mkongwe, mimi Mhe. Spika, ningesema visiwa vya Bawe na Changuu vingeongezwa kwenye orodha au kwenye Mamlaka ya Mji Mkongwe. Kwa sababu nako kule ni sehemu kulikuwa na majengo lakini sasa hivi watu wanajenga hoteli wanavyotaka, bado kulikuwa na urithi wa ujenzi wa zamani sasa unapotea, ili katika kuweka huko madhali na kule ni sehemu ya karibu na Mji Mkongwe basi Mhe. Waziri nigependa nako kukawekwa kwenye ukanda wa Mji Mkongwe wa Zanzibar.

Mhe. Spika, jengine barabara. Barabara hivi sasa tunaambiwa tuna *master plan* ya Mji Mkongwe lakini bado mimi kwa hakika sijajua vipi? Lakini kama tunahifadhi basi kuna mambo mengi ya kuhifadhi. Kuanzia Msikiti wa Ijumaa wa zamani palikuwa na njia inayopita *Library* ya Agakhan inapita Kiponda mpaka stesheni ya Darajani. Njia ile ukitoka huku unaweza kukata unapita kwa gari mpaka Darajani, hivi sasa huwezi kupita, utamaduni wa wakati ule ukishakufika Agakhan pale kwa sababu pale palikuwa wakiachiwa watu kwa gari, kwa miguu wanakata kati, wanapita msikiti wa Masinashir na wengine wanapita kwa Gobal Samji pale, *spice in* wanakuja zao Darajani kule kunaachiwa zipite gari. Hivi sasa kumezibwa huwezi kupitisha gari.
Kwa mfano, Benki ya Watu wa Zanzibar napo palikuwa ni njia nyembamba lakini unaweza kupita ukatokea Kanisani mpaka *Joes Corner* halafu unateremka mpaka Vuga, Mnazi Mmoja kwa gari, hivi sasa huwezi kupita.

Sasa Mhe. Spika, katika mambo hayo aliyozungumza Mzee Karume basi ilikuwa utaratibu huu wenzetu wa zamani ulikuwepo lakini fikira zake ilikuwa ni lazima muwe na sehemu ambazo akiweko mgonjwa au huduma za zimamoto ziweze kufanywa, lakini sasa hivi mnatiwa vikuta. Sasa sijui kama ni mamlaka au Baraza la Mji, hili ni tatizo, kama haziwezi kupita gari zile za *touring car* basi hata zile bajaji Mhe. Spika, lakini ziweze kupita kwa sababu tuna walemavu na wao wana haki yao waweze kutumia. Kuwe na utaratibu wa barabara zile ziwemo kama zamani kwa sababu ndio tulikuwa tunahifadhi.

Mkunazini mpaka Zenabay Skuli ya Hamamni gari zilikuwa zikifika zinapeleka bwana harusi na mambo mengine, lakini sasa hivi haziwezi kufika. Sasa kama tunahifadhi basi tuhifadhi na yale mambo yaliyokuwepo, na hii sifikirii kama ni mamlaka ni Baraza la Mji.

Sasa nafikiri ili mambo haya yafanywe Baraza la Mji linahusika zaidi au katika mambo haya Baraza la Mji liondolewe mkono wake ili mamlaka iweze kufanya kazi vizuri. Lakini kuna kanuni za Baraza la Mji zinafanya kazi na mamlaka ya vyombo hivi viwili vyote vina mamlaka yake, vitafanya ugumu katika utekelezaji wa shughuli hizi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, upande wa barabara katika Mji Mkongwe hivi vichochoro naomba nalo lizingatiwe, hivi sasa kuna usumbufu hasa kwa zimamoto.

Juzi pale palipokuwa Makao Makuu ya Wizara ya Elimu palitaka kupita gari angalau zile *rover* basi ilibidi wakaazime nyundo kwanza kuondoa viguzo kwenda kuzima moto. Haya ni mambo ya kawaida. Kwa hivyo, uwekaji wa viguzo tu ndani ya Mji Mkongwe nao uzingatiwe, kwa sababu sehemu hizo zinakaa watu mnatakiwa huduma na kila kitu.

Mhe. Spika, nije katika kifungu cha 10(8)(b) mwisho wa Sehemu ya Pili. hapa inaonesha katika kifungu cha (8) Mjumbe wa bodi ikijumuisha Mwenyekiti na Mkurugenzi Mkuu pamoja na muajiriwa wa mamlaka hatoruhusiwa katika kipindi cha utumishi wake na baada ya muda wa miezi 12 baada ya kumalizika au kusitishwa kipindi cha utumishi wake kwenye mamlaka.

Kifungu (8)(a)

> “Kuingia kwenye mkataba wa kazi au mkataba wa kutoa huduma kwa mamlaka ndani ya kipindi cha ajira ya mfanyakazi na mamlaka”. Hiyo sina matatizo.

Kifungu cha (8)(b)

> “Atajipatia au atahodhi maslahi yote ya kifedha yawe kama ya muajiriwa, mbia, mshika hisa, afisa au amejiunga kwenye biashara yoyote au taasisi inayotoa huduma kwa mtu yeyote ambaye yupo ndani ya eneo la hifadhi”.

Mhe. Spika, hapa sijafahamu, kama nimefahamu vizuri bora mambo kama haya yangewekwa kwenye hizo kanuni, lakini kuweka kwenye sheria ni kumnyima haki, kwa sababu tu amefanya kwenye mamlaka halafu asiwe na biashara au kitu chengine chochote pesa zenyewe za siku hizi na pale keshaona pana njia. Nafikiri hii itakuwa haifai, kwa sababu hii itambana hata Mhe. Waziri, mana

naona ana mkahawa na yeye ndio kiongozi wa mamlaka hii kama atakuwa hahodhi, au tutamnyima Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kuwa mjumbe kwenye bodi hii. Kwa sababu na yeye ana *Mazsons* pale na kama mtu anataka anaweza kumpa mjumbe wa bodi ili ile kazi aache.

Kwa hivyo, nafikiri kipengele hiki kitizamwe upya tusimnyime haki au usijihofu Mhe. Waziri juu ya hili, nafikiri kifungu hiki naona kitamnyima mfanyakazi tu kwa sababu asijiendeleze kwa kuwa anafanya kazi kule. Kufanya kazi kwenye mamlaka sio kama ndio utakuwa tajiri au utakuwa umeshatosheka na mambo huhitaji zaidi, ingekuwa angalau mtu ukishakufanya kazi mamlaka kila kitu bure au vipi? Lakini bado atakuwa anahitaji mambo. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kujikurupusha kutafuta njia pengine (riski) asifungwe. Mimi hilo ni wazo langu.

Mhe. Spika, jengine kuhusu hifadhi za mazingira ya bahari. Na mimi nakubaliana na wajumbe wote waliosema kuwa hivi sasa bado fukwe zetu hasa kuanzia Ikulu unapita pale ras ya Shangani kuendelea mpaka Forodhani hali ni mbaya sana na sijui nani mwenyewe, kama ni Mji Mkongwe, Idara ya Bandari, Baraza la Mji. Kwa sababu hapa pana gharama kwa vile sasa hapana mwenyewe, lakini nafikiri kama pangekuwa pana ruhusa ya kufungwa gati Manispaa ingekwishasema hii *parking*.

Nina hakika Mhe. Spika, zingetengenezwa vizuri, unaweka boti wangesema hii ndio *parking* Manispaa keshachukua pesa, lakini kwa sababu panataka gharama ya kutengenezwa sasa kila mmoja mwenyewe hapana, lakini hii ni hatari. Kwa sababu ardhi, bahari inahatarisha maisha ya majengo ambayo yako karibu na huu Mji Mkongwe.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa, ili sheria hii iweze kufanya kazi basi tusiwe na hiyana kwenye bajeti, kwa sababu mambo ya humu makubwa sana. Tumezungumza humu mna mambo ya kibiashara, barabara na kila kitu, sasa kutengeneza sheria tu hiyo kutengeneza nyumba moja sijui shilingi bilioni ngapi na majumba ya Mji Mkongwe si kidogo, moja moja tu kila mwaka. Kwa hivyo, nafikiri Mhe. Spika, wajumbe ndio tumepewa mswada nasema wengi tushakuwa tunaukubali, lakini pia tuhakikishe ili hii sheria iweze kufanya kazi basi tuiambie serikali itenge fedha za kutosha ili mswada huu uweze kufanya kazi.

Hali ya barabara gharama zake anazijua Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi, kilo mita moja shilingi milioni mia tatu, sasa tukianza tu pale Kiponda – Darajani, Forodhani – Malindi na nyengine, mpaka Mlandege sasa ni Mji Mkongwe basi kwa barabara tu kwa mwaka mmoja tunataka angalau shilingi bilioni saba sijui? Au ngapi mbali kulikamata hilo

jengo kubwa la Darajani angalau kulitengeneza, huko kwengine tumeshapata mfadhili Agakhan, lakini huku kwengine bado hatujapata mfadhili.

Lakini la mwisho Mhe. Spika, kuhusu maji machafu. Sijui nani tumpe dhamana, watachukua wenyewe mamlaka au Baraza la Mji nalo ni tatizo. Maji machafu katika Mji Mkongwe haiba yote, katika jambo la harufu hiyo hawajaliona wazee, kuna harufu sasa hivi inayotoka kuanzia hapo kwa Mzee Khamis Machungwa, Haile-es-Selasie, ukipita Darajani, wakati mwengine samaki japo yuko juu ya kisaruji hutotamani kumnunua kwa ile harufu inayotoka.

Kwa hivyo Mhe. Spika, na hili la maji machafu hebu tulitizame ni Mji Mkongwe, Manispaa au pawe na mashirikiano mazuri, hao wageni hawatoweza kuja kutembea kwenye harufu mbaya anaweza kutembea huku kaziba pua. Lakini pia yale mabanda ya papa yaliyokjo Ras-el-Khaima, hivi sasa yanatumika vibaya na upo uchafu, basi nako katika ujenzi wa nyumba kuanzwe kutengenezwa kule kidogo kidogo, kama tunaanza Hoteli yetu ya Bwawani mwenginemo basi kidogo kidogo tutengeneze na kule yale mabanda isiwe kama kambi ya wala unga! Ule ni Mji Mkongwe nao ndio tumeshautungia sheria tuutekeleze basi na kule tukutizame kwa jicho la hali ya juu kabisa.

Mhe. Spika, moja nilikuwa nataka kulisahau kwenye mambo ya utamaduni. Mji Mkongwe kuna mambo ya utamaduni ya vyakula hata ngoma. Mji Mkongwe zamani ukienda Malindi saa hizi unapata ile ngoma ya shabuwan, hakuna sasa hivi disko, taradhia, sasa lazima tuhakikishe mtu anakwenda Mji Mkongwe anakuta yale mambo ya kule, dane dane ilikuweko ya vijiti wanacheza mpaka harusini wakicheza wenyewe Wahindi, sasa hivi unakuta disko, taradhia ndio inayolia kule, sijui msondo.
Kwa upande wa utamaduni nao tuhakikishe mtu anakuja kutembea Mji Mkongwe kama kwa historia basi ayakute mambo yale, anaikuta ile ngoma ya kifuani kabisa nayo ifanyiwe utaratibu, kama haipo wapigaji wapo. Kama hivi sasa watu wanavyotaka haluwa wanakwenda kwa Kidemi, wanaotaka shurba wanakwenda Corbies, lakini sasa ukienda Forodhani utakuta vyakula vikubwa chipsi, si vitu vya Forodhani hivyo, zamani unakuta zarubia, ladu, bajia, hivyo angalau vya moto moto lakini pamojana mambo ya vyakula hayo ndio yanayoleta haiba ya Mji Mkongwe.
Mhe. Spika, leo mtu ametoka huko anakuja Mji Mkongwe ayakute yale mambo ya Mji Mkongwe hasa. Mimi nazungumza hivyo kwa sababu ni mkaazi wa kule robo karne, miaka 25 nimekaa kule, kwa hivyo, nazungumza kwa kuyajua. Mhe. Waziri anajua kule yeye mwenyeji, Mhe. Najma Halfan jirani yangu, Ndugu Nassor Ahmed jirani yangu, Fatma Abdulhabib Fereji, hao ndio watu wa Mji Mkongwe, nafikiri wataniunga mkono kwa haya ninayoyazungumza.
Mhe. Spika, mimi naunga mkono hoja, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Spika, mimi niungane na yote yaliyosemwa na wenzangu kuhusu Mji Mkongwe. Lakini naomba nianze kifungu cha 4(f) ukurasa wa 45 kinachozungumzia majukumu ya Mamlaka ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe. Kifungu hiki kinazungumzia kufanya juhudi mbali mbali ili kufikia malengo yaliyowekwa kwenye mpango usimamizi wa urithi wa Mji Mkongwe. Nadhani mimi niwapongeze sana wataalamu wa wizara kwa kukiweka kifungu hiki kwamba ni kimoja katika malengo ya Mji Mkongwe.

Mhe. Spika, matatizo yanayozungumzwa leo hapa yote yametokana na kutokukifanyia kazi kifungu hiki. Kwa sababu ukiangalia malengo ya *heritage site* kwa nini *UNESCO* wanachagua hiyo miji na yale masharti na kazi za kufanywa ni chache sana ambazo zimefanywa na Mamlaka ya Mji Mkongwe. Sasa sisi tunaotoka sekta ya utalii tunauza Zanzibar *point* yetu yakwanza ikiwa ni Mji Mkongwe. Tunauuza Mji Mkongwe kwa mambo kadhaa, tunauza Mji Mkongwe *architect* ya Mji Mkongwe ambayo ni ushahidi tosha wa kuonesha watu wote ambao walifika Zanzibar.

Lakini pia tunautangaza, nimerekebishwa samahani, hatuuzi, tunatangaza. Tunautangaza Mji Mkongwe kwa ufundi wa zile nyumba zilivyojengwa ambazo zinaonesha ufundi wa mataifa mbali mbali ambayo yameingia Zanzibar. Tunauza Mji Mkongwe kwa zile barabara, vichochoro vile, ambavyo navyo vinatoa ushahidi ukilinganisha na vichochoro vya nchi nyengine kama Istamble, Rom na miji kama hiyo au hata sanaa aliyosema Mhe. Said Ali Mbarouk. Kuna vichochoro vile vile na hiyo nayo inaonesha kwamba ni *architect* ya watu gani ambao walikuja Zanzibar.

Lakini pia tunautangaza Mji Mkongwe kwa kutumia vifaa vilivyopo. Kwa mfano milango, ambayo inatoa historia tofauti, milango yenye ufundi wa Kihindi, ufundi wa Kishihiri, ufundi wa Kizanzibari ambayo wamechanganya sasa, milango ya Kiarabu, Kihindi wamechanganya wamefanya ya Kizanzibari na ikapewa jina *Zanzibar Dor* tunauza pia.

Pia tunauza samani zilizokuwa zikitumika au zilizoingia hapa Zanzibar, lakini nyingi utazikuta katika Mji Mkongwe na ndio maana tuna maduka ya *antics* na yote tunapiga picha na tunaonesha. Tunamwambia mtalii ukija utaona vitu hivi ndani ya Mji Mkongwe.

Ndani ya Mji Mkongwe tunawatangaza pia watu wa Mji Mkongwe. Kwa sababu tunasema kwamba ukija Zanzibar utaona mchanganyiko wa utamaduni, utakuta sura za watu mbali mbali, watu waliochanganya Mwarabu kwa Muhindi, Mwarabu kwa Mswahili, Mswahili kwa Muhindi, Mchina kwa Mswahili, yaani watu wa aina mbali mbali. Tunasema Mji Mkongwe umekuwa

characterized na mchanganyiko wa damu, sasa watalii wakija wanayakuta kweli Mji Mkongwe.

Halafu tunautangaza Mji Mkongwe kwa mambo mengi, *religions tolerance*, hapa pana kanisa, hapa msikiti, watu wanaishi vizuri na hawagombani mambo mengi tunauza Mji Mkongwe au tunautangaza Mji Mkongwe. Kwa hivyo, mtalii anapokuna anategemea yale ambayo tunamuonesha ayakute. Kinachotukwaza sasa ni hiki kimoja.

Suala la kwanza ni uhamiaji ndani ya Mji Mkongwe, ndani ya Mji Mkongwe kuna nyumba zinazomilikiwa na watu wenyewe wa Mji Mkongwe, ndani ya Mji Mkongwe kuna nyumba zinazomilikiwa na Idara ya Wakfu na Mali ya Amana, ndani ya Mji Mkongwe kuna nyumba za serikali. Sasa mafungu matatu haya au makundi haya kukua kwa utalii kumewafanya wageuze nyumba zao ziwe miradi ya kuwaingizia fedha.

Kwa mfano, kuna wenye nyumba ndani ya Mji Mkongwe ambao wameziuza wenyewe wamejenga Kwarara, Mombasa, Tunguu na maeneo mengine, lakini nyumba yake ya Mji Mkongwe ni kitega uchumi chake.

Lakini kuna nyumba zinazokodishwa za Serikali za Wakfu na Mali ya Amana. Hizi nyumba zinakodishwa kwa bei rahisi mno kiasi ambacho wenzetu wanaoleta hivyo vinyago na machinga wengi wamejazana huko ndani. Utakuta nyumba moja wanakaa watu 20 au 30. Wanakaa kwa zamu, msimu huu wanatoka wengine wanaingia, lakini sio sura ambazo sisi tunazitangaza tukiwa nje. Kwa maana hiyo, mtalii akija anakuta sura tulizozitangaza ziko finyu, ziko Kwarara, Tunguu, Mombasa, lakini sura za Mji Mkongwe sasa ni nyengine.
Kwa hiyo, ile uhifadhi wa urithi wa utamaduni na urithi wenyewe wa Mji Mkongwe unakuwa haupo. Hii inasababisha sasa Zanzibar tuingie kwenye hatari ya kufutwa kwenye Mji Mkongwe.

Sasa nimefurahishwa sana na kifungu hiki cha kuyafanyia kazi yale masharti yaliyowekwa na *UNESCO* ya usimamizi wa miji ya aina hii. Ningeomba sana Mamlaka ya Hifadhi ya Mji Mkongwe kuyafanyia kazi hii ili kurudisha hadhi au kutoa sura halisi ile ambayo wanaofanya kazi ya utalii wanakwenda kuitangaza basi sura ile iwepo.

Mhe. Spika, hapa suluhisho ni kuongeza kama walivyosema ku-*control* majumba yale na uhamiaji wake. Lakini kubwa ni kuongeza mara chungu nzima kodi ya majumba yale ili ku-*restrict* wakaazi katika mji ule.

Mji Mkongwe sasa umeelekezwa zaidi kibiashara na ile dhana ya urithi wa dunia na utamaduni wake inakuwa haipo, watu wameelekeza zaidi kwenye

biashara na pengine umekuwa kama ni mji wa kuleta mapato. Kama alivyosema Mhe. Najma Khalfan Juma nchumi n'ndu sijui. Imekuwa zaidi ni mchumi mndu kwa sababu kweli una-*generate* mapato lakini hayarudi. Mapato yanakuwa *generated* yanavuka nchi hayarudi tena kuweka ile hali ya Mji Mkongwe. Wanaleta vinyago wanaondoka. Kwa hiyo, ningeomba sana hili lifanyiwe kazi vizuri.

Mhe. Spika, nimefurahishwa pia na kifungu cha 11© cha ukurasa wa 47 kinachomuingiza Mkurugenzi wa Manispaa na Mkurugenzi wa Sanaa na Mambo ya Kale kuwa ni Wajumbe wa Bodi ya Mji Mkongwe. Kwa sababu huwezi kuzungumza masuala ya Mji Mkongwe bila ya kuzungumza watu hawa. Hawa ndio wenye maeneo ya historia ambayo na wao wanasema yamekuwa *gazetted* yamehifadhiwa, lakini maeneo yale yale tunataka yafunguliwe na historia ielezwe ili watalii wasome historia iliyopo.

Kwa kweli kuna historia ndani ya Mji Mkongwe ambayo bado haijaelezwa. Kwa hiyo, nadhani tungefanya kazi zaidi kueleza na ikawa kivutio zaidi watu wakawa wanakuja wengi zaidi.

Tunapata maswali mengi tukiwa nje, mengine tunaweza kuyajibu, mengine hatuwezi kuyajibu kwa sababu hatuna majibu kutoka nyumbani. Kwa hiyo, nadhani tungeifanyia kazi vizuri zaidi.

Mhe. Spika, jengine kuna mchangiaji aliyezungumzia Siku ya Mji Mkongwe. Mimi ningependa sana Mamlaka waikubali hii Siku ya Mji Mkongwe. Kwa sababu siku hii itatupa fursa sasa ya kufanya mapitio ya ile historia a kuona nini kipo, wapi tumekwenda vibaya, wapi turekebishe. Kwa maana hiyo, kama tutaiadhimisha kila mwaka ina maana tunaweza tukawa na *festival* ya Mji Mkongwe pengine kwa wiki nzima. Wiki moja tukaangalia bandari ilivyokuwa na sasa hivi ina *improvement* na historia yote, tukawashirikisha pia na watoto wa skuli.

Wiki inayofuata majumba, kila nyumba kule Mji Mkongwe ina maana yake. Kuna nyumba sijui walionana Princess Selme na yule mzungu kwa dirishani lakini watu wanaoneshwa nyumba nyengine wala hawaoneshwi zile. Kwa hiyo, hayo ni mambo ambayo tungeweza kuyaweka vizuri na tukafanya wiki nzima siku ya bandari, siku ya majumba, mambo mengi kule. Kwa hiyo, tunaweza tukawa na *festival* ambayo itaongeza katika idadi ya watalii kuja nchini.

Mhe. Spika, katika malengo ya *UNESCO* ya kuendesha hii Miji Mikongwe wanashajiisha nchi kushirikisha wananchi wanaoishi katika mji ule kushiriki kikamilifu katika uendeshaji wa Mji Mkongwe. Nishukuru hapa Zanzibar Mji Mkongwe nadhani kuna kamati, mbali ya Kamati ya Maendeleo lakini kuna

kamati kabisa ya wenyewe watu wa Mji Mkongwe ambayo kwa kiasi kikubwa inafanya kazi na Mamlaka ya Mji Mkongwe.

Lakini mimi ningependa basi wafanye kazi kubwa zaidi ya kuhakikisha kwamba Mji Mkongwe unawekwa vile inavyotakiwa, kiusafi, watu, biashara zinazofanywa na mambo kama hayo ili kutoa sura halisi ile ya Mji Mkongwe wenyewe washiriki.

Nakumbuka nimewahi kushiriki katika sijui uzinduzi au sherehe tu ile Kamati ya Mji Mkongwe walikuwa wanafanya, lakini pia nimewahi kualikwa na Mji Mkongwe wenyewe nikazungumze na wana wa Mji Mkongwe. Mambo niliyokuwa nikiwaambia wana wa Mji Mkongwe ni kwamba mbona mnaacha mji wenu unaharibika, huu mji ni wenu, nyinyi ndio wenye Mji Mkongwe, mnatoka yaani mmeshajitekesha mnaacha watu wengine wameteka mji nyinyi mmetoka nje ya mji.

Sasa hii si sura nzuri, ni vizuri wenyewe watu wa Mji Mkongwe mkalinda mji wenu, mkaangalia biashara gani zinafanyika, mkaona tabia gani zinabadilika ndani ya Mji Mkongwe za watoto na hata watu wazima. Kwa hiyo, suala la kuwashirikisha watu litatusaidia sana katika kuuhifadhi Mji Mkongwe.

Mhe. Spika, jengine wakati napitia malengo ya *UNESCO* nimeona kabisa kwamba wameweka kifungu kinachozungumzia kwamba *UNESCO* wako tayari kutoa msaada kwa miji ambayo iko kwenye hatari. Tunapozungumza kwenye hatari wajumbe wamesema, kuna hatari kuta zinamong'onyoka kwa hiyo bahari inaweza ikala Mji Mkongwe. Kuna hatari ya usalama ndani ya Mji Mkongwe watoto wetu ambao wanakula madawa, watoto ambao wameharibika.

Kwa hiyo, mimi nadhani tukishirikiana na watu wa ndani ya Mji Mkongwe pamoja na Mamlaka, tukikaa kitako kufanya miradi mizuri, miradi ambayo inaeleweka, nadhani *UNESCO* wanaweza wakatusaidia kutoka kwenye hatari hiyo.

Mhe. Spika, nizungumze sasa ukurasa wa 58 kifungu cha 50(1) ambacho kinazungumzia "Masharti ya Kurukia". Mimi Mhe. Spika, nilikuwa naomba tu nipendekeze marekebisho kwa sababu ukisema masharti ya kurukia kama Mji Mkongwe unataka kurukia labda sijui kazi nyengine au kitu gani. Lakini kifungu kinazungumzia kwamba Mji Mkongwe unaweza kufanya kazi zake na kuruka masharti ambayo yamewekwa na sheria nyengine. Wamepewa ruhusa hiyo chini ya sheria hii. Kwa hiyo, hicho kifungu *marginal note* isomeke kwamba ni kuruka masharti kuliko masharti ya kurukia.

Mhe. Spika, katika kuendeleza Mji Mkongwe kuna maswali mawili hapa yameulizwa kuhusu *Starehe Club* na eneo lililo wazi jirani yake. Mhe. Spika, labda nikitoa ufafanuzi hapa walioulizia wanaweza wakaondosha maswali yao.

Mhe. Spika, eneo la *Starehe Club* hata sisi tunaona kwamba hatulitumii ipasavyo. Kwa sababu kwa sasa hivi eneo lile liko kwenye kodi ya mwezi. Tunashindwa kulitumia kwa muda mrefu kwa sababu tulipata maelekezo ya Mji Mkongwe pamoja na Serikali kwamba eneo lile tusilitumie wala tusimpe mwekezaji kwa muda mrefu. Kwa hiyo, tunachoweza kukifanya tukisubiri amri nyengine ya serikali tumelikodisha mwezi hadi mwezi na ni kweli kwamba pahala pale pangetumika vizuri zaidi, kwa sasa hivi hapatumiki vizuri zaidi.

Kwa hiyo, niseme tu kwamba kwa upande wetu wa kupitia Shirika la Utalii tunasubiri amri ya Serikali tutaambiwa kipi kingine. Sisi kama wapokeaji wa wawekezaji tunapokea wawekezaji lakini bado hatujaweza kutoa eneo hili mpaka tuelewane na wenzetu wa Mji Mkongwe na Wizara inayohusika. Sasa ni juu ya wizara inayohusika kutuelekeza vyenginevyo. Kwa sasa hatuwezi kupafunga tunapatumia na shirika linapata pesa hiyo ndogo ndogo.

Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na niseme tu kwamba kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini Unguja tunaunga mkono mswada huu, ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, kwanza naunga mkono mswada huu. Lakini la pili Mhe. Spika, ndani ya Baraza lako tukufu kuna kitu maarufu kimejitokeza kwa Wajumbe wako karibu wanne hivi, hawa ni wanakindaki kindaki wa Mji Mkongwe. Wa kwanza ni Mhe. Waziri mwenyewe ambaye sina hakika lakini nadhani kazaliwa Mji Mkongwe, kakulia Mji Mkongwe, kakaa Mji Mkongwe na baadhi ya shughuli zake anazifanyia Mji Mkongwe.

Lakini pia kuna Mhe. Zakiya Omar Juma, Mhe. Haji Mkema Haji na wengineo. Bahati mbaya sisi Mji Mkongwe tunauona sasa hivi tu na pengine kama si Mapinduzi tusingeuona.

Mhe. Spika, mswada huu umechangiwa na wajumbe zaidi ya 10 na kila mjumbe ambaye amepata nafasi ya kuuchangia na hata wale ambao hawakupata nafasi ya kuuchangia, wote kwa namna moja au nyengine wanauunga mkono lakini pia wanakubaliana na azma nzima ya kuwepo kwa Mji Mkongwe ukiwa ni hifadhi ya dunia.

Mhe. Spika, jengine binafsi napenda nimshukuru Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu, Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi akisaidiwa na Mhe. Hamad Masoud Hamad na wajumbe wengine wote. Mhe. Spika, mimi binafsi

nililalamika kidogo. Nilisema huu mswada ni mkubwa na ulipata siku moja ya marekebisho hatimaye Wajumbe wa Kamati hawa walichoka na mswada huu ungestahili zaidi ya siku moja. Kwa sababu ulianza asubuhi na ulimalizikia nadhani kwenye saa kumi na moja. Lakini waliweza kufanya kazi hizo wakaweza kufanya marekebisho hayo na ndio leo tuko hapa.

Mhe. Spika, ukitoa wajumbe wote ni mjumbe mmoja tu ambaye yeye alionesha pengine yuko tofauti ni Mhe. Said Ali Mbarouk alipokuwa anasema basi tungefanya utafiti tuone kama kweli tuna haja ya kuendelea kuwa na Mji Mkongwe au tufanye vyenginevyo.

Mhe. Spika, nataka nimhakikishie Mhe. Said Ali Mbarouk haja ya kuwa na Mji Mkongwe ipo na itaendelea kuwepo. Mhe. Spika, nchi ya Oman ambayo sasa hivi nadhani haimo tena inawezekana ikawa inajuta kwa sababu imefanya makosa na hatimaye imeondolewa.

Kwa hiyo, Zanzibar nayo ikifanya makosa hayo itaondolewa na hata ile shughuli ambayo Mhe. Samia Suluhu Hassan ameizungumza ya kuitangaza Zanzibar wakipitia Mji Mkongwe itakuwa nayo haipo. Kwa hiyo, pia inaweza ikapunguza hata idadi ya watalii watakaokuja Zanzibar. Mhe. Spika, kwa kweli bado kuwepo kwa Mji Mkongwe wa Zanzibar kama Urithi wa Kimataifa ni jambo la lazima.

Mhe. Spika, hili nataka niseme kwa mfano Bagamoyo nao wanao Mji Mkongwe kule Mlingotini una historia yake. Lakini pamoja na yote hayo Bagamoyo kuna mambo hawawezi kuyafanya kama hawajafika hapa Zanzibar.

Kwa mfano, hivi karibuni walikuwa wanafanya matengenezo ya jengo lao moja pale mjini Bagamoyo ambalo nadhani lilijengwa na Wajerumani. Lakini wakati wa kulifanyia matengenezo ilibidi lazima waje hapa waonane na Mkurugenzi na wapate mafundi wataalam kutoka hapa Zanzibar, wao wenyewe pale wameshindwa. Kwa hiyo, hii unaona umuhimu gani wa Mji Mkongwe huu wa Zanzibar.

Lakini jengine Mhe. Spika, Sweden wanao Mji Mkongwe ni eneo dogo sana ukilinganisha na hili letu. Kwa sababu wenzetu wameanza mbali huko kuhifadhi mji wao, ni mji ambao wale wakaazi wanaokaa pale ni akina ehe, wale “Pangu pakavu tia mchuzi” hawawezi kukaa. Wanaokaa kwenye mji ule ni watu *very expensive*, mimi na Mhe. Shamsi Vuai Nahodha hatuwezi kukaa kwenye mji ule kwa sababu ni mji ambao wanaokaa lazima wawe na fedha.

Ni mji unaotakiwa uwe umetulia hawaruhusu hata vyombo vya moto kama hizi pikipiki. Watu wanaokaa mle wanaruhusiwa kutembea kwa miguu tu. Kwa

hiyo, wale wanaokaa pale wanapata utulivu ule unaotakiwa. Hata kama kuna hoteli mle basi gharama yake ni kubwa mno. Sasa bado Zanzibar na sisi tunatakiwa tuelekee huko na nina imani kabisa kwa kweli tunaweza tukaelekea huko.

Kwa mfano, nchi kama Israel kuna mji wa Tel Aviv na Jerusalem. Lakini ukiangalia mji wa Jerusalem kwa namna moja au nyengine kuna baadhi ya maeneo yake yanalingana lingana na Mji Mkongwe, maeneo haya ni ya kihistoria pale Jerusalem. Hata uchumi wa Jerusalem pale Israel unategemea utalii. Watalii wengi wanakwenda kwenye mji wa Jerusalem na pale kuna historia kubwa. Ni mji wa kale, ni mji una historia kubwa ya dini zote.

Mhe. Spika, nashukuru niliwahi kufika kule, Mhe. Waziri wangu alinambia niende ingawa kuna vita, akanambia nenda najua unajua kukwepa risasi. Unaona historia ya pale kuwa hili ndio kaburi la Nabii Daud, Yesu amezikwa hapa, nimeona hii ni nyumba ambayo sasa hivi imezama kabisa lakini bado ipo. Kwa hiyo, bado Mji Mkongwe wetu wa Zanzibar lazima tuendelee kuuhifadhi kwa nguvu zote.

Mhe. Spika, kuna swali ambalo liliulizwa kesho nadhani kwa majibu ambayo leo mengi yametolewa na mimi nitayatoa na hili ambalo amelitoa Mhe. Samia Suluhu Hassan, yule ambaye ameuliza swali simjui nani inawezekana kabisa akaondoa swali lake. Eneo baina ya *Tembo Hotel* na *Starehe Club*.

Mhe. Spika, ni kweli lile eneo kama wajumbe wengi walivyopendekeza kuna haja ya kuliangalia upya na kulitengeneza likawa eneo la bustani. Kuna Forodhani kubwa tukiacha *Mini Foro* Mombasa, eneo lile ni zuri mno. Wamependekeza kwamba libaki kuwa wazi lakini litengenezwe vizuri sio kama lilivyo leo. Wamesema sasa hivi kuna vigenge tu pale vyengine vya wavuta bangi na wengine. Imani yangu kwamba muda mchache ujao eneo lile litakuwa kivutio kikubwa na inawezekana kabisa watu badala ya kwenda Forodhani wakaja pale. Kwa mchango wa Mhe. Samia Suluhu Hassan pale basi inawezekana pia kwa wakati huo ikawa kuna maingiliano makubwa kati ya *Starehe Club* na lile eneo la pale.

Lakini pia tuna utamaduni wa mashindano yetu ya ngarawa, sasa hivi huwezi ukaiendesha vizuri pale, inawezekana pia mashindano haya ya ngarawa yakawa na kasi mpya na eneo lile watu wakapata fursa ya kwenda pale kuona mashindano hayo.

Kwa hiyo Mhe. Spika, wazo la wajumbe wako wengi kwamba eneo lile sasa liangaliwe upya, lakini pia lile ambalo liko mbele ya *Africa House* wazo lile linakubalika na nina imani kabisa huko mbele tunakokwenda maeneo haya

kuwa katika mapendekezo haya wajumbe wako ambayo wameyasema.
Mhe. Spika, jengine hili ambalo Mhe. Haji Faki Shaali alitaka kujua juu ya kifungu cha 4. Utamaduni uliokusudiwa katika kifungu cha 4 kwa kweli ni watu na historia yao na vilivyowazunguka tangu kuanza kwa Mji Mkongwe wa Zanzibar. Silka, mila na desturi nzuri ambazo zimeupatia sifa Mji wa Zanzibar.

Lakini vile vile ni kweli wajumbe wengi wamekuwa wakizungumza juu ya ule muingiliano uliokuwepo ndani ya Mji Mkongwe sasa hivi na watalii wetu waliokuwepo. Ni kweli kabisa tulipoanzisha masuala haya ya utalii sisemi kwamba hatukuwa makini lakini hamu ilikuwa zimetuzidi. Kwa hiyo, ikawa hatukuweza kuwa makini kuangalia ni utalii wa aina gani tunauhitaji na wapi ukae. Ndio maana hata vinyago sasa vikawepo Mji Mkongwe na vikaenea kila pahala. Mhe. Spika, nina imani kabisa kuja kwa mswada huu pole pole tunaweza tukabadilika na hatimaye Mji Mkongwe ukarudia katika ile historia yake.

Mhe. Spika, kwanza nataka niwapongeze sana Mamlaka ya Mji Mkongwe kwa hatua ambazo wamefikia angalau ya kuanza kulifanyia matengenezo jengo ambalo liko pale Kiponda nyuma ya Wizara ya Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi karibu na Hoteli ya Asumini na hoteli nyengine nimeisahau jina lake.

Mhe. Spika, ninaamini kabisa kama sheria hii ingepitishwa miaka mitano iliyopita basi jengo lile lisingefikia vile. Mswada huu utakapokuwa sheria itaweza kuzuia majengo yale kufikia hali ile. Kwa sababu ni kweli kwamba jengo lile sasa hivi lina hatari na hata ile miega iliyowekewa pale tayari imekwishaoza. Lakini Mamlaka ya Mji Mkongwe imeweza kushirikiana na wale wamiliki wa jengo lile.

Kwa sababu jengo lile ni la familia moja lakini kila mmoja ana eneo lake. Sasa katika hali hiyo inakuwa tabu kidogo huyu anataka ufanye hivi, huyu mnyonge. Lakini wameweza kushirikiana na angalau wameweza kuanza kulifanyia matengenezo na kuweza kulihami lisiweze kuanguka. Nina imani kila baada ya muda wataweza kushirikiana hatimaye jengo lile litaweza kuwa salama kama ilivyokuwa.

Mhe. Spika, binafsi mimi nakubaliana na mawazo ya baadhi ya wajumbe juu ya eneo la Bwawani. Eneo la Bwawani limejigawa katika maeneo mawili, nusu ya Bwawani ipo katika eneo la Mji Mkongwe pamoja na *buffer zone* ile na eneo lililobaki halimo.

Lakini ni kweli Mhe. Spika, lazima tufike pahala wizara zetu mbili zikae ziangalie. Kwa sababu wenzetu wengine hawako tayari kuona pale panafukiwa na wanazo hoja zao za msingi. Hoja kubwa iliyokuwepo kwamba kuna ndege

wanakuja pale, wanataga pale, wanazaa, *seasonal*. Lakini ndege wale wale hakuna mtu ambaye amewaambia waje pale, wao wenyewe kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa wanajua pakwenda. Ndege wale kwa hapa Unguja wanaweza kuja kwenye Jimbo la Uzini pale Miwani kuna bwawa kama lile na baadhi ya ndege wapo pale.

Kwa hiyo, kama tutamudu kulifukia, tukalitengeneza vizuri eneo lile, tukaweka bustani nzuri inaweza ikashinda hata ile Forodhani. Kwa hiyo, hili ni wazo zuri tuliangalie ingawa lina gharama zake. Ni gharama kubwa kufukia pale lakini hakuna lisilowezekana. Safari ya maili elfu huanzwa kwa hatua moja.

Mhe. Spika, jengine kuna suala hili la kufanya ukaguzi wa majengo haya ambalo nadhani limezungumzwa na Mhe. Nassor Ahmed Mazrui. Mhe. Spika, napenda nimthibitishie Mhe. Mazrui na Wajumbe wako kwamba kwa kweli wenzetu wa Mamlaka ya Mji Mkongwe wamekuwa wakifanya ukaguzi wa mara kwa mara katika majengo haya na kutoa ushauri juu ya nini cha kufanya. Hata wale wenye majengo haya ambao wanayamiliki wao wenyewe pia huwa wanakwenda Mji Mkongwe kwa ajili ya kupata maelekezo juu ya mambo mbali mbali.

Lakini kuna jambo moja ambalo sasa hivi labda wale Mhe. Nassor Ahmed Mazrui na wenziwe ambao wako Mji Mkongwe ambao wanajivunia Mji Mkongwe wakiwa wazaliwa wa pale. Mji Mkongwe kama walivyosema una milango tu tunayoiita *Zanzibar Doors* baadhi yake ilikuwa na shaba lakini sasa hivi shaba zile imekuwa ni balaa. Karibu milango yote ambayo ilikuwa na shaba sasa ina tundu.

Mhe. Spika, juzi nilipita katika jengo lililoungua lililopo nyuma ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya zamani, jengo lile lilikuwa na shaba katika mlango wake lakini nimekuta imebakia shaba moja tu zote zimeibiwa. Sasa hili ni tatizo.

Kwa hiyo, hata watalii kuna baadhi ya mambo wanakuja kuyaangalia unayakuta nayo yako kasoro kasoro. Sasa hili nadhani tushirikiane kuwakamata watu hawa na hasa wale wanaonunua ambao wanachangia kuharibu ile haiba ya Mji Mkongwe. Milango yote ile ambayo mtalii anakuja makusudi kwa ajili ya kwenda kuiangalia ile tu lakini akenda pale haikuti. Mhe. Spika, hili ni jambo ambalo linakera kwa hiyo tutoe taaluma tushirikiane na wenzetu kuona yale mambo ambayo yana umuhimu wake basi tuyahifadhi.

Mhe. Spika, jambo jengine nalo hili wenzetu wa Mamlaka ya Mji Mkongwe wanajitahidi lakini wakaazi wa Mji Mkongwe pamoja na kama wenyewe watu wa Mji Mkongwe mnavyojiita, lakini kuna mambo mengine ifike pahala

tukwambieni kwamba si ustaarabu maeneo ambayo yanasafishwa na Mamlaka ya Mji Mkongwe kwa ajili ya watalii baadae yanageuzwa jaa.

Kwa mfano, hapa kwenye jengo la *Tip Tip*, kuna kaburi la *Tip Tip* huwa linatengenezwa vizuri panasafishwa lakini ukipita baada ya mwezi ni watu wa Mji Mkongwe ule ule ndio wanageuza jaa. Sasa ombi langu kwa wakaazi wa Mji Mkongwe maeneo kama hayo ya *Tip Tip* tuyahifadhi vizuri na tusirudie kwenda kutupa taka pale. Kwa sababu watalii wanakwenda kuangalia kaburi la mtu maarufu *Tip Tip* na jengo lake liko pale, lakini sasa badala ya kuangalia kaburi anakwenda kuangalia jaa. Hili si jambo lenye kupendeza.

Mhe. Spika, baadhi ya wajumbe wako na ni jambo ambalo linakubalika wamezungumzia juu ya suala la Uwanja wa Mnazimmoja. Ni kweli uwanja huu sote tunaufahamu umo ndani ya eneo la Mji Mkongwe lakini sasa hivi umepoteza hasa ile haiba yake.

Mhe. Spika, sote tunakubali kwamba hapo zamani siku za mvua za vuli wakati wa sikukuu ya Mfunguo Tatu uwanja ule huwa unafurika maji ndio sikukuu inafanyika kwa kule mbele. Lakini mvua ya siku moja tu uwanja ule sasa haufai tena. Kwa mfano, mvua ya juzi tu uwanja ule umejaa maji. Kwa hivyo ninayo imani kwamba mamlaka ya hifadhi ya mji mkongwe kwa kushirikiana na manispaa wataweza kuangalia utaratibu gani ili haiba ya mnazi mmoja irudi kama ilivyokuwa zamani, au hata zaidi badala ya sasa hivi mvua ya siku moja

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri, wajumbe wanataka waziri aje amalize kazi. Kwa hivyo, malizia kwa muda mchache wa dakika kama mbili tu.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Ahsante Mhe. Spika. La mwisho Mhe. Spika, na hili pia naomba tusaidiane, wenzetu wa mamlaka ya mji mkongwe sasa hivi pamoja na barabara nzuri zilizojengwa mule ambazo Mhe. Ame Mati wakati huo aliziita barabara za visahani. Lakini watu wanaiba mafuniko yale ya makaro, ambayo ni hatari na kwa hivyo tatizo litaendelea kuwepo. Kesho tutatengeneza mafuniko siku ya pili yake yanaibiwa.

Mhe. Spika, baada ya hayo nasema naunga mkono tena hoja ya mswada huu. Ahsante. *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, nakushukuru sana na nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yao ambayo itaufanya mswada huu kuwa bora zaidi .
Mhe. Sika, hoja ya wizara yangu imechangiwa na wajumbe 13 na mheshimiwa mmoja Mhe. Mahmoud Thabit Kombo amechangia kwa maandishi, kwa hivyo kufanya jumla yao kuwa 14. mjumbe wa mwanzo ni;

1. Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu
2. Mhe. Hamad Masoud Hamad
3. Mhe. Ali Suleiman Ali
4. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
5. Mhe. Haji Faki Shaali
6. Mhe. Ali Denge Makame
7. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui
8. Mhe. Najma Khalfan Juma
9. Mhe. Said Ali Mbarouk
10. Mhe. Zakiya Omar Juma
11. Mhe. Haji Mkema Haji
12. Mhe. Samia Suluhu Hassan
13. Mhe. Tafana Kassim Mzee
14. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo

Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru sana Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa mchango wake wa kina ambao umenipunguzia kazi. Amefanya kazi kubwa ya kujibu hoja nyingi za wajumbe na kutoa hasa maana na tafsiri ya urithi na uendelezaji urithi, utamaduni, silka na kadhalika, kwa zama za kale na hali halisi ambayo tunakwenda nayo hivi sasa, nina mshukuru sana.

Pia nimshukuru Mhe. Tafana Kassim Mzee kwa kujibu takriban hoja zote za Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Spika, nikianza na Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu, nimshukuru zaidi kwanza kwa nafasi yake ya uenyekiti na kazi kubwa tuliyoifanya wakati kamati yake inapitia mswada huu na marekebisho mengi na ya msingi ambayo umefanyiwa mswada huu na hatimaye leo kazi ya wajumbe kuupitia imekuwa ni nyepesi mno, namshukuru sana Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu.

Namshukuru pia kwa pongezi na maelekezo ambayo ameyatoa wakati akichangia hoja hii, hasa hili eneo lililobaina ya Hoteli ya Tembo na Starehe *Club*. Wengine wanasema Tembo Hoteli, mimi nimetanguliza kusema Hoteli ya Tembo.

Mhe. Spika, kama alivyojibu Mhe. Samia Suluhu kwamba ni kweli Starehe *Club* ni hazina na ni kwa siku nyingi sana, matumizi yake pengine hayakuwa sawa na hali halisi na mazingira ya uwekezaji hivi sasa. Juhudi za serikali za kupunguza umaskini kwa upande mmoja na kutafutia vijana wetu ajira na upande wa pili kwamba eneo liko ndani ya mji mkongwe. Pia juhudi za serikali za kulinda desturi nzuri za Wazanzibari na utamaduni wetu nalo linakwenda kinyume na hali halisi ya mazingira hayo.

Mhe. Spika, eneo lililokuwa wazi ubavuni mwa Starehe Club kama tunavyoelewa miaka mingi sana eneo lile walipewa Serikali ya Oman kwa ajili ya ujenzi wa ubalozi, lakini wakalitelekeza kwa miaka mingi sana. Kwa kweli hali ile kwa kiasi kikubwa imechangia hali ya pale kuzidi kuwa mbaya zaidi. Lakini baada ya kuombwa na serikali kwamba kwanza kwa usalama na hadhi ya ubalozi pale hapafai na wamepewa eneo jengine Mazizini na eneo lile sasa wameliachia.

Lakini nakubaliana na Mhe. Nyonje kwamba ipo haja ya Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kukaa pamoja na kutafakari kwa kina, ili kuweza kuishauri serikali juu ya namna bora ya kutumia eneo lile kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, nikiendelea nije kwa Mhe. Hamad Masoud Hamad na yeye namshukuru sana kwa mchango wake, akiwa Waziri Kivuli na pia ni makamo mwenyekiti wa kamati hii. Nakubaliana na pendekezo lake la kutaka kuongeza kifungu cha 38(b) ni jambo la msingi sana na tunalikubali. Alitaka kifungu hicho kisomeke kama hivi ifuatavyo;

Kwa maana ya waziri, kina utangulizi wake.

Kifungu cha 38(b)

> “Atakuwa na uwezo wa kupiga marufuku matumizi ya jengo eneo lolote la serikali katika mji mkongwe, endapo ataona matumzi hayo yanaharibu sifa ya Zanzibar. Kwa hivyo, tunakubaliana naye na mapendekezo hayo, kwa maana tunaamini yanazidi kuimarisha au kufanya mswada huu uwe bora. Yeye pia alilizungumzia hili eneo la Starehe Club na eneo la wazi. Hilo pia nimeshalijibu.

Namshukuru sana Mhe. Ali Suleiman Ali kwa mchango wake ambao umejaa hekima na maelekezo juu ya mazingira ya hali halisi ya mji mkongwe wa leo. Tunapokea maelekezo hayo na tunamuahidi kwamba yote aliyotueleza tutayazingatia na kuyafanyia kazi ipasavyo. Tunapokea hongera na shukurani zake kwa kazi tuliyoifanya ya bustani ya Forodhani.

Mhe. Spika, naomba nichukuwe fursa hii kwamba kazi za awali za ukingo wa bahari unaoanzia Forodhani kuelekea mkahawa wa Mercury zimeshaanza. Kwa hivyo, tayari timu ya benki ya dunia na wataalamu kutoka Agakhan Trace for Culture wapo hivi sasa na pengine tunategemea Mwenyezi Mungu akipenda mambo yakienda sawa, mwezi wa Juni tutaingia mikataba rasmi na kazi ya kurekebisha ile hali, kwa maana ukingo ule utavutwa kwenda baharini kwa mita 4 hadi 5 kuwa na eneo la wapita njia na watawekewa ma-*bench* yale ya

kukaa. Hata barabara nayo itapanuliwa ili pawe na nafasi ya wale wanaopita kwa miguu, kupata nafasi pia ya kupunga upepo na kujionea mandhari ya bahari, wanaokoga pwani, wanaokaa pale ili kuwe na nafasi ya kutosha kupita magari. Kwa hivyo, tunategemea mwezi wa Juni Mwenyezi Mungu akipenda kazi hiyo itaanza.

Mhe. Spika, kuna matumaini makubwa sana kwamba yale aliyozungumza Mhe. Najma ya kulinda, hata aliyozungumza Mhe. Nassor Ahmed Mazrui ya kulinda huu ukuta. Kuanzia Mercury pale mpaka maeneo ya Ikulu huku na kuimarisha maeneo mengine ya mji mkongwe. Hayo pia kuna matumaini makubwa kwamba Benki ya dunia na Agakhan Trace for Culture watashirikiana na sisi katika kuyatekeleza. Kwa hivyo, vijana wa mamlaka ya hifadhi ya mji mkongwe wanaendelea kuyazungumza na kuyafanyia kazi hayo.

Mhe. Spika, Mhe. Suleiman Hemed Khamis na yeye tunamshukuru sana kwa maelekezo na pongezi zake. Mhe. Haji Faki Shaali alizungumzia vifungu vinavyo kinzana, kwamba maelezo ya vifungu na maelekezo ya vifungu ndani ya mswada na hili amelizungumza Mhe. Nassor Mazrui na Mhe. Said Ali Mbarouk.

Ni kweli Mhe. Spika, lakini kwa bahati mbaya marekebisho ya kamati tumeyapata leo asubuhi. Lakini yote mliyoyazungumza yamefanyiwa marekebisho na kamati. Ndio maana mtaona marekebisho safari hii kutokana na uandishi wa mswada wenyewe ni mengi mno. Lakini yote yamezingatiwa na kufanyiwa marekebisho na Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Kwa hivyo, ninaomba niwaelekeze kwenye marekebisho haya ya kamati ambayo wizara imeyapokea na kuyakubali na hoja zenu zote zimejibiwa na marekebisho ya kamati.

Mhe. Haji Faki Shaali aliuliza utamaduni wa mji mkongwe ni upi? Kwanza Mhe. Spika, utamaduni ni watu, historia yao na vilivyowazunguka tangu asili huko. Pia vikihusisha silka, mila na desturi nzuri. Kwa hivyo, utamaduni wa mji mkongwe ni ule ambao umeanzia huko ulipoanza mji mkongwe hadi hii leo. Lakini kwa mnasaba wa yale uliyoyazungumza wewe, zile desturi nzuri na yale mbayo tumetokana nayo ambayo ni mema na ambayo yanatufaa, basi hayo tunayahesabu kama ndio utamaduni wetu sisi.

Mhe. Spika, wengi wamezungumza hapa haya mambo ya vinyago na mambo mengine. Ule sio utamaduni wetu, hatuwezi kuukubali, sio wa kwetu na hautokuwa wa kwetu na ili kuulinda wa kwetu ni lazima tuusemee na tuukemee na tufanye kila jitihada kuuzuia. Kwa sababu tukiuachia baada ya miaka 10 au 20 utakuwa ni wa kwetu. Vinyago utakuwa ni sehemu ya utamaduni wetu, kwa sababu ndivyo utamaduni unavyokwenda. Kwa sababu tuliyokuwanayo leo na

watakujanayo watoto wetu utakuwa sasa ukiunganisha na ya kale ndio sehemu ya utamaduni wa miaka 20 au 30 au 50 na kuendelea mbele huko.

Kwa hivyo, ninaungana na wajumbe. Hili limesemewa na wajumbe takriban wote waliosimama kuchangia, kwamba utamaduni ambao sio wa kwetu hasa huu wa tinga tinga vinyago na mambo mengineyo, basi lazima tufanye jitihada ya kuweza kuuzuia. Kama alivyotoa ufafanuzi Mhe. Samia Suluhu Hassan ni kwamba mswada huu ambao tumeuleta kwenu sasa utatoa fursa kwa mamlaka ya hifadhi ya mji mkongwe kuchukua hatua za uhakika kuhifadhi utamaduni huo kwa mujibu wa malengo na maelekezo ya UNESCO.

Kwa hivyo, nafasi hiyo na meno hayo tunayo, kwa sababu hata kwenye hotuba yangu nilisema mkishakuupitisha tutakuwa na meno ya kufanya hayo ambayo mmeyazungumza. Meno hayo tukiyaona si makali ya kutosha, basi ipo haja pia kwa siku za mbele baada ya kuzingatia utekelezaji wa sheria hii kuyafanya makali zaidi na makubwa zaidi. Lakini kwa haya kwa hatua hii, mimi nina imani ya kwamba tunaweza tukaanza kuchukua hatua zilizokuwa madhubuti.

Mhe. Haji Faki Shaali pia alitaka kujua nini tafauti baina ya kazi na majukumu? Kwanza kama nilivyokueleza mheshimiwa zile *marginal note* zimerekebishwa na marekebisho yaliyofanywa na kamati, kwa hivyo zote ziko sawa baada ya marekebisho. Kwa hivyo, hoja yako kwa mantiki hiyo ilikuwa ni sahihi kwa maelezo, lakini marekebisho yameshafanywa.

Mhe. Spika, nikijibu hoja hiyo ya Mhe. Haji Faki Shaali kwamba majukumu ni kazi kwa ujumla wake, lakini kazi ni shughuli za kila siku na kule marekebisho yameshafanywa katika *marginal note* kama ulivyotaka iwe. Hiyo pia ni hoja yako ile ya kifungu cha 11(d) ambayo imerukia kwenda kifungu cha 11(2) navyo hivyo vimefanyiwa marekebisho na kamati kwa kuviweka sawa.

Pia ulizungumzia kuna haja gani ya kutaja posho za bodi na sheria hii ya mitaji ya umma. Sheria ya mitaji ya umma ndio inayoelekeza juu ya namna bodi inafanya shughuli zake, muundo wake, marupurupu na masuala mengineyo. Kwa hivyo, kuitaja sheria hiyo kutokana na kupata maelekezo wakati wa utekelezaji wa sheria na bodi kufanya shughuli zake ni jambo la msingi, ambapo tunafanya kwenye sheria zote ambazo tunaziandika na kuzileta huku Barazani. Kwa hivyo, nakuomba mheshimiwa ukubaliane na sisi.

Vile vile hata lile ulilozungumza la karatasi za mizania, ulikuwa sahihi ni karatasi za mizania. Nalo hilo limefanyiwa marekebisho kwa kina kabisa. Pia hili la mwanasheria wa bodi nalo limefanyiwa marekebisho. Kwa hivyo, yote yale uliyoyaona yale kwa kweli kamati nayo imeyaona na kuyafanyia marekebisho na imekubaliana na yale mawazo ambayo umeyatoa wewe.

Mhe. Spika, Mhe. Ali Denge Makame na yeye tunamshukuru sana kwa mchango wake, tunakubali hoja yake ya kwamba kuwe na maelekezo ya angalau mara moja kwa kila baada ya miaka mitano, kwa zile rangi ambazo zinakubalika ndani ya mji mkongwe basi wamiliki wake wafanye jitihada hizo.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui na yeye tunamshukuru sana kwa mchango wake. Narudia kueleza kwamba Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi imefanya marekebisho kwenye maeneo yote yale ambayo ameyagusia. Alizungumzia mamlaka kupewa hati miliki ya majengo ambayo yako chini ya usimamizi wake. Hilo nalo sio tatizo ni jambo la msingi kabisa. Pia alizungumzia waziri kutoa uwezo wake kwa maana kukasimu mamlaka yake, kwamba lifikiriwe upya.

Mhe. Spika, kwa hapa tulikusudia kwamba pale waziri anapoona kwa jambo makhususi na kwa muda maalum kuweza kukasimu hivyo. Lakini si jambo ambalo ni rahisi kufanyika, lakini linampa fursa tu waziri ya kuweza kukasimu madaraka yake, lakini limefikiriwa kwa kina na si jambo rahisi kwa kutendeka. Si rahisi kumuona waziri ana kasimu madaraka yake, lakini ni kutoa ile fursa tu ya kuweza kufanya hivyo kwa mambo maalum ambayo atahisi haitoathiri na yeye pia mamlaka yake ya kikazi ambayo kwa mujibu wa sheria anakabidhiwa yeye peke yake, kwa sababu kuna kazi za waziri hawezi kufanya mtu mwengine yeyote, hizo haziwezi kukasimiwa.

Mhe. Spika, kuhusu suala la mmong'onyoko wa ukinga wa bahari nimelijibu. Wengi walizungumzia pia usafi wa mji mkongwe. Tunakubaliana nanyi Waheshimiwa Wajumbe na jitihada makhususi zitafanywa tukishirikiana na manispaa ya Zanzibar, ili kuona hali hiyo inabadilika na sheria pia inatoa fursa zaidi kwa hayo.
Mhe. Mazrui vile vile alizungumzia juu ya majengo ambayo hayakutaifishwa na serikali na wenyewe wapo ili warudishiwe wenyewe, kwamba majengo hayo yaliandikwa tu usajili wa nyumba.

Mhe. Spika, naomba nitowe ufafanuzi juu ya utaifishwaji. Utaifishwaji wa mali usiohamishika una sehemu mbili. Sehemu moja ni zile mali au mashamba yaliyotangaziwa kwenye gazeti rasmi la serikali. Tafsiri ya pili ni mali au mashamba yaliyokhodhiwa pia na kutumiwa na serikali. Kwa hivyo, nyumba zilizokhodhiwa na serikali zinahesabika kwamba zimetaifishwa. Lakini sera ya taifa ya makaazi tuliyoipitisha hapa Barazani, sasa yale tumeyabadilisha kwa maana imetoa fursa kwa serikali kuweza kuuza mali zake kwa pale inapoona inafaa. Lakini Baraza hili liliagiza kwamba kwanza tuanze na nyumba hizi za vijijini, ili tuone zoezi linavyokwenda na hatimaye sasa kuhamia kwenye maeneo ya mji. Hayo pia ni maelekezo ya Baraza la Mapinduzi. Kwa hivyo, tunaelekea huko.

Kwa hivyo, hiyo pia inajibu hoja ile iliyozungumzwa na wajumbe wengine kwamba kutokuwa na uwezo wa serikali na wananchi pia kuweza kumiliki au kwa maana ya kutunza majengo hayo. Tunaamini kuwa wakati huo ukifika hali hiyo itaondoka wenyewe kwa maana yatawekwa kwenye soko na wanaoweza kuyamiliki watamiliki kwa mujibu wa utaratibu na sheria za nchi yetu.

Mhe. Najma Khalfan Juma na yeye tunamshukuru sana kwa nasaha zake na maelekezo. Nyingi ya hoja hizo alijibu Mhe. Samia Suluhu Hassan, na mimi nimetangulia. Lakini hii hoja yake ya siku ya mji mkongwe nayo imeungwa mkono na wajumbe wengi na sisi pia tunaikubali, tunaona ipo haja ya kutangazia hasa kuwe na siku ya mji mkongwe, kwa mapendekezo uliyotoa wewe Mhe. Najma na yaliyoimarishwa zaidi au kufanywa yawe bora zaidi na Mhe. Samia. Kwa hivyo, hilo tutalizingatia na tuna amini lina maslahi na nchi yetu.

Mhe. Spika, wajumbe wengi walizungumzia pia hii *Satellite town's* za kale, yaani hii miji midogo midogo iliyokuwa kwenye manispaa au halmashauri ya kisiwa cha Unguja na kwengineko tunaifanyaje? Sheria hii imejikita zaidi katika eneo la mamlaka ya hifadhi ya mji mkongwe. Maeneo yale yana sheria ambayo iko chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inayosimamiwa na Mhe. Haroun Ali Suleiman na Idara ya Mambo ya Kale. Kwa hivyo, naamini na yeye akipata nafasi, nafikiri mara kadhaa hapa katika marekebisho ya sheria na mengineyo, amekuwa akiyazungumza kwa kina juu ya mikakati ambayo wizara yake inayo kwa kutunza maeneo yale.

Mhe. Said Ali Mbarouk tunamshukuru na yeye kwa mchango wake na zile hoja zake nyingi tumezijibu kama nilivyoeleza kwenye marekebisho yaliyofanywa na kamati. Kifungu cha 45(1) alichokizungumzia hicho nacho kimefutwa na kamati.

Vile vile alizungumzia kwamba mji wa Mascut nao umeachana na mji wao mkongwe. Hiyo sio sahihi. Mji mkongwe nao nafikiri walishindwa na waliona bukhudha zile sheria na maelekezo na masharti ya UNESCO, basi wakaamua kujitoa wao wenyewe. Lakini hifadhi ya mambo yao ya kale nafikiri nchi moja ambayo kwa kweli wako makini sana nafikiri ni Mascut, kwa maana Oman yenyewe. Wale kwa kweli kwa mambo yao ya kale na historia yao wako makini sana, wanaitunza, wanaitangazia, wanavutia na wanaithamini historia yao. Hata ukiona maandiko na mengineyo utaona kwamba ni watu waliokuwa na umakini sana kwa kulinda masuala yao.

Mhe. Spika, Mhe. Zakiya Omar Juma tunamshukuru kwa mchango wake mkubwa alioutoa kwenye kamati kwanza na tunashukuru kwamba hiki kifungu ambacho wengi tulipitikiwa nacho tunakubali kwamba ni sahihi kama

alivyoelekeza. Kwa hivyo, pale kwenye ufafanuzi kisomeke kifungu cha 3 na sio 4. tunamshukuru sana.

Pia alizungumzia vinyago kwa hisia. Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji na mimi tunakubaliana na yeye. Kuhusu Jamhuri *Garden* nayo tumeyasikia na tutayaendeleza katika mipango yetu.

Tunamshukuru sana Mhe. Haji Mkema Haji kwa maelezo yake na ufafanuzi juu ya mazingira ya mji mkongwe akiwa mkaazi wa miaka mingi wa mji huo mkongwe, ametusaidia sana kuweza kuelewa mengi. Hoja yake ya matumizi ya vifaa vya asili, kulinda uwasilia wa mji mkongwe wenyewe ni jambo la msingi na limepewa nafasi kubwa kwenye sheria hii. Tunamshukuru kwa kuliona hilo na litaendelea kuwekewa mkazo.

Kuhusu *traffic plan* aliyoizungumzia kwamba ipo haja ya zile njia za asili ili kuendelea kuulinda ule uasilia wenyewe, tuzizingatie gari za aina gani zinaweza kupita humo badala ya kuweza kuziba na kuondosha ule uasilia wenyewe. Nalo hilo tutalizingatia zaidi katika *traffic master plan*. Naliona ni jambo la msingi katika kuhifadhi na kuendeleza. Kwa hivyo, linapaswa kupewa kipaumbele.

Vile vile amezungumzia umuhimu wa kuwa na mashirikiano ya karibu zaidi kwenye yale mambo matano makuu aliyozungumza. Kwa mfano utalii, uvuvi na mawasiliano. Hilo limedhihirika baada ya mchango wa Mhe. Samia Suluhu, ni sahihi kwamba kwa maeneo hayo ni lazima mashirikiano yawepo na yawepo ya hali ya juu, hapo tu tutakapoweza kufikia katika malengo ambayo tumeyakusudia.

Mhe. Spika, pia alizungumzia katika kifungu cha 8 yeye anavyotafsiri kwamba kinamuondoshea maslahi mtumishi wa mamlaka kwa maana mjumbe wa bodi au mtumishi wa mamlaka yenyewe haki ya kujitaftia rizki. Mhe. Spika, kifungu hiki hakimzuwii mtumishi wala mjumbe wa bodi kufanya shughuli mbali na zile alizokuwanazo kwenye bodi na utumishi wake wa mamlaka, ana uhuru wa kutafuta. Lakini kifungu hiki kinazungumzia kwamba kile kipindi ambacho ataacha kazi kwenye mamlaka, asubiri basi miezi 12, naamini kwamba kamati ilifanya marekebisho ikaweka miezi 6 ili hapo aweze kuingia mkataba na mamlaka kwa shughuli zake binafsi. Lakini kipindi cha huko nyuma hakuna jambo au kitu kinachomzuia kutafuta rizki kwa njia nyengine yoyote ile nje ya utumishi ambao amekua nao ndani ya serikali, kwa sababu hata serikali yenyewe inaruhusu hivyo.

Mhe. Spika, baada ya majumuisho hayo ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na ninawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kunisikiliza. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Basi niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaoafiki hoja ya Mhe. Mjumbe wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Kufuta Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe na Kuanzisha Sheria mpya ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe pamoja na Mambo mengine Yanayohusiana na hayo

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza zima ili kuupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Sehemu ya Kwanza
Utangulizi

Kifungu cha Kwanza	Jina Fupi na Kuanza Kutumia
Kifungu cha pili	Ufafanuzi Pamoja na Marekebisho yake

Sehemu ya Pili
Mamlaka

Kifungu cha Tatu	Kuanzishwa kwa Mamlaka pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha Nne	Majukumu ya Mamlaka pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha Tano	Hadhi ya Kisheria ya Mamlaka pamoja na Marekebisho yake.

Kifungu cha Sita	Majukumu ya Mamlaka pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha Saba	Kazi za Mamlaka.
Kifungu cha Nane	Muundo wa Mamlaka pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha Tisa	Mkurugenzi Mkuu pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha Kumi	Mkurugenzi, Washauri Waelekezi na Wafanyakazi wengine pamoja na Marekebisho yake.

Sehemu ya Tatu
Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka

Kifungu cha Kumi na Moja	Kuanzishwa Muundo wa Bodi ya Wakurugenzi pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha Kumi na Mbili	Uwezo na Kazi za Bodi pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha Kumi na Tatu	Kuvuliwa Ujumbe pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha Kumi na Nne	Makamo Mwenyekiti pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha Kumi na Tano	Muda wa Uteuzi pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha Kumi na Sita	Katibu.
Kifungu cha Kumi na Saba	Vikao vya Bodi pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha Kumi na Nane	Koramu ya Kikao pamoja na Marekebisho yake.

Kifungu cha Kumi na Tisa	Kumbukumbu za Vikao vya Bodi pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha Ishirini	Maamuzi ya Bodi pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu cha 21	Mhuri Rasmi wa Mamlaka pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 22	Mwenendo wa Bodi kutokanguliwa.
Kifungu cha 23	Kushindwa kuhudhuria vikao vitatu Mfululizo vya Bodi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 24	Bodi kujipanga shughuli zake wenyewe pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Nne
Uwezo na Shughuli za Mamlaka

Kifungu cha 25 -

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana, kuna kitu kimoja ambacho ni muhimu kwetu sote bahati mbaya Mhe. Waziri wakati alipofanya majumuisho hakukizungumzia.

Wakati nilipokuwa nikichangia kuhusu uwezo wa Mji Mkongwe nilizungumza kitu ambacho sina uhakika nacho na nilitaka alisaidie Baraza lako tukufu kuhusu Gati mpya ya Bodi, kwamba jengo limevunjwa lakini ule ukuta wa nje haukuvunjwa ambao nadhani kama ungevunjwa basi tungepata *parking* nzuri ya magari yetu.

Vile vile nilisema kwamba hivi sasa watu naoweza kuingia na gari ndio hao wanaopita kwenye mlango wa Mamlaka ya Bandari, lakini si gari zote ambazo zinaruhusiwa kuingia kwenye mlango ule. Isipokuwa kuna taarifa ambazo si rasmi kwamba pale ukuta hauwezi kuvunjwa kwa sababu Mamlaka ya Mji Mkongwe hawataki na itaharibu mandhari ya Mji Mkongwe. Sasa suala hili nadhani Mhe. Waziri hakulijibu, kwa hiyo naomba atusaidie.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Mwenyekiti, ni sahihi kwa Mamlaka ya Mji Mkongwe kukataa kwa maana ndio kazi yake, kuhifadhi na kuendeleza na tumewapa majukumu hayo. Kwa maana kila maamuzi

yanayofanywa lazima yazingatie kwa misingi ya majukumu waliyopewa.
Lakini kama ulivyosema kwamba hakuna sheria iliyokuwa haina *exception*. Kwa hivyo, tunapoona ipo haja ya kuzingatia haya masuala, basi tunaweza kukaa na wahusika kwa ajili ya kuyatizama na kazi hiyo inafanyika. Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, kwa maana ya Shirika la Bandari na Mamlaka ya Hifadhi wa Mji Mkongwe wamekuwa wakiendeleza mazungumzo kuona namna bora ya matumizi ya eneo lile.

Kwa hiyo, jambo hilo lipo na tutaendelea kulipa mkazo na kutizama wapi tunaweza kufanya hiyo *compromise* inayohitajika, kwa ajili ya kukidhi mahitaji yetu ya leo pamoja na majukumu yetu ya uhifadhi wa Mji wetu Mkongwe.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwamba majibu mazuri. Lakini ombi langu kwa sababu pale lile jengo lote limevunjwa umebakia ukuta mmoja tu na kuta nne pamoja na paa vyote vimevunjwa, kwa hiyo ile *structure* pale kwa asilimia 75 haipo tena. Kwa maana hiyo, naomba mazungumzo yao yaende vizuri na wakubaliane ule ukuta uvunjwe kwa ajili ya kupata parking ya magari.

Ahsante sana naomba tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, tayari wizara zetu mbili tumeshakubaliana na kupata ruhusa kutoka Mamlaka ya Mji Mkongwe, kwamba pale ndani tupatengeneze vizuri. Isipokuwa tulikuwa na tatizo la lami, lakini hivi sasa lami tayari imeshafika nchi na muda wowote tutanza kutia lami na gari zitaweza kutumia sehemu ile bila ya matatizo yoyote *(Makofi)*.

Kifungu cha 25	Uwezo wa jumla pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 26	Uwezo wa kuingia kwenye jengo na kutoa notisi na amri ya kusimamia pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 27	Uwezo wa kufanya mapitio pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 28	Uwezo wa kupata taarifa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 29	Uwezo wa kufanya uchunguzi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 30	Mashauriano na wadau na serikali pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 31 Kuhifadhi siri pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Tano
Uwezo na Utekelezaji

Kifungu cha 32 Majumba yaliyohamwa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 33 Uwezo na utekelezaji pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 34 Kufutwa kwa mkataba na madhara yake pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 35 Utekelezaji wa amri pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 36 Miongozo inayotolewa na Mamlaka pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 37 Kanuni.
Kifungu cha 38 Uwezo wa waziri pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 39 Makosa.
Kifungu cha 40 Adhabu pamoja na marekebisho.
Kifungu cha 41 Adhabu ambayo haukutajwa pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Sita
Masharti ya Fedha

Kifungu cha 42 Fedha za Mamlaka pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 43 Kodi ya adhi malipo na kodi na jengo ya eneo pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 44 Fedha za hifadhi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 45 Bajeti ya ziada.
Kifungu cha 46 Bajeti pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 47 Ukaguzi matumizi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 48 Ripoti ya mwaka.

Sehemu ya Saba
Masharti ya Jumla

Kifungu cha 49 - Kubakiza na kufuta.

Kifungu cha 50 - Masharti ya kurukia pamoja na marekebisho yake.

Baraza lilirudia

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Baraza Zima imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali bila ya mabadiliko yoyote pamoja na masahihisho. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda *(Makofi)*.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe, 2010

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe 2010 usomwe mara ya pili.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubali mswada huu katika kusomwa mara ya pili wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda *(Makofi)*.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya pili na kupitishwa)

Katibu Mezani: Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Mswada wa

Kufuta Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe na Kuanzisha Sheria mpya ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe pamoja na marekebisho yake na mambo mengine yanayohusiana na hayo, sasa umepitishwa rasmi na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar *(Makofi)*.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni kwa mashirikiano makubwa katika kutekeleza shughuli zetu za kila siku.

(Saa 1:40 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 26/03/2010 saa 3:00 asubuhi)